

**MCHANGO WA NYIMBO ZA MICHEZO YA WATOTO KATIKA KUKUZA
MAADILI YA JAMII YA WAPEMBA**

RIZIKI OMAR NASSOR

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA
KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (FASIHI) YA
CHUO KIKUU HURIA TANZANIA**

2016

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma kazi hii na anapendekeza kuwa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kukubali kupokea tasnifu hii inayoitwa:

Mchango wa Nyimbo za Michezo ya Watoto katika Kukuza Maadili ya Jamii ya Wapemba, ikiwa ni Sehemu ya Masharti ya Kupatiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili (Fasihi) ya Chuo Kikuu Huria Tanzania.

.....
Profesa, Dkt, Sk, Mwl. T.Y.S.M Sengo

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile Tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile Kieletroniki, Kurudufu nakala Kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya Mwandishi au Chuo Kikuu Huria Kwa Niaba.

TAMKO

Mimi, **Riziki Omar Nassor** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni yangu mwenyewe haijatolewa na haitotolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyingine ambayo ni sawa au karibu sawa na hii katika chuo kikuu chengine.

.....

Sahihi

.....

Tarehe

TABARUKU

Kazi yangu hii ninaitabaruku kwa watoto wangu iwe ni chachu kwao ya kupata
elimu kuzidi kiwango alichofikia mama yao.

SHUKRANI

Awali ya yote napenda kumshukuru M/mungu (SW) kwa kunijaalia afya njema na kubahatika kupata nafasi ya kusoma Digirii ya uzamili MA Kiswahili kwa mwaka 2014/2015 kwani wengi hawajapata nafasi hii.

Shukurani zangu pia zimwendee msimamizi wangu Profesa T.S.Y Sengo kwa kusimamia kazi hii mpaka ikakamilika, namshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kumpa taufiki ya kuniongoza mpaka kukamilika kwake.

Napenda pia kuishukuru familia yangu yote kwa kuniunga mkono kwa hali na mali wakati wote nikiwa masomoni, lakini shukurani hizi hasa ziende kwa wazazi wangu Bibi Mwanaidi Khamis Uledi na Bwana Omar Nassor Hamad. Pia ziende kwa walezi wangu, bibi Naima Kombo Zidkheir na Bwana Moh'd Haji Lada, kwa kunipa msingi mzuri wa elimu kuanzia msingi hadi kufikia ngazi hii ya umahiri. Pia zimuendee mume wangu mpenzi Abdalla Khalid Juma na mkwe wangu Khalid Juma kwa msaada wao mkubwa wa kifedha walionipatia.

Vilevile nina washukuru wanafunzi wenzangu tuliosoma kozi hii kwa kipindi chote cha masomo. Hata hivyo haitokuwa rahisi kuwataja wote walionisaidia kwa njia moja au nyengine kwani ni wengi hivyo nimewataja wachache kwa niaba yao. Lakini nitakuwa mwizi wa fadhila endapo nitashindwa kuwashukuru mwalimu Bakar Kombo wa chuo Kikuu Huria Pemba na mwalimu Mussa Khamis kwa msaada wao hadi kufanikisha kazi hii.

IKISIRI

Utafiti huu unachunguza Mchango wa Nyimbo za Michezo ya Watoto Katika Kukuza Maadili ya Jamii ya Wapemba. Tasinifu hii inalenga katika kuonesha mchango unaopatikana kuitia nyimbo za michezo ya watoto kwani kuitia nyimbo hizi jamii inapata kujifunza mengi tu kama vile, uvumilivu kwa wanandoa, uwajibikaji katika kazi, umuhimu wa usafi, nidhamu, umuhimu wa elimu na kadhalika. Hii inatokana na kwamba watu wengi walidhani kuwa hamuna mchango wowote unaopatikana kuitia nyimbo hizi. Mtafiti kwa kutumia nadharia ya uchambuzi matini, nadharia ya mwingiliano matini na mwitiko wa msomaji amefanikiwa kuonesha na kubainisha mchango hasa unaopatikana kuitia nyimbo za michezo ya watoto. Vile vile mtafiti alitumia mbinu ya kuitia machapisho mbali mbali na kwenda maskani Pandani, Uwondwe na Mzambarautakao katika wilaya ya Wete –Pemba kwa ajili ya kukusanya nyimbo, vyanzo vyake na maana zake. Nadharia hizo ndizo zilizomuongoza mtafiti katika uchanganuzi wa data katika utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa nyimbo hizi asili yake haikuwa na lengo la kuburudusha tu kama ilivyokuwa mawazo ya wengi, lakini zilikuwa na lengo zaidi ya hilo kama vile kuelimisha, kuadilisha na kadhalika. Baada ya kuhakiki sampuli ya nyimbo imebainika kuwa nyimbo hizi husawiri maisha ya kinamama, baba na watoto wenyewe ambao mara nyingi ndio waimbaji wa nyimbo hizi katika michezo yao mbali mbali. Ingawa utafiti huu umeegemea upande wa ujumbe zaidi na jinsi fani inavyoibua ujumbe huo lakini bado kuna maeneo mengine ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti kuitia nyimbo hizi. Maeneo wenyewe ni kama vile ni jinsi gani sayansi na teknolojia (ugen) unavyoadhiri nyimbo za michezo ya watoto na pia kuangalia muundo wa nyimbo hizo.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKIMILIKI	iii
TABARUKU	v
SHUKRANI.....	vi
IKISIRI	vii
ORODHA YA VIAMBATANISHO.....	xiv
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti.....	1
1.3 Asili ya Nyimbo za Michezo ya Watoto	3
1.4 Tatizo la Utafiti	7
1.5 Malengo ya Utafiti	7
1.5.1 Lengo Kuu	7
1.5.2 Malengo Mahasusi	8
1.6 Maswali ya Utafiti.....	8
1.7 Umuhimu wa Utafiti.....	8
1.8 Mpangilio wa Kazi ya Utafiti	9
1.9 Hitimisho	9
SURA YA PILI	11
MAPITO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA	11
2.1 Utangulizi	11

2.2	Maandiko Kuhusu Asili na Maana ya Nyimbo	11
2.2.1	Asili ya Nyimbo	11
2.2.2	Maana ya Nyimbo	11
2.2.3	Maandiko kuhusu Uanishaji wa Nyimbo	14
2.2.4	Kazi na Maandiko kuhusu Nyimbo.....	15
2.2.5	Maandiko kuhusu Nyimbo za Michezo ya Watoto.....	15
2.2.6	Fasili ya Fani na Maudhui	17
2.3	Kiunzi cha Nadharia.....	18
2.2.1	Nadharia ya Uchambuzi Matini	18
2.3.2	Nadharia ya Mwingiliano Matini	20
2.3.3	Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.....	22
2.3.4	Misingi ya Nadharia ya Mwingilianomatini na Uchambuzi Matini	23
2.3.5	Misingi ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji	24
2.3.6	Umuhimu wa Nadharia Hizi katika Tasnifu Hii	24
2.3.7	Hitimisho	25
SURA YA TATU.....	26	
MBINU ZA UTAFITI.....	26	
3.1	Utangulizi	26
3.2	Njia za Kukusanya Data	26
3.3	Mbinu za Ukusanyaji wa Data.....	27
3.3.1	Mbinu ya Usaili.....	27
3.3.2	Mbinu ya Ushuhudiaji	28
3.3.3	Mbinu ya Kimaktaba	28
3.4	Vyanzo vya Data.....	29

3.5	Zana na Vifaa vya Kukusanya Data.....	29
3.5.1	Kalamu na Daftari.....	29
3.5.3	Komputa na Vifaa Vyake	30
3.6	Sampuli.....	31
3.7	Eneo la Utafiti	32
3.8	Mipaka ya Utafiti	33
3.9	Uchambuzi wa Data	33
3.10	Hitimisho	33
	SURA YA NNE	35
	UWASILISHAJI WA DATA, UCHAMBUZI NA MJADALA	35
4.1	Utangulizi	35
4.2.1	Ukuti Ukuti	36
4.2.2	Kula Mbakishie Baba	37
4.2.3	Kiguru Cheche	37
4.2.4	Baba Uyo	38
4.2.5	Yai Bovu.....	39
4.2.6	Mabata	39
4.2.7	Nani Kaona Upopo	40
4.2.8	Ainaku Tabal Amsi	41
4.2.9	VituVyenyehai	42
4.2.10	Tumbili Walani?	42
4.2.11	Anjikicha	43
4.2.12	Chagua Mwenzako	44
4.2.13	Kichupa.....	45

4.2.14	Sisimizi	45
4.2.15	Kitango Malemale	46
4.2.16	Majani ya Mdimu	47
4.2.17	Mnara wa Njiwa.....	48
4.2.18	Chakula Bora	48
4.2.19	Elimu	49
4.2.20	Jina Lako Nani?	50
4.2.21	Safari Yetu	51
4.2.22	Jungu la Uji.....	51
4.2.23	Kanambia Baba Nichupe	52
4.2.23	Samaki	53
4.2.24	Wakati.....	53
4.3	Usanii Unaojitokeza Katika Nyimbo za Michezo ya Watoto.....	54
4.3.1	Matumizi ya Methali na Misemo	54
4.3.1.1	Matumizi ya Methali	54
4.3.1.2	Matumizi ya Misemo.....	56
4.3.2	Matumizi ya Tamathali za Semi	57
4.3.3	Matumizi ya Tauria/ Tafsida.....	58
4.3.4	Matumizi ya Balagha.....	60
4.3.6	Matumizi ya Kejeli.....	63
4.3.7	Matumizi ya Sitiari.....	65
4.3.8	Matumizi ya Tashbiha	67
4.3.8	Matumizi ya Tashhisি	68
4.3.9	Matumizi ya Takriri	69

4.3.10	Mtindo wa Kutaja Majina ya Vyakula	70
4.3.11	Mtindo wa Daiolojia.....	72
4.3.12	Mtindo wa Kutumia Viumbe Wadudu	74
4.3.13	Mtindo wa Utahoaji Maana	74
4.3.14	Mtindo wa Kutaja Majina ya Miji na Mitaa	75
4.4	Dhamira Zilizojitokeza Katika Nyimbo za Michezo Ya Watoto.....	76
4.4.1	Dhamira ya Uvumilivu katika Ndoa	77
4.4.2	Dhamira ya Ruhusa kwa Wanandoa	78
4.4.3	Dhamira ya Tabia ya Wanawake Kutochagua Waume.....	79
4.4.4	Dhamira ya Tabia Njema.....	80
4.4.5	Dhamira ya Kuepuka Kiburi.....	81
4.4.6	Dhamira ya Mazoezi ya Viungo kwa Watoto.....	82
4.4.7	Dhamira ya Uweza wa Allah	83
4.4.8	Dhamira ya Kufanya Kazi kwa Bidii	86
4.4.9	Dhamira ya Kuepuka Utégemezi katika Maisha	86
4.4.10	Dhamira ya Kutowajibika katika Familia.....	87
4.4.11	Dhamira ya Madhara ya Tabia Mbaya	88
4.4.12	Dhamira ya Uvivu	89
4.4.13	Dhamira ya Malipo ya Uovu	90
4.4.14	Dhamira ya Usafi	92
4.4.15	Dhamira ya Umuhimu wa Chakula Bora	93
4.4.16	Dhamira ya Madhara ya Mama wa Kambo	95
4.4.17	Dhamira ya Umuhimu wa Elimu	95
4.4.18	Dhamira ya Utoaji Mimba.....	96

4.4.19 Dhamira ya Umuhimu wa Wakati.....	97
4.4.20 Dhamira ya Kuwa na Malengo katika Maisha.....	97
4.4.21 Dhamira ya Utetegemezi kwa Allah (s.w)	98
4.4.22 Dhamira ya Onyo kwa Wanajamii.....	99
4.5 Muhtasari	100
SURA YA TANO	101
MUHTASARI NA MAPENDEKEZO	101
5.1 Utangulizi	101
5.2 Muhtasari	101
5.3 Mchango wa Utafiti.....	103
5.4 Mapendekezo	103
5.5 Hitimisho	104
MAREJELEO	105
VIAMBATANISHO	109

ORODHA VIAMBATANISHO

Kiambatanishi 1: Nyimbo za Michezo ya Watoto.....	109
Kiambatanishi 2: Michezo Yenyewe Inavyochezwa.....	122
Kiambatanishi 3: Orodha Ya Wahojiwa	132

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kuitambulisha mada ya utafiti na sababu za kufanyika kwa utafiti huu. Utafiti huu unachunguza mchango wa nyimbo za michezo ya watoto katika kukuza maadili ya jamii ya Wapemba. Mambo mengine ya msingi yanayoangaziwa katika sura hii ni usuli wa mada ya utafit, asili ya nyimbo za michezo ya watoto, tatizo ta utafit, malengo ya utafiti, masuali ya utafiti, umuhumu wa utafiti na kumalizia hitimisho la sura ya kwanza.

1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti

Mashairi na nyimbo hupatikana katika kila jamii duniani. Huhusisha uwasilishaji kwa njia ya kuimba, kukariri au kughani. Mashairi na nyimbo hutungwa na watu katika jamii. Hivyo baadhi ya watanzi wanajuilikana, na kwa nyimbo nyengine, majina ya watanzi wake hawajuilikani au wameshasahaulika na nyimbo zimekuwa mali ya jamii, baadhi ya nyimbo hizo na mashairi hutungwa na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo kutegemea na tukio.

Uteuzi na mpangilio wa maneno maalum katika mashairi na nyimbo huibua hisia zinazohusiana na tukio. Hisia hizi ni kama vile furaha, huzuni, uchungu, utulivu wa moyo, chuki na kadhalika. Kwa kawaida ushairi una nguvu na mvuto wa ajabu (M'ngaruthi 2008:01) na nyimbo za michezo ya watoto ni mionganini mwa mashairi ya nyimbo.

Nyimbo hizi ni za tangu enzi ya zamani kwani mara nyingi watoto baada ya kwisha kula chakula cha usiku ndani ya mbaramwezi hukusanyika majumbani na kujikuta wakicheza michezo mbali mbali ambayo ndani yake ina nyimbo zenye maana. Nyimbo hizi huwa na sauti nzuri na ya kuvutia ambao watoto walikuwa wakiimba kwa kujiburudisha na kuwapumzisha wazazi wao kwa muda huo, kuamsha hamasa nakadhalika (Matteru, 1982).

Kawaida nyimbo hizi huwa zinainmbwa na watoto wenyewe, lakini ukweli ni kwamba hata mama na dada nao wanaweza kujumuika na watoto hawa katika kuonyesha lengo la mashirikiano. Kwasababu nyimbo hizi huimbwa na watoto wenyewe wakati wa usiku baada ya chakula huku wazazi wamejipumzisha kutokana na heka heka na harakati za kujitafutia maisha.

Moja ya lengo la kuimba nyimbo hizi katika michezo ya watoto, ni kuwaburudisha katika michezo hiyo (Materu 1982). Wazazi nao wakati huu hulazimika kujipumzikia ama kulala kabisa ama kufanya majukumu mengine yanayomsubiri (Haji na wenzake, 1992).

Aidha lugha iliomo katika nyimbo za michezo ya watoto ni ya kishairi, kwa sababu baadhi ya nyimbo munapatikana vina vya kati na vina vya mwisho. Aidha ushairi si lazima kujitambulisha kwa vina na mizani, mara nyengine mpangilio mzuri wa maneno na ukamilifu wa dhana unatosha Msokile, M (1992).

Jambo la kusositiza hapa ni kwamba, ni kweli nyimbo hizi huimbwa na watoto wenyewe katika michezo yao mbali mbali, lakini utafiti unaonesha kuwa, maudhui

yaliyomo ndani ya nyimbo hizi ni mazito na hayamgusi mtoto peke yake, bali jamii nzima kwa ujumla, wakiwemo akina mama na akina baba.

1.3 Asili ya Nyimbo za Michezo ya Watoto

Asili hasa ya nyimbo hizi haijulikani ila inasemekana ni pale mtoto baada ya kumaliza pirika zake ambapo hujikuta akicheza michezo mbali mbali kama njia ya kurutubisha akili yake (Materu 1982). Katika jamii ya waswahili, kwa mfano Wazanzibari hakuna tofauti na dhana hiyo, kwani dhana kama hii ipo mionganoni mwa wanajamii wanaamini kuwa mtoto nae ili akue kiakili na kimwili njia nyengine ni kumpa nafasi ya kucheza michezo yao mbali mbali. Kwa kutilia mkazo, Mn'garuthi (2008) anafafanua kuwa mtoto alilelewa kwa uangalifu mkubwa, hivyo kumuacha mtoto akacheza maeneo ya nyumbani si jambo baya ni mionganoni mwa malezi.

Aidha, inasemekana kuwa kwa kawaida katika sehemu nyingi za nchi yetu watu hula chajio baada ya watu kusali sala ya Isha. Kwa watoto wadogo ambao kutwa huwemo katika pirika mbalimbali, ikikaribia wakati huu, watoto huwa taabani kwa machofu. Wakishakoga, ili wabaki macho na waweze kula chakula hicho hufanyika kitu cha kuwafanya wawe macho na hujikuta wakicheza michezo mbali mbali ambayo ndani yake huwemo nyimbo, Ameir, I (1983).

Aidha, Mazigwa (1991) anasema kuwa michezo ya watoto huchezwa na watoto wa kike na wa kiume, wa nyumba moja au nyumba zilizo jirani. Katika kufanya hivyo, lazima washiriki waanzie wawili na kuendelea ili wakati wa kuimba nyimbo, sauti inoge.

Ufafanuzi wa maelezo hayo, ulitosha kumuingiza hamu mtafiti, kuona kuwa ipo haja kubwa ya kufanya utafiti katika utanze wa nyimbo za michezo ya watoto. Na sababu hasa zilizomsukuma mtafiti, kuzitafiti nyimbo hizi ni kama zifuatazo:

Kwanza, mtafiti alitaka kuhakikisha uwepo wa nyimbo za michezo ya watoto ndani ya maeneo tofauti tofauti ya kisiwa cha Pemba.

Pili, kuanza kwake kupotea kwa kusahaulika, kwa sababu haziimbwi tena kama zamani, kama asemavyo Ali (1969: 20).

“Nyimbo hizi ni za zamani, zikitumika sana hapa petu Unguja na Pwani ya Afrika ya Mashariki. Siku hizi hazisikikani tena majumbani, zimeanza kupotea na Kusahaulika kidogo kidogo na mpaka mwisho baada ya muda si mrefu zitapotea kabisa”

Tatu, mtafiti alitaka kujua, ni kwa kiasi gani nyimbo za michezo ya watoto zinaweza kuleta mchango wa kimaadili katika jamii ya wapemba.kwani baadhi ya wanajamii wanahisi ni kazi nyengine za fasihi tu kama vile Riwaya au semi ndio zenyenye wajibu wa kufunza jamii.

Ambapo huziona nyimbo zilizo ndani ya michezo ya watoto kuwa hazina maana, kumbe ukichunguza kwa undani utakuta kuwa nyimbo hizi si tu kuwa zinaburudijasha au kupoteza muda kwa watoto hao bali pia zinatoa mchango mzuri katika kumfunza mtoto na kumkuza kiakili na kimaadili. Kutokana na maudhui mengi kumgusa mwanamke na hali yake katika jamii au mtoto na uhusiano wake na mama, (Mulokozi 1996).

Hivyo iaminike kuwa nyimbo hizi aghlabu huwa hazimburudishi mtoto, bali pia zinatoa mafunzo mbali mbali mionganii mwa wanajamii. Mfano wimbo ufuatao wa “**Kachiri**” unafafanua haya.

Kachiri kachiri.....saga

Mume wangu kasafiri.....saga

Kaniachia ukili.....saga

Upatao pima mbili.....saga

Na kipande cha hariri.....saga

Kachiri saga,kachiri saga.

Katika wimbo huu, unamfunza mwanamke awe na moyo wa uvumilivu .Kipindi ambacho mume wake hayupo, na badala yake aweze kujishughulisha na kazi nyengine za stadi za maisha ili kuficha aibu yao, mfano kupakasa, biashara, kulima, kubeba zege nakadhalika.Vile vile nyimbo hizi hutoa mafunzo kwa mtoto pia. Mfano kuna wimbo unaosema:

“Watoto Wangu”

“ *Watoto wangu ee,* *ee*

Mimi mama enu, *ee*

Sina nguvu tena, *ee*

Zakuuwa simba, *ee*

Simba ni mkali, *ee*

Anauwa baba, *ee*

Anauwa mama, *ee*

Anauwa dada, *ee*

Anauwa kaka, *ee*

Watoto wangu *ee*

Haidhuru piteni.....”

Hapa wimbo huu unawashajihisha watoto waachane na mambo yasiyo na maana na badala yake wajishughulishe na masomo ili waweze kupigana na njaa kwani njaa inauwa. Kutokana na dondoo hizo, ni wazi kusema kuwa: Nyimbo za michezo ya watoto hazikuwa na lengo la kuburudisha watoto tu bali zilitoa mafunzo mbali mbali mionganoni mwa wanajamii.

Katika kueleza mambo haya, mbinu mbalimbali zimetumika ili kufichua ukweli huo. Kupitia tasnifu hii mambo hayo yalishughulikiwa na imejaribu kuona kama ni kweli kuwa kuna mchango mkubwa unaopatikana kupitia nyimbo za michezo ya watoto kama wataalamu wengi walivyojadili.

Wataalamu hao ni pamoja na Finnegan (1970), Haji na wenzake (1992), Othman (2007), Fasihi Simulizi Zanzibar (2003) na Mulokozi (1996). Ingawa hawakuonesha kwa kina mchango huo. Tasnifu hii inakusudia kulitazama hili na kuweka dhahiri mchango wa Nyimbo za michezo watoto hususan katika kujenga maadili ya jamii ya wapemba.

Vile vile, katika kueleza mambo haya, wataalamu hawa hawakuweka ni njia na mbinu zipi zitakazotumika mpaka jamii ifaidike na mchango wa nyimbo hizi. Tasnifu hii itazijadili mbinu hizi kwa undani, na pia tasnifu hii inatambua madai ya baadhi ya wahakiki wa kazi za fasihi kuwa mshairi huitungia nafsi yake. Kauli hii ni

vizuri kuihusisha na mada ya utafiti huu, kwani ingawa watoto ndio wanaoimba na kucheza lakini ujumbe huwa ni wa wanajamii husika wakiwemo akina mama, baba na watoto wenyewe.

1.4 Tatizo la Utafiti

Haja ya kuchunguza mchango wa nyimbo za michezo ya watoto inatokana na sababu kwamba, nyimbo za michezo ya watoto hazijafanyiwa utafiti wa kutosha, tafiti nyingi ambazo zimewahi kufanywa zimegusia tu utanzu huu labda kwa kuonyesha jinsi athari za Sayansi na Teknolojia zinavyoathiri nyimbo hizi, au pengine ni usanii upi unaojitokeza katika utanzu huu nakadhalika. Mathalani Maalim Mbaruk wa Chuo Kikuu cha Dodoma (2015) alionyesha athari za Sayansi na Teknolojia katika nyimbo za harusi na Bi Fatma Juma Ali wa UDSM (2014) alionyesha usanii uliomo kwenye nyimbo za msondo nakadhalika. Hivyo utakuta bado tafiti zinazozungumzia nyimbo za michezo ya watoto ni chache sasa.

Mambo hayo ndiyo yaliyomsukuma mtarufi kubainisha na kuchambua kwa kina mchango hasa unaopatikana kuitia nyimbo za michezo ya watoto na kuonyesha umuhimu wa kuendelezwa kwa nyimbo hizi ndani ya jamii ya Pemba Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini.

1.5 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahsusini matatu kama ifuatavyo:

1.5.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchambua na kubainisha mchango wa nyimbo za michezo ya watoto katika kukuza maadili ya jamii ya Wapemba.

1.5.2 Malengo Mahasusi

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahasusi yafuatayo:

- (i) Kuainisha nyimbo za michezo ya watoto katika maeneo tofauti tofauti ya kisiwa cha Pemba.
- (ii) Kubainisha mchango unaopatikana kuitia nyimbo za michezo ya watoto ndani ya kisiwa cha Pemba.
- (iii) Kuonesha jinsi mbinu mbali mbali za kisanii (fani) zilivyotumika kuibua maudhui katika nyimbo za michezo ya watoto.

1.6 Maswali ya Utafiti

Ili kufanikisha lengo kuu na madhumuni mahasusi, utafiti huu ulikuwa na maswali matatu yafuatayo:

- (i) Je, ni nyimbo zipi za michezo ya watoto zinazopatikana katika maeneo tofauti tofauti ya kisiwa cha Pemba?
- (ii) Je, ni mchango gani unaopatikana kuitia nyimbo za michezo ya watoto kama ni sehemu ya ujumbe?
- (iii) Je ni mbinu zipi za kisanii ambazo zimetumika ndani ya nyimbo za michezo ya watoto ambazo zimesaidia kuibua ujumbe husika?

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya kazi hii yana makusudio yafuatayo:

- (i) Utafiti huu bila shaka utatoa mchango mkubwa katika uwanja wa fasihi hasa kwenye utanze wa nyimbo.
- (ii) Utafiti huu unaonekana kuwa ni nyezo ya kuwashajihisha watoto kushiriki kwenye michezo yao ya asili ya kila siku.

- (iii) Utafiti huu unatoa mwanga kwa walimu wa Maandalizi na Msingi kuona umuhimu wa kutumia nyimbo hizi katika kufundishia mema ya jamii zao.
- (iv) Utafiti huu pia unaonekana kuwa ni chombo cha kuwaamsha waandaaji mitalaa kuona haja ya kuingiza michezo ya watoto katika elimu ya maandalizi, msingi hata sekondari.

1.8 Mpangilio wa Kazi ya Utafiti

Utafiti huu umegawanyika katika sura tano kama ifuatavyo:

- (i) **Sura ya kwanza** inahusu utangulizi wa jumla wa utafiti na usuli wa tatizo la utafiti kuhusiana na suala la mchango wa nyimbo za michezo ya watoto katika kukuza maadili ya jamii, mfano katika jamii ya wapemba wilaya Wete. Pia inaonesha tatizo la utafiti, malengo, maswali, na umuhimu wa utafiti pamoja na muhtasari wa sura ya kwanza.
- (ii) **Sura ya pili** inaonesha mapitio ya machapisho mbalimbali na nadharia iliyotumika.
- (iii) **Sura ya tatu** inaelezea mbinu mbalimbali zilizotumika kukusanya na kuchambuwa data.
- (iv) **Sura ya nne** ni uwasilishaji na uchambuzi wa data.
- (v) **Sura ya tano** inahusu muhtasari wa kazi ya utafiti, utoshelevu wa nadharia, mapendekezo ya utafiti na tafiti zijazo na kumalizia na hitimisho.

1.9 Hitimisho

Katika sura hii ya kwanza vipengele vilivyofafanuliwa ni Usuli wa mada, Tamko la tatizo la utafiti, Malengo ya utafiti, Maswali ya utafiti na Umuhimu wa utafiti. Kwa ujumla inaonekana kuwa nyimbo za michezo ya watoto zimeandikwa na wataalamu

mbali mbali na kujulikana na watu tofauti tofauti na katika kuzijua kwao, wameonesha umuhimu wa kuendelezwa nyimbo hizi katika jamii zetu. Ambapo utafiti huu umedhamiria kwa kina kuonesha ni mchango gani hasa unaopatikana kupitia nyimbo za michezo ya watoto katika jamii ya Wapemba, utafiti huu umelenga kuonesha mchango huo katika tasnifu hii.

SURA YA PILI

MAPITO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia kazi mbalimbali zilizoandikwa na ambazo zinahusiana na mada na dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu. Mambo yanayojadiliwa ni dhana ya nyimbo, maana na aina za nyimbo. Umuhimu wa nyimbo kwa jamii, dhana ya nyimbo za michezo ya watoto. Kwa kumalizia sehemu hii inahitimishwa kwa kiunzi cha nadharia kinachotumika katika tasnifu hii.

2.2 Maandiko Kuhusu Asili na Maana ya Nyimbo

2.2.1 Asili ya Nyimbo

Msokile (1992: 46) anaona kuwa nyimbo zinazobuniwa kimsingi hazitofautiani na ushairi katika fasihi, ndio maana ameweka na ushairi pamoja. Haji na wenzake (1992: 36) wanaona kuwa nyimbo ni utanzu wa ushairi, na kwamba tanzu zake nyengine ni tenzi. Hamad (2008:40) naye anaunga mkono kauli hii kuwa nyimbo zinatokana na ushairi simulizi asemapo:

“Nyimbo ni utanzu mkongwe wa fasihi simulizi ambao ulianza kuimbwa kwa mahadhi ya sauti tu. Ikaongezeka kwa kupigwa kofi kukoleza mahadhi nayo na hata kwa kutumia ala mbali mbali zinazokoleza muziki wa nyimbo hizo.”

2.2.2 Maana ya Nyimbo

Mazigwa (1991) amefasili wimbo kuwa ni kifungu cha maneno yaliopangwa katika utaratibu maalum wenye kutekeleza mapigo ya muziki.

Aghlabu lugha yake huwa ni ya mkato ambayo hifuata mapigo ya ala za muziki kwa mfano ngoma zeze, marimba, njuga, filimbi nakadhalika. Nyimbo pia huenda sambamba na ngoma kwani wakati wa kuimba ngoma huendelea kulia na wakati huo huo waimbaji hucheza. Pia wengine huimba kwanza, halafu ngoma kufuatia na wachezaji hifuata mlion wa ngoma.

Mkwera na wenzake, amefasili nyimbo kuwa ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Katika kufafanua maana ya muziki anasema ni mpangilio wa sauti za ala na uimbaji unaoleta athari fulani kwa binaadamu kupitia hisia zake na pia akili yake. Mkwera amehitimisha kwa kusema: muhimu ni uimbaji, sauti za ala na miondoko sio lazima.

Haji na wenzake (2004:4) wamefasili nyimbo kuwa ni mashairi mafupi ambayo hujitokeza katika sehemu nyingi za jamii. Wameendelea kwa kusema nyimbo huwa ni fupi aghlabu huwa ni ubeti mmoja tu wenyenye mistari mitatu. Nyimbo huweza kuambatana na Sanaa ya kughani, ngoma, makofi au muziki.

Wamitila (2003:4) amesema kuwa tungo za utawa huu zina mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi ambayo hupangwa kwa utaratibu au muwala wenyenye mapigo ya kimziki au mizani. Ingawa kanuni ya ala si yalazima katika kuanisha nyimbo, inawezekana wimbo ukaambatana na ala, kwa mfano chapuo, vugo, ngoma, marimba, pembe na zumari.

King'ei na Kisovi (2005) pia wamefasili nyimbo kuwa ni utungo wenyenye mpangilio maalum wa maneno au una mahadhi. Wamesema nyimbo huambatana na shughuli

au jambo fulani na sauti ya muimbaji au waimbaji huwatia moyo watu kama vile wavuvi au wakulima katika kazi zao. Vile vile nyimbo huimbwa kwa burudani katika sherehe fulani kama vile harusi, ibada ya kidini, kafara, matambiko, (na katika tohara) za jando na unyago.

Mulokozi (1996) amefasili wimbo kuwa ni kila kinachoimbwa, hivyo ni dhanna inayojumuisha tanzu nyingi kama vile hadithi huweza kuingia katika utanzu huu pindi zinapoimbwa. Anaendelea kwa kusema kuwa vitu muhimu vyatutambulisha nyimbo ni kama vile, muziki, sauti ya muimbaji, muziki wa ala, matini au maneno yanayoimbwa, hadhira inayoiwanya na muktadha unaofungamana na wimbo huo.

Kutokana na fasili hizo za wataalamu mbali mbali imedhihirika kuwa nyimbo zina sifa zake maalum za kuzitambulisha. Baadhi ya sifa hizo ni maneno yanayoimbwa na yenye mpangilio maalum, hufungamana na muktadha, sauti ya muimbaji au waimbaji. Sio lazima kutumia ala na vyombo vyatutambulisha. Nyimbo katika jamii zina dhima mbali mbali: kama burudani, nyimbo ni njia nzuri ya kutumbuiza na kumpa msikilizaji au muimbaji mwenyewe burudani.

Vile vile nyimbo nyingi hutumiwa kuwahamasisha watu kutenda jambo fulani, hii ni kwasababu huchochea hisia za kuchangamkia shughuli inayofanyika; kwa mfano vita, kutwanga au kulima.

Hata hivyo, nyimbo hutumika kurithisha utamaduni wa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Nyimbo zaweza kutumika kuhifadhi historia ya jamii, kwa mfano matokeo kama ya vita.

Mwisho nyimbo ni njia nzuri ya kuelimisha na kupitisha maarifa mbalimbali mionganii mwa wanajamii. Kwa mfano katika nyimbo za harusi, bibi harusi hufunzwa mambo ya kwenda kufanya kwa mumewe na maisha ya ndoa kwa ujumla.

2.2.3 Maandiko kuhusu Uanishaji wa Nyimbo

Okupweho (1992:1227) ameeleza kuwa katika jamii watu hutumia vigezo tofauti tofauti vya kuainisha nyimbo na maghani. Vigezo hivyo ni kama vile maudhui, dhamira, ala zitumikavyo, mtindo wa uimbaji, muktadha na muimbaji wa nyimbo hiyo. Amependekeza kutumika kigezo cha maudhui katika kugawa ushairi wa kiafrika kwa kuangalia dhamira kuu za ushairi huo.

Finnegan (1970), Mulokozi (1989 na 1996), Mazigwa (1991), Mkerwa. (ht) na wenzake (1992), Msokile (1992), Wamitila (2005) na Kingei na Kisovi (2005) kupitia uainishaji wao huu wa nyimbo, tumepeata nyimbo mbali mbali kama vile nyimbo za dini, nyimbo za harusi, nyimbo za sifo, nyimbo za watoto, nyimbo za taarabu kati ya hawa waliotaja nyimbo za michezo ya watoto ni Mulokozi (2006) na Fasihi simulizi Zanzibar.

Uanishaji wa nyimbo umekuwa na utata kwa sababu hakuna kigezo maalumu kinachotumika katika uainishaji wake. Hii inatokana na maelezo ya Wamitila (2002) yasemayo takriban shughuli zote za binaadamu huandamana na nyimbo hali ambayo imepelekea kutokea kwa aina nyingi za nyimbo na kutofautiana kwa aina hizo kati ya wataalamu mbalimbali. Vilevile tatizo la kuwa na nyimbo za aina fulani zilizoainishwa na mtaalamu mmoja na mtaalamu mwengine huainisha aina nyengine za nyimbo. Kwa mfano nyimbo za kuamsha daku zilizoainishwa na Haji na wenzake

zinapatikana katika jamii ya Wazanzibari au waislamu kwa ujumla na haiwezi kupatikana katika jamii isiyokuwa ya waislamu. Aidha kila shughuli huwa na aina yake maalumu ya nyimbo.

2.2.4 Kazi na Maandiko kuhusu Nyimbo

Utanza wa nyimbo umebahatiwa kutafitiwa katika vipengele vyake muhimu nya fani na maudhui, kama vile dhamira, matumizi ya lugha, tafsida, ishara na picha. Mathalani nyimbo za kilimo za kabilia la Wafipa zimeangaliwa fani, maudhui, na dhima yake. Nyimbo za harusi za kabilia la Wapagua zimefanyiwa utafiti katika matumizi ya lugha, dhima na dhamira zilizomo. Nyimbo za waimbaji walemavu zimetafitiwa dhamira zake mfano nyimbo zinazohusu Ukimwi zimefanyiwa utafiti kwa kuangaliwa lugha yake kisanii na namna inavyoibua maudhui yanayohusu ugonjwa huo. Utafiti pia umefanywa katika nyimbo za jando na unyago za jamii ya Wamwera na kuangalia zinafungamanaje na jamii hiyo ya Wamwera.

Kutokana na maelezo ya tafiti mbalimbali zilizofanyika katika utanza wa nyimbo na kugusia nyimbo za harusi, jando na unyago na nyimbo za taarab. Mtafiti alipata hamu ya kufanya utafiti wa nyimbo za michezo ya watoto kama ni aina moja ya nyimbo zilizokuwa hazijatafitiwa.

2.2.5 Maandiko kuhusu Nyimbo za Michezo ya Watoto

Ameir na wenzake (1983) amezungumzia suala la aina ya nyimbo za michezo ya watoto, kuwa lugha yake inayotumika huwa ni nzito, yenye mafumbo na picha, hivyo huwa nzito kuhakiki ujumbe uliomo kwenye nyimbo hizo ama michezo hiyo na wazee. Anaendelea kwa kusema, kawaida katika sehemu nyingi za nchi yetu,

watu hula chajio, baada ya watu kusali sala ya Isha. Kwa watoto wadogo ambao kutwa huwemo katika pirika mbalimbali, ikikaribia wakati huu, huwa taabani kutokana na machofu. Wakishakoga ili wabaki macho na waweze kula chakula hicho, hufanyika kitu cha kuwafanya wawe macho hujikuta wakicheza michezo mbalimbali ambayo ndani yake huwemo nyimbo zenyenye maana.

Aidha ameongeza kwa kusema kuwa nyimbo nyingi za michezo ya watoto huwa hazina mantiki, yaani mpangilio wa vina na mizani, na hivyo huonekana hazina maana. Ukoefu huu wa mantiki kwenye nyimbo za michezo ya watoto, ndiyo husababisha jamii kutozitilia maanani sana na kuona hazina mchango mkubwa katika makuzi ya watoto wenyewe kimaadili. Fasihi Simulizi Zanzibar (1983) ameeleza kuwa katika kisiwa cha Pemba imo michezo mingi tu ya watoto, tatizo ni kwamba wanajamii huchukulia nyimbo zilizomo michezoni kuwa hazina maana, huimbwa ziendane na mshindo na mpangilio mzima wa michezo na hivyo, huonekana kuwa dhima yake kubwa ni kuburudisha tu.

Anafafanua kwa kusema kuwa, ukoefu huu wa mantiki ndani ya nyimbo hizi, ndio wanajamii hawazitilii maanani sana na kuona hazina mchango mkubwa katika makuzi ya watoto wenyewe kimaadili. Lakini ukweli ni kwamba, nyimbo za michezo ya watoto ukizichunguza kwa undani zina taathira kubwa kwa wanajamii.

Aidha, Ali (1969:20) anafafanua kwa kusema kuwa, nyimbo za michezo ya watoto ni nyimbo za kuburudisha watoto katika michezo yao ambapo huonekana kutoka kila khabila. Anaongeza kwa kusema, maudhui mengi ya nyimbo hizi, aghlabu humhusu mwanamke na hali yake katika jamii au mtoto na uhusiano wake na mama.

Kwa upande mwengine, nyimbo nyingi za michezo ya watoto, huwashinda wahakiki wa maudhui kutohana na lugha yake. Lugha yenyewe huwa nzito, yenyewe picha, na mafumbo, na hata wahakiki wengi wamekuwa na wasiwasi kwamba huenda watoto wakawa wametungwa nyimbo hizi na wakubwa. Aidha mtaalamu huyu, anafafanua kwa kusema kuwa, nyimbo za michezo ya watoto zitakuwa hazikutendewa haki iwapo hazitoangaliwa vipengele vyote vya kisanaa.

Kwa upande mwengine, inasemekana kuwa lugha iliomu katika nyimbo za michezo ya watoto ni ya kishairi, kwa sababu munapatikana vina na mizani katika nyimbo hizo vya kati na vya mwisho. Kingei na kisovi (2005). Aidha anasema ushairi si lazima kujitambulisha kwa vina na mizani, mara nyengine mpangilio mzuri wa maneno unatosheleza ukamilifu wa dhana.

2.2.6 Fasili ya Fani na Maudhui

Mulokoza Kahigi (1979: 54) wamefasili kuwa fani kama Sanaa na ni jumla ya vipengele vya lugha vilivyowekwa katika mpangilio mahususi ili kutoa maana fulani. Vipengele vya lugha kwa sababu lugha hiyo ndio nyezo kuu ya kuimba kazi ya Sanaa. Ujumbe ni yale mawazo yanayozungumziwa (dhamira mama).

Msokile (1992:53-54) kwa upande wake anafasili fani kuwa ni jumla ya mambo mengi yanayojenga kazi ya fasihi. Na maudhui ni jumla ya mawazo katika kazi ya fasihi. Wamitila (2003:41) anafasili fani kuwa ni dhana itumiwayo kueleza muundo na mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi hata sehemu zake. Fani hueleza mbinu na mtindo wa kuyawasilisha maudhui. Maudhui ni neno linalotumiwa kujumuisha yaliyomo katika kazi ya fasihi. Pia Madumulla (2009:124) amesema kuwa fani ni ule

ufundi anaotumia msanii katika kazi yake. Katika kueleza dhana ya maudhui anasema kuwa ni yale mawazo, fikra na ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi.

Senkoro (2011:7) anafasili fani kuwa ni ujumla ya ufundu wakisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake. Na maudhui ni yale yapatikanayo kutokana na mawazo, mafunzo na ujumbe uliomo katika kiini cha fani. Hivyo fasili hizi zimemsaidia mtafiti kuweza kuchambua kazi yake kwa umakini kabisa kwa kuangalia uwiano uliopo katika vipengele vya fani na maudhui ndani ya nyimbo za michezo ya watoto.

2.3 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani (TUKI 2004: 300). Maana ya nadharia kwa mujibu wa BAKITA (2010:298), ni mawazo yanayotumika kuwa ni mwongozo wa kutekeleza jambo na kutambulikana kwa dhana. Tasnifu hii imeongozwa na nadharia tatu, nazo ni: Nadharia ya Uchambuzi Matini, Nadharia ya Muingiliano Matini na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

2.2.1 Nadharia ya Uchambuzi Matini

Huu ni mkabala wa kizamani ambao unajikita katika kuchunguza ubunifu wa msanii katika vipengele vya fani na maudhui kwa ujumla katika kazi za Sanaa. Lengo la kazi ya Sanaa huangaliwa kwa kuzingatia uhusiano uliopo wa kazi za fasihi katika vipengele tofauti vya kifani. Uhakiki huu unazingatia upeo wa msomaji atakavyoifasiri matini kwa kurejelea muktadha na historia ya jamii iliyokusudiwa ili kupata athari ya kazi hiyo kama vile mwamko, kuburudishwa nakadhalika. Mkabala huu ulilenga kuchunguza falsafa, ubunifu wa mwandishi, historia na mambo ya

kiutamaduni. Hii ilikuwa ni chanzo cha kuzaliwa kwa nadharia mbalimbali za fasihi. Maendeleo ya kijamii, kiutamaduni na kiugeni ya karne ya 20 yameitanua nadharia hii ya uchambuzi matini katika nchi nyingi kama vile Ulaya, Amerika ya kati na Afrika ya Kusini na hata ulimwengu mzima.

Kwa mujibu wa Jabish (2012) uchambuzi wa matini ni njia ya Sayansi ya jamii ambayo matini inahakikiwa kwa kuangaliwa maana, utunzi na uhalisi. Lassweu (1948) ametoa maswali ya kujiuliza wakati wa uchanganuzi wa matini nayo ni: Nani amesema nini, kalengwa nani, kwa nini, kwa kiwango gani, kazi inaathiri hadhira iliojengwa?

Misingi mikuu ya nadharia hii imejengwa katika wazo kuwa fasihi hutumia lugha ambayo ndio nyezo yake kuu, na hutumia vionjo tofauti ambavyo huitofautisha kazi ya fasihi na kazi nyengine zisizo za kifasihi, hivyo ni kazi ya mhakiki kuchambua vipengele hivyo. Maana ya kazi ya fasihi yaani maudhui, falsafa, ujumbe na mafunzo hupatikana baada ya mhakiki kuvichambua vipengele vyake na sio kuchukulia maana ya juu au ya kikamusi kama inavyojitokeza katika matini inayohakikiwa.

Vilevile katika nadharia hii, uchambuzi wa kazi ya fasihi huweza kutofautiana kulingana na elimu, ujuzi na uwelewa wa mhakiki wa kazi hiyo. Kazi ya Sanaa ni lazima iathiriwe na mambo yaliomo katika jamii kama vile siasa. Pia mtunzi huathiriwa na hali hiyo kwani ndimo anamoishi na hawezikuepuka na ndio sababu hujitokeza katika kazi zake kwani muktadha hubeba maudhui ya kazi ilioandikwa. Fani ni lazima ioane na maudhui yanayosawiriwa katika kazi ya Sanaa. Kazi ya fasihi ikizidi kipengele kimoja na kingine huwa dhaifu na kazi hiyo huonesha

udhaifu huo. Hii ina maana kuwa kazi ya Sanaa inapoegemea kuwa na fani dhaifu au maudhui yakiwa dhaifu kazi hiyo yote huonesha udhaifu huo. Pia fani inapokuwa nzuri na maudhui yakiwa dhaifu, udhaifu huo pia hujitokeza katika kazi na pia kinyume chake.

Kazi ya fasihi huwa na hadhira maalumu ambayo hulengwa kupata na kuathiriwa na ujumbe wa msanii kuitia kazi ya fasihi, kinyume chake lengo la msanii hushindwa kufikiwa. Nadharia hii ya uchambuzi wa matini imetumika kuhakiki kipengele cha fani na kuibua maudhui yanayopatikana katika nyimbo za michezo ya watoto kwa kuangalia nani anaongea nini na athari yake kwa hadhira yake iliyokusudiwa.

2.3.2 Nadharia ya Mwingiliano Matini

Mwingiliano matini ni dhana inayorejelea matini ndani ya matini, huongelea uhusiano wowote unaoweza kuonekana katika matini moja au zaidi. Ili kupata maana ya matini ni lazima msomaji arejelee matini nyingine zilizotangulia, hii inatokea pale mtunzi anapoiga au kuunda matini iliyopita au kuirejelea matini moja au nyingine. Nadharia ya mwingiliano matini ilizuka kwa ajili ya kuzikosoa nadharia za Umuundo na Semiotiki zilizolenga kuonesha kuwa mwandishi pekee ndie ajuaye maana ya kazi za fasihi. Katika nadharia hizi ilionekana kuwa maana ya matini hupatikana ndani ya matini yenye tu kwa kuangalia miundo yake na namna lugha ilivytumika.

Ubunifu wa Kristeva (1980) wa mwingiliano matini unapingana na nadharia ya Semiotiki ya Ferdinand de Saussure ambayo inazungumzia vipi ishara huwakilisha maana ya ndani ya muundo wa matini. Nadharia hii imetoka kwenye nadharia ya Udiolojia ya Mikhail Bakhtin ambayo kwayo maana huwa siyo ya upekee katika

matini moja kwa mfano riwaya. Bakhtin anaamini kuwa kila tamko huwa na athari ya matamko mengine yanayolitangulia au yatakayofuatia kama majibu au itiko.

Dhana kuu katika nadharia hii ni usemezano katika maongezi ya kila siku. Dhana hii huyarejelea mazungumzo ya binaadamu na hasa kama mazungumzo hayo yameandikwa mazungumzo hayawezi kuweko bila ya kuwako na lugha. Bakhtin anasema kuwa lugha huwa na sifa za kisemezano ambazo huchochea na kutawala katika uwandishi wowote ule.

Wamitila (2002:151) anasisitiza kuwa maana ya tamko haina budi kuangaliwa muktadha wa kisemezano, hata matamko ya kuzungumzia nafsi hutegemea kuingiliana kimaana kunakopatikana katika mazungumzo. Kauli hii ya Wamitila ina maana ya kuwa mtu hawezi tu kuongea kama hakuwahi kuulizwa au kuna kauli ambayo inafanya aseme hata kama mtu atawaza akilini mwake kwanza kabla ya kuongea ni kama kufuata kauli ya akilini ambayo ndiyo ya asili kabla hajaitamka.

Nadharia ya Mwingiliano Matini inachukua nafasi ya nadharia ya Semiotiki ambayo imebainika kuwa maana ya matini haitoki kwa mtunzi kumfikia moja kwa moja. Maana ya matini hupitiwa na kuchujwa na ishara ambazo huingizwa na muandishi, na msomaji huzitafsiri kwa kuhusisha na matini husika. Frednand disessaure (2009). Miiongoni mwa wafuasi wanaoiunga mkono nadharia ya mwingiliano matini ni Bathes anayesema kuwa maana ya matini hupatikana pale inapohusishwa na kusaili matini wakati wa mchakato wa kuisoma.

Baada ya kuoneka mwingiliano wa kazi za wasanii na vitabu mbalimbali, nadhara hii ilipokuja ikaleta suluhi ya mwingiliano na ikaonyesha ni kwa namna gani hutokeea.

Nadharia hii ilikuja na kuangalia kazi katika miundo yao ya mwisho kama mambo yanayoungana. Hii ina maana ya kuwa sio wigo wa kazi za msanii aliyetangulia, bali ni athari alizozipata msanii wa pili kutoka kwa msanii wa kwanza.

Katika tasnifu hii nadharia ya Muingiliano Matini ndani ya tasnifu hii imetumika kuonesha ni jinsi gani ishara mbali mbali zilivotumika ili kuleta maana iliookusudiwa ndani ya nyimbo za michezo ya watoto. Kwani nadharia ya muingiliano matini inachukua nafasi ya nadharia ya Semiotiki ambayo inaonesha kuwa maana ya matini hupitiwa na kuchujwa na ishara ambazo huingizwa na mwandishi na msomaji huzitafsiri kuhusisha na matini nyengine Fredinand dessessaure (2009).

2.3.3 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Ni nadharia ya kifasihi inayojikita katika kumuangalia msomaji (hadhira) na uzoefu wake wa kazi za kifasihi. Hii ni tofauti na nadharia nyengine zinazojikita katika msingi wa kumwangalia mwandishi, maudhui na fani katika kazi za fasihi. Nadharia ya mwitiko wa msomaji, iliasisiwa na Stanley Fish (1980), Jane Tompkins (1980) na Wolf Gang Isser (1974), na waasisi wote hawa ni wajerumani. Wanadharia hawa wanasema kuwa kazi ya kifasihi inapaswa kutazamwa kulingana na mila na desturi, au utamaduni wa msomaji, kwani msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake na si kutokana na uzoefu wa mwandishi.

Wanaendelea kusema kuwa, kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira mbali mbali, kwa hivyo kutokana na taswira na ishara hizo, matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja. Mathalani katika wimbo ufuatao:

*“ Watoto wadogo,
Kunywени maziwa,
Akija Raisi,
Muruke ruke kama njiwa stop!”*

Katika wimbo huu inaonekana kuwa maana ya kwanza ni watoto wanatakiwa wawe na tabia ya kunywa maziwa ili wapate afya njema. Na maana ya pili ni kuwa unatakiwa uwe na afya nzuri ili uweze kufanya pirika mbali mbali kama kushangiria Raisi.

Wananadharia hawa huona kazi ya fasihi kuwa ina mapengo mengi ambayo yanamlazimisha msomaji kuyaziba, katika kuyaziba msomaji atajikuta ametunga matini nyengine mpya inayotokana na matini ile asilia, kwa hivyo kazi kubwa ya msomaji ni kusoma kazi kwa ufatiliaji wa hali ya juu kabisa, na hatimae kufasili kazi hiyo kutokana na uzoefu pamoja na uwezo wake. Hivyo nadharia hii hasa ndio ilimvuta mtafiti katika kuchambua data kwa vile ilikuwa haina mipaka maalum katika uchambuzi wake.

2.3.4 Misingi ya Nadharia ya Mwingilianomatini na Uchambuzi Matini

Msanii hutoa kazi yake aliyoikusudia mwenyewe lakini pia hadhira hupata maana ya kazi hiyo na huenda ikawa sawa sawa na ile ya msanii au ikawa tofauti. Matini ya kifasihi huwa haipitiwi na wakati hata kama kipindi kilichoandikiwa kazi hiyo kimeshapita. Kazi zaidi ya moja huweza kuhusiana katika dhamira zake, wahusika wake, na falsafa yake ingawa wasanii walitumia tanzu tofauti na vipindi walivyoandika ni tofauti. Hii ni kutokana na sababu ya kuwa mwandishi hupata

mawazo katika jamii yake au huathiriwa na mtunzi fulani aliyetangulia au matini hiyo ilisomwa na waandishi wote. Maana ya kazi ya fasihi hupatikana kwa kuhusisha na mambo mengine yilio nje ya kazi hiyo kwa mfano matukio makuu ya jamii, historia, maafa na mabadiliko kadhaa ya jamii wanayoishi wasanii na wahakiki.

2.3.5 Misingi ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Kazi ya Sanaa, hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsili ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji wa kazi za fasihi. Vile vile hubainisha jinsi miktadha ya matini isiohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji. Pia hudhihirisha kuwa maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi Wamitila (2002).

2.3.6 Umuhimu wa Nadharia Hizi katika Tasnifu Hii

Nadharia hizi zina umuhimu mkubwa, kwani ndizo zimeongoza uandishi wa tasnifu hii.

Kwanza, kazi yejote ya kisanaa ni lazima ichambuliwe ili yapatikane yale yaliokusudiwa kwa hadhira lengwa, na bila ya kuchambua hivyo, maana huwa haipatikani.

Pili, kazi yejote ya fasihi huundwa na vipengele viwili ambavyo ni fani na maudhui na kupitia fani ndipo hadhira huibua maudhui.

Tatu, kazi ya fasihi inapochambuliwa, hubainika kuwa kuna mambo yanayoingiliana na kufungamana na mambo mbalimbali ya jamii kwa mfano historia.

Nne, muktadha husaidia sana katika kuchambua kazi za Sanaa na hii huonyesha kuwa maudhui huendana na muktadha, mhakiki lazima ajue eneo, jiografia, siasa,

historia ya jamii anayotaka kuihakiki kwani haya yote hujitokeza katika kazi za Sanaa za jamii hiyo. Nyimbo za michezo ya watoto katika tasnifu hii zimefafanuliwa kwa kuhusishwa na mila, dini, shughuli za kiuchumi, na jiografia ya Zanzibari.

Njogu (1997) katika kutilia mkazo hili anasema Msanii hawezi kujitenga na hali za kihistoria zilizomkita au zilizoikumba jamii aizungumziayo, endapo kazi zake zitakuwa na uyakinifu kwa hakika fasihi huathiriwa na matukio ya kihistoria, vile vile historia huathiriwa na fasihi. Akifafanua baada ya Mapinduzi ya Zanzibar 1964 amebaini kuwa zimeyashawishi Mapinduzi hayo kwa mfano Asali chungu (1967) na Nyota ya Rehema (1989).

2.3.7 Hitimisho

Sura hii ya pili imechambua kwa kina dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu, ambazo ni asili ya nyimbo, maana ya Nyimbo, muanisho wa nyimbo, nyimbo za michezo ya watoto na asili yake, dhana ya maadili na umuhimu wake. Dhana ya fani na maudhui imejadiliwa kwa kujikita zaidi katika kipengele cha maadili ya jamii. Mwisho wa sura hii ni ufanuzi wa viunzi vya nadharia viliviyotumika katika tasnifu hii. Sura inayofuata inahusiana na mbinu na vifaa viliviyotumika katika utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia njia, mbinu na vifaa vilivyotumika katika mchakato wa utafiti huu, kuanzia mwanzo katika ukusanyaji wa data hadi mwisho wakati wa kuandika tasnifu hii. Katika sura hii, mambo yaliyojadiliwa ni vyanzo vyatya data vilivyotumika katika utafiti huu, njia, mbinu, zana na vifaa vyatya kukusanya data, sampuli iliyotumika, eneo na mipaka ya utafiti. Mwishoni mwa sura hii imeonesha mkabala na namna ya uchambuzi wa data ulivyoofanyika.

3.2 Njia za Kukusanya Data

Njia ni namna au jinsi ya kufanya au kupatia jambo (TUKI 2004: 310). Utafiti huu umetumia data za msingi na data za upili. Data za msingi (awali) ni zile data ambazo hukusanywa mara ya kwanza na ni za asili (Kothari 2004:95). Data hizi mtafiti alizipata uwandani ambako alienda huko kwa ajili ya kukusanya taarifa. Maeneo aliyokwenda ni Pandani, Uondwe na Mzambarauni na katika shule za Msingi na Maandalizi za Pandani na Mzambarauni.

Alikusanya data hizo kwa njia ya kusikiliza nyimbo wakati watoto wakicheza michezo hiyo na huku wanaimba nyimbo ndani ya michezo yao. Nyimbo hizo mtafiti amezinukuu katika daftari na kwa kutumia kamera ya simu ya "htc". Alipiga picha ili kuyaona yaliyo yakifanywa na watoto. Vile vile msaidizi wa mtafiti alikusanya nyimbo katika shule ya msingi Mzambarauni kwa kuskiliza na kunukuu katika daftari.

Data za upili /fuatizi, ni zile ambazo tayari zilishakusanya na zimeshatumika na zimeshahifadhiwa (Kothari 2004:95). Data hizi mtafiti alizipata kupidia maandiko ya wataalamu mbaliambali aliowarejelea katika utafiti wake, mfano: Senkoro (1988), Sengo na Kiango (1991), Fasihi simulizi ya Zanzibar (1983) nakadhalika. Vilevile data hizi zilipatikana kwa kutumia mitandao na maandiko mbalimbali ya maktabani, kama vile: Makala, Majarida, Tasnifu na vitabu mbalimbali vilivyoandikwa kuhusu nyimbo na nadharia za uhakiki wa kazi za fasihi kwa ujumla.

3.3 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu ni njia ya kufanya jambo kwa urahisi, (BAKITA 2010: 231) Mbinu za ukusanyaji wa data zilizotumika ni usaili, uchunguzi makini, kusikiliza, kurekodi kwa kutumia vyombo vya kidijitali na pamoja na mbinu za kimaktaba. Mtafiti ameona ni vizuri kutumia mbinu hizi kwa sababu utanzu huu ni wakifasihi na hupatikana kwa kuchezwa, kughaniwa na kuimbwa. Pia watu wanaozitumia nyimbo hizi ni watoto waliopo majumbani na mashulenii ambao wengi wao hawajui kusoma na kuandika. Hivyo watafitiwa waliulizwa maswali na majibu yalirikodiwa kwa maandishi na kwa simu kubwa yenyeye camera ya kidijitali ambayo ilinasa sauti na picha.

3.3.1 Mbinu ya Usaili

Mbinu hizi huhusisha maswali ya ana kwa ana ambayo mtafiti anapata taarifa kwa kukutana na watafitiwa, kama walimu, wanafunzi, nakadhalika. Mtafiti amebadilishana mawazo na watafitiwa, na huwa na makutano ya ana kwa ana baina yao. Mtafiti hueleza lengo la utafiti wake na ni kitu gani anachotaka kutoka kwa watafitiwa (Amin 2005:178). Mtafiti alikwenda kuonana na watoto ambao wanazijua

baadhi ya nyimbo za michezo mbalimbali ambao waliimba na kucheza na kutoa maelezo yaliyohitajika. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa kuwaauliza watafitiwa (watoto na walimu wao) kuhusu matumizi ya nyimbo za michezo ya watoto na maana ya baadhi ya nyimbo hizo. Njia hii ni nzuri kwasababu ilimuezesha mtafiti kupata taarifa za kina juu ya mada yake.

3.3.2 Mbinu ya Ushuhudiaji

Mbinu hii ya ushuhudiaji ilifanywa na mtafiti kwa kutembelea kwenye maeneo ambayo watoto wamekusanyika na kuimba. Mtafiti alikwenda huko na kushuhudia nyimbo za watoto ambao aliwaomba wamuimbie nyimbo hizo. Alizirikodi kwenye simu ya kijiditali. Ingawa ilikuwa ni mbinu ya ushuhudiaji mtafiti aliibia kwa kuwaauliza maswali yaliyokuwa yanahusiana na mada inayoshughulikiwa ili iwe ni rahisi wakati wa uchambuzi wa Data husika.

3.3.3 Mbinu ya Kimaktaba

Kothari (2004:110) ameifasili mbinu hii na kusema kuwa inajumuisha uchambuzi wa maandiko kama vile Vitabu, Magazeti, na matini mbali mbali zilizochapishwa. Njia hii inahusisha kupata habari za kina kwa kusoma maandiko na kuangalia taarifa katika vyanzo mbalimbali. Maandiko yanaweza kuwa vitabu, magazeti, makala, hotuba, matangazo, picha na mengine, mfano wa hayo (Amin 2005:177).

Mtafiti amepitia maandiko mbalimbali na kupata nukuu na ufanuzi wa dhana, nadharia na data za kutosha za utafiti wake kulingana na mada, malengo na mipaka ya utafiti.

3.4 Vyanzo vyaa Data

Utafiti huu umetumia vyanzo vyaa utafiti vyaa maktabani na uwandani. Katika chanzo cha maktabani, mtafiti alipitia maandiko mbalimbali kuhusu nyimbo za michezo ya watoto, nadharia na dhana muhimu za utafiti huu katika makavazi ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam na makataba binafsi ya nyumbani kwake. Vilevile mtafiti alisoma kupitia tovuti mbalimbali kupata taarifa za nyimbo za michezo ya watoto, dhana na nadharia zilizohusika katika utafiti huu.

Akiwa uwandani, mtafiti alikwenda Mzambarauni, Pandani na Uondwe - Mtambwe katika shule za Msingi na Maandalizi kwa ajili ya kukusanya nyimbo na pia alisaidiwa na wasaidizi wake kupata nyimbo katika maeneo hayo kwa watafiti wengine majumbani kwao ambako mtafiti hakubahatika kwenda kwa mda huo.

3.5 Zana na Vifaa vyaa Kukusanya Data

Katika kutoa maana ya zana/vifaa TUKI (2002:467) wanasema ni chombo kinachohitajika kufanyia kazi fulani. Utafiti huu umetumia vifaa kama vile kalamu, daftari, kompyuta, simu kubwa yenye kamera ya kidigitali pamoja na kamera yenyewe.

3.5.1 Kalamu na Daftari

Kalamu na daftari ni vifaa viliviyotumika sana wakati wa utafiti huu katika kunukuu nyimbo, ambazo alizipata mtafiti akiwa uwandani. Amevitumia vifaa hivi pia, kuandika dondo na nukuu za wataalamu waliorejelewa wakati mtafiti akiwa maktabani. Rasimu ya mswada wa tasnifu hii pia iliandikwa kwa kutumia vifaa hivi kabla haijachapwa kwenye komputa. Vifaa hivi ni nafuu na vinaweza kubebeka

katika masafa marefu na pia hutunza kumbukumbu kwa muda mrefu vikihifadhiwa kwa umakini.

3.5.2 Kamera na Simu

Mtafiti alitumia kifaa hiki uwandani katika kurikodi sauti na picha za waimbaji wa nyimbo mbalimbali ili zitumike kama data. Kamera na simu zilitumika kurikodia kwa sababu maneno katika nyimbo hutamkwa haraka haraka na iwapo kalamu na daftari vinetumika pekee baadhi ya mistari ya nyimbo inayofuata mahadhi inakuwa ni vigumu kuifuatisha na kuweza kuinukuu. Mtafiti alifaidika na rikodi zake zilizokuwa kwenye kamera na simu, kwa kurikodi kwa utulivu zaidi.

Mtafiti pia amenufaika na kifaa hiki kwa kupata mahadhi na toni za nyimbo wakati zikiimbwa. Mtafiti amekumbana na changamoto katika kutumia kifaa hiki, kama vile baadhi ya watafitiwa kukataa kupigwa picha kwa vile wengine walikuwa ni watoto wadogo sana hata picha hawajaionapo. Pia mtafiti hakuwa na utaalamu wa kutosha juu ya kifaa hiki, kwani kilikuwa na programu nyingi na kwa hivyo ilimlazimu atumie kinasa sauti ili kuepusha upoteaji au kufuta bila kujua kazi alizozichukua kwa kamera na simuya kijiditali.

3.5.3 Komputa na Vifaa Vyake

Komputa ni kifaa kilichotumika sana katika utafiti huu, mtafiti alikitumia kuchapa tasnifu hii yote tokeya mwazo hadi mwisho (tasnifu yenewe). Komputa pia ilitumika kupakuwa majorida, vitabu na nukuu kutoka mtandaoni zinazohusu dhana na nadharia muhimu zilizotumika katika utafiti huu na pia ilitumika kuhifadhi data za

utafiti. Matumizi mengine ya kifaa hiki ni yale ya kumuezesha mtafiti kuwasiliana na msimamizi wake wakati akiwa safarini nje ya nchi.

3.6 Sampuli

Sampuli ni vitafitiwa au watafitiwa waliochaguliwa kwa ajili ya kuwakilisha utafiti au watafitiwa wengine wa aina hiyo kutoka katika kundi kubwa. Usampulishaji ni mpango wakuchagua sampuli maalum kutoka katika kundi kubwa (Kothari 2004:55-56). Amini (2005:236) anafafanua kuwa sampuli hupatikana kwa kuchagua sehemu tu kutoka katika kundi kubwa na matokeo yake yanaweza kujumuishwa kwa kundi lote la watafitiwa. Sampuli lazima iwakilishe watafitiwa wake na kadiri itakavyowezekana, vile vile sifa zote za kundi zipatikane katika sampuli ilyochaguliwa kulingana na mada ya utafiti husika, kwa mfano dini, jinsi, kiwango cha elimu nakadhalika.

Nussu (2012:41) akimnukuu Babbie (1999:107) anaeleza kwamba ni vigumu kwa mtafiti kushughulikia idadi kubwa ya wanajamii wanaohusika katika utafiti hata kama anavutiwa na wanajamii hao. Mtafiti hutakiwa kuchagua idadi maalum ya wanajamii wa kushughulikia katika utafiti wake. Idadi hiyo ya wanajamii lengwa, mtafiti alichagua wanafunzi (21) kwa kutumia visampulishaji nasibu saba kutoka kila shehia ya utafiti, yaani Pandani, Mzambarauni na shule ya Uwondwe Msingi na Maandalizi.

Watafitiwa hawa waliimba nyimbo zinazotokana na michezo mbali mbali, watoto hao na walimu wao walizitolea ufanuzi wakutosha wa chanzo pamoja na maana yake. Hivyo basi tasnifu hii imetumia sampuli ya nyimbo arobain na mbili (42) kama

zitakavyoonekana katika kiambatanisho. Nyimbo hizi zimeteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Mtafiti ameteuwa nyimbo kwa kuamini kuwa zitampatia data na taarifa zitakazomsaidia kujibu maswali ya utafiti wake. Nyimbo hizi pia zilitumika kama vyanzo vya data na taarifa za msingi zilizowezesha kujibu maswali katika tasnifu hii. Sampuli lengwa ndiyo inayomuwezesha mtafiti kuteuwa nyimbo za michezo ya watoto za shule za Msingi na Maandalizi, Mzambarauni, Pandani na Uwondwe katika mkoa wa kaskazini Pemba wilaya ya Wete.

3.7 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika sehemu zote mbili, yaani Uwandani na Maktabani. Kwa upande wa Uwandani, utafiti huu umefanyika Zanzibar katika kisiwa cha Pemba Wilaya ya Wete mkoa wa Kaskazini Pemba ndani ya miji ya Pandani, Uwondwe na Mzambarauni katika shule za Msingi na Maandalizi. Mtafiti alichagua maeneo haya kwa sababu bado wanafunzi wanaendelea kuimba katika muda maalum wa michezo. Na pia ni maeneo ambayo mtafiti alikuwa na uhakika wa kupata data kwa urahisi na kwa vile wasaidizi wake wengi wako katika maeneo hayo.

Sababu nyengine ni kwamba watu wengi wanaofanya utafiti katika kisiwa cha Pemba hufanyia mkoa wa kusini tu wilaya ya Chake Chake na kusahau kabisa mkoa wa Kaskazini na wilaya ya Wete. Sababu nyengine mkoa wa kaskazini, wilaya ya Wete, ni mkoa ambao mtafiti kazaliwa katika kijiji cha Pandani, hivyo ni rahisi kupata data.

Na kwa upande wa maktabani, utafiti huu ulifanyika katika sehemu tofauti tofauti, kama vile, maktaba ya Chake Chake Pemba mkoa wa Kusini, maktaba ya Vuga Zanzibar, na kumalizia maktaba kuu Dar:es:salaam.

3.8 Mipaka ya Utafiti

Tasnifu hii imeangalia mifano mbalimbali ya nyimbo za michezo ya watoto ambazo ndani yake zina maana ya kimaadili, pia umeangalia ni jinsi gani nyimbo za michezo ya watoto zinavyosaidia kujenga maadili ya jamii. Aidha imeangalia ni mchango gani unapatikana katika jamii ya wapemba kupitia nyimbo hizi.

Pia tasnifu hii imeangalia vipengele vyta fani kama vile matumizi ya methali, misemo, tamathali za semi na mitindo mbali mbali kama vile mtindo wa maswali, majibizano, kutumia ukale wa miji na mitaa nakadhalika. Kupitia vipengele hivi mtafiti alipata kujuu kwa mapana zaidi munafunzwa nini ndani ya nyimbo za michezo ya watoto, ambapo nadharia ya mwitiko wa msomaji, uchambuzi matini na mwingiliano matini zilisaidia katika kuchanganua data hizi.

3.9 Uchambuzi wa Data

Kothari (2004:18 - 122) anasema kuwa baada ya kukusanya Data inampasa mtafiti kuzichakata na kuzichambua Data kwa kurejelea malengo ya utafiti. Uchambuzi wa Data hufanyika kwa kupitia hatua kadhaa kama vile uwekaji wa misimbo, ujedwalishaji, uhariri na inapolazimu kunakuwa na uchoraji wa michoro ya kitakwimu kwa lengo ya kuyafupisha maelezo. Utafiti huu umetumia mkabala wa kimaelezo katika kuchambua na kuzichakata Data zilizokusanywa. Mkabala huu umetumika kwasababu Data ni matini za sayansi ya jamii (fasihii) na uchambuzi wake ni wamaelezo.

3.10 Hitimisho

Sura hii ya tatu imeeleza njia na mbinu zilizotumika katika kufanya utafiti huu. Kwa kuanzia na vyanzo vyta Data, njia za kukusanya Data, mbinu zilizotumika katika

kukusanya Data hizo, dhana na vifaa vilivytumika kukusanya Data wakati mtafiti akiwa uwandani, maktabani na pia wakati wa kuanda mswada huu wa tasnifu yake. Sampuli ya utafiti huu ni nyimbo arubaini na mbili (42) ambazo zimechambuliwa katika tasnifu hii. Eneo lililofanyiwa utafiti huu ni kisiwa cha Pemba wilaya ya Wete kijiji cha Pandani, Mzambarauni na Uwondwe pamoja na mipaka ya utafiti. Mwisho sura hii imeonesha namna data zitakavyochakatwa, kuchambuliwa na namna zitakavyo jibu maswali ya utafiti huu na hatimae kukamilika kwa tasnifu hii.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI WA DATA, UCHAMBUZI NA MJADALA

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua data zilizopatikana uwandani na maktabani. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia misingi na kanuni za viunzi nya nadharia ya Mwingiliano Matini na Mwitiko wa Msomaji. Uchambuzi na mjadala huu umelenga kujibu maswali ya tasnifu hii kukamilisha malengo ya utafiti huu.

Sura hii imegawika sehemu kuu tatu zifuatazo:

Sehemu ya kwanza: Sehemu hii imesawiri mifano mbalimbali ya nyimbo za michezo ya watoto. Mifano hiyo imepatikana uwandani (Pandani, Uondwe, na Mzambarauni).

Sehemu ya pili: Sehemu hii imechambua usanii uliojitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto na jinsi ulivyoibua maudhui.

Sehemu ya tatu: Hii inalenga kusawiri dhamira ambazo zimejitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto katika kujenga maadili ya jamii.

Amir et al (1983) anaeleza kuwa nyimbo za michezo ya watoto huwa inatumia lugha nzito, yenye mafumbo, na picha, kwa hivyo inkuwa ni vigumu kuhakikiujumbe uliomo ndani yake.

Baadhi ya watafitiwa kama vile Maalim Ramla wa shule ya Mzambarauni na wanafunzi wake, waliofafitiwa februari (2015) walisema kuwa, “ni kweli, lugha ya nyimbo hizi ni nzito, inakuwa vigumu kuzifafanua kwa urahisi ila watoto huzitumia kwa kujichangamsha tu na kujifurahisha”.

Bi Fatma wa Uwondwe na Maalim Ali wa Pandani pamoja na wanafunzi wao, waliotafitiwa februari (2015), walitilia mkazo suala hili la ugumu wa lugha katika nyimbo hizi, isipokuwa watoto huzitumia tu kwa kujifurahisha. Lakini ukweli ni kwamba kupitia nyimbo za michezo ya watoto, munafunzwa mengi tu ambayo yanaendana na maadili ya jamii ya Pemba. Mafunzo ya nyimbo mbali mbali za watoto ambayo yanafafanuliwa katika sura hii kwa uwazi kama ifuatavyo.

4.2 Mifano ya Nyimbo Mbalimbali za Michezo ya Watoto

4.2.1 Ukuti Ukuti

Ukuti ni wimbo na jina la mchezo wenyewe pia, Mchezo huu huchezwa na watoto wenyewe wakiwa wamejipanga kwa mtindo wa kufanya duara na huku wameshikana mikono na kukamilisha duara zima. Katika kufanya hivyo, watoto hujikuta wanazunguka kwa mendo wa mbio na huku wanaimba kama hivi:

“Ukuti ukuti,

Wa mnazi wa mnazi

Mwenzetu mwenzetu,

Kapondwa kapondwa,

Na nini na nini?

Na gari na gari,

Tukampelekeni hospitali, atakaeanguka, shauri yake,

Mama huyu alia lia, pa pa pa pa.....”

Maana ya wimbo huu ni kuwa, wanajamii wanatakiwa wawe na tabia ya kwenda hospitali pale wanapopatwa na ajali ya aina yoyote ile, badala ya kukimbilia kwenye tiba za kiasili (kiganga) au kujikalia nyumbani tu. Baadhi ya watafitiwa walitilia

mkazo suala hili kwa kusema: Wanajamii waliowengi sasa hivi wamelemaa na tabia za tiba za kiganga, jambo ambalo hupelekea vifo vyta mara kwa mara, wakatoa mfano wa nyumbani pao wanapoishi, kijiji cha Kele kuwa tabia hii ipo kwa kiwango cha juu sana. Hivyo jamii inaadilishwa iachane na tabia ya kutegemea tiba ya uganga pekee.

4.2.2 Kula Mbakishie Baba

Hili ni jina la wimbo na pia ni jina la mchezo. Katika mchezo huu, watoto kike na wakiume kwa pamoja hujikusanya kwenye duara moja, wakiwa wamekaa kitako na huku wameweka chungu ya mchanga kati kati, na katikati ya mchanga huwekwa kijiti, wakiwa wanaimba wimbo huu, hufanya ishara ya kuchota tongue kwa kila mmoja, mpaka wanabakisha kidogo, mwisho wanakula mpaka atakaekiangusha kijiti hicho anafukuzwa na wenzake , wimbo wenyewe ni huu:

“ Tule tumbakishie baba

Tule tumbakishie baba

Tule tumbakishie baba...”

Katika wimbo huu jamii inafunzwa kuweka akiba na kuwakumbuka na wenzao katika jambo lolote la kheri. Pia watoto nyumbani wanafunzwa tabia ya kuacha uroho na kwamba yoyote mwenye tabia ya uroho siku zote hupaswa kuadhibiwa ili aachane na tabia hiyo

4.2.3 Kiguru Cheche

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, ambao huchezwa na watoto wenyewe kwa kujipanga duara na huku kila mmoja akiwa amenyoosha mguu mmoja na mwingine umesimama na huku wanaruka ruka na kuimba kama ifuatavyo,

*"Kiguru cheche, cheche cheche,
 Alo na donda, tumtoneshe,
 Alo na jipu, tumtumbue,
 Alo na chawa, tumparure,
 Kiguru cheche, cheche cheche."*

Nyimbo hii, inafunzwa jamii iachane na tabia ya uchafu, na ishikamane na tabia ya usafi, ili kuepukana na maradhi na mwenye maradhi hatakiwi kuyafuga na badala yake afanye tiba za maradhi husika ikiwa ni pamoja na kwenda hospitali haraka iwezekanavyo.

4.2.4 Baba Uyo

Hili ni jina la wimbo, na jina la mchezo wenyewe mchezo huu huchezwa watoto wakiwa wamesimama na kupanga mstari mmoja na huku wakiimba na kushangilia kwa makofi, Watoto huimba wimbo ufuatao.

*"Baba uyo
 Atoka Rwanda,
 Na mkungu wa ndizi,
 Baba baba uyo"*

Wimbo huu unawafunza wanajamii hususan watoto, kuwa na heshima kwa wazazi wao, ikiwa ni pamoja na kuwapokea wakubwa pindi wawakutapo njiani. Wazee nao kwa upande wao wanatakiwa wawe na ucheshi na watoto wao, ili wajenge mapenzi kwao.

4.2.5 Yai Bovu

Hili ni jina la wimbo, na jina la mchezo wenyewe. Kupitia mchezo huu, watoto huipanga duara moja na huku wanaimba kwa kupiga makofi kama ifuatavyo,

“Yai bovu, yai bovu

Linanuka linanuka

Linanukaje, linanukaje

Hm hm lishachachacha,

Macho juu juu, macho chini chini,

Macho juu juu, macho chini chini,

Watoto msitizame nyuma,

Yai bovu linanuka”

Maana ya wimbo huu, wanafunzwa akina mama wakiwa kwenye hedhi wawe nadhifu ili wasitoe harufu pindi wakaapo na wenzao. Pia wanafunzwa wanajamii kuwa baadhi ya maeneo ni mwiko hivyo hayafai kupitwa wala kufanyiwa upekuzi wa aina yoyote ile kama vile Giningi nakadhalika. Hata hivyo kupitia wimbo huu jamii inaaswa kuwa na tabia ya kutizama huku na kule pindi watembeapo barabarani ili kuepusha ajali za barabarani. Baadhi ya watafitiwa kama vile Maalim Ramla wa Skuli ya Mzambarauni alitilia nyama hili kwa kusema siku hizi watoto wengi hupata ajali kwa kutoangalia huku wala kule wakati anapokata barabara.

4.2.6 Mabata

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, katika kucheza mchezo huu, watoto huipanga mistari miwili, wanachuchumaa na kufunga mikono yao mithili ya

kipapatiko kumaanisha eti ndio mabawa ya bata mwenyewe. Hapo hucheza na kuimba huku wakirusha vile vipapatiko juu na chini kama wimbo unavyoonesha.

“Mabata madogo dogo,

Yanaogelea, yanaogelea,

Katika shamba zuri la bustani,

Wanapenda kutembea,

Bila viatu, bila viatu,

Katika shamba zuri la bustani,

Na mabawa yao yanalia kwakwa, kwakwa,

Kwakwa, kwakwa, kwakwa”

Maana haswa iliyokusudiwa katika wimbo huu walipohojwa watafitiwa wa shule ya Mzambarauni, walisema kuwa, inasisitiza uhuru wa mtu binafsi kwamba ili mtu aishi maisha ya raha duniani basi suala la uhuru ni muhimu, walitoa mfano, wa mwanamke anatakiwa apewe uhuru wa kujichagulia mchumba mwenyewe hapo ataishi mithili ya bata akiwa katika shamba zuri la bustani.

4.2.7 Nani Kaona Upepo

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, mchezo huu kama ambavyo mtafiti aliwaona wanafunzi wa shule ya maandalizi ya Pandani wakicheza wakiwa watoto wamekaa kwenye vikalio vyao huku wanaimba na kupiga makofi, wakionesha na ishara mbali mbali zinazopatikana katika wimbo huu kama unavyoonesha wimbo ufuatao.

“Nani kaona upepo,

Si mimi wala si wewe,

*Unapopita chini ya mti,
Majani hupeperuka”*

Kupitia wimbo huu, mtafiti alipowahoji watafitiwa wa shule ya Maandalizi Pandani walimu walijibu kuwa wimbo huu unaonesha uweza wa Allah (s.w) ulivyo mkubwa ya kwamba upopo ni kitu ambacho hakionekani kwa macho lakini hewa nzuri tunayopata ni ya ajabu, jambo ambalo hawezi kulifanya yoyote isipokuwa ALLAH (sw).

4.2.8 Ainaku Tabal Amsi

Ni jina la wimbo na ni mchezo wenyewe, ambapo katika mchezo huu, mara nyingi washiriki huwa ni wawili, mmoja anauliza maswali na mwengine anajibu kama ifuatavyo.

*“Ainakum tabil amsi, ulikuwa wapi jana
Kuntum maridhwa, nilikua ni mgonjwa
Alwaa jantu dawa, vipi ulipata dawa
Dawa jantum, hapana sikupata
Bal-ash-rab maa, bali nilikunywa maji
Allahu ya shafiy, Mungu akaniponesha”*

Kupitia wimbo huu, mtafiti katika uchambuzi wake wa data aliona kuwa, maana yake hasa ni utegemezi kutoka kwa muumba wa mbingu na ardhi, ambae ndie mponeshaji wa maradhi yote, na kwa vile Pemba asilimia kubwa ni waislamu, basi huwa wanamtegemea Allah kwa kila kitu, kama ambavyo wanafunzi wa Uondwe Msingi walivyothibitisha juu ya hilo.

4.2.9 Vitu Vyenyе Uhаi

Hili ni jina la wimbo, ama ndio mchezo wenyewe. Mchezo huu huchezwa na watoto wenyewe wakiwa wameshikana mikono na kuipeleka huku na huku wakionesha ishara mbali mbali za vitu hivyo.kama wimbo unavyoonesha:

“Vitu vyenyе uhаi, vitu vyenyе uhаi,

Watu, wanyama na miti. Watu wanyama na miti

Visivyo uhаi, meza kabati na viti

Visivyo uhаi, meza kabati na viti.”

Katika mchezo huu, maana ya wimbo ambayo ilitolewa na watafitiwa wa shule ya msingi Pandani, ilionesha kuwa wimbo huu unamaanisha kuwa katika ulimwengu kuna vitu vya aina mbili ambavyo vinatumika katika maisha ya kila siku. Vitu hivyo vinatokana na uweza wa Allah [s.w]. Navyo ni vitu vyenyе uhаi na visivyo na uhаi kama ambavyo vimeainishwa katika wimbo.

4.2.10 Tumbili Walani?

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, mchezo huu, huchezwa na watoto wakiwa wamejipanga duara na huku wamekamatana mikono,wakati wakiimba wimbo huu,huwa wanainama juu na chini na huku wanakwenda kwa kasi.kama wimbo unavoonesha.

“Tumbili walani

Nala komamanga,

Nigaie nami, nikampe mwanangwa,

Akija akifa

Nitatoa sanda na kombe la wanja.

Kidege zunguruka, hata ukichoka inama inuka”

Mtafiti alipowahoji watafitiwa wa shule ya Msingi Mzambarauni walifafanua maana ya wimbo huu kuwa, katika jamii ya Wapemba siku zote kitu ama tunda akishalila mnyama, ni miko au si vizuri kitu hicho akakila binaadamu wa kawaida kwani huenda ikawa mate ya mnyama huyo na binaadamu hayaendani. Hivyo ikawa ni dhara au ni sababu ya kifo kabisa. Watafitiwa hao waliendelea kufafanua kuwa, na ndio maana siku hizi serikali imetukataza tusile matunda yaliyobebenywa na wanyama ili kupiga vita maradhi mbalimbali kwa mfano ugonjwa wa EBOLA.

4.2.11 Anjikicha

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, katika kucheza mchezo huu, watoto hujipanga wawili wawili wakiwa wamekaa kitako na huku wanaimba wimbo ufuatao kwa kupigana vikofi vya mikono

“Anjikicha, anjikicha, anjikicha anjikicha, anjikicha, anjikicha.

Nilikwenda, nilikwenda Darisalama Darisalama Darisalama,

Nikala, nikala, nikala wali kwa nyama, wali kwa nyama

Tonge ya kwanza ikanipita x3

Tonge ya pili ikanisama, ikanisama, ikanisama,

Kibibi kanipe maji, kanipe maji, kanipe maji,

Kibwana kanitukana, kanitukana kanitukana,

Kwaheri nakwenda zangu x3

Anjikicha x3 njikicha x3

Kwa upande wa maana ya wimbo huu, watafitiwa wote walisema kuwa, wimbo huu unamaanisha mtu akitaka kula anatakiwa aweke maji, kwani kinyume na hivyo chakula kitakuja kumsakama kama wimbo ulivyoonesha. Aidha katika kufafanua wimbo huu watafitiwa wa Shule ya Uondwe Msingi, walisema katika jamii ya Wapemba kwa vile asilimia kubwa ni waislamu, ni jambo la lazima kula chakula wakaweka maji kama ambavyo dini yao inavyowasisitiza kufanya hivyo.

4.2.12 Chagua Mwenzako

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, mtafiti aliwaona watafitiwa kwa njia ya kushuhudia wakati wanacheza mchezo huu, watoto walijipanga duara wakiwa wamesimama, mmoja anaingia kati na huku wanaimba kama ifutavyo,

“Chagua mwenzako, chagua mwenzako,

Zamani tulifanya,

Umpeleke disco, umpeleke diskoo

Zamani tulifanya,

Cheza nae dansa,

Zamani tulifanya,

Umrejeshe hapa, umrejeshe haa,

Zamani tulifanya,

Mwambie kwaheri, mwambie kwaheri,

Zamani tulifanya”

Katika wimbo huu, mtafiti kuititia maana mbali mbali zilizotolewa na watafitiwa, alibaini kuwa wimbo huu unamaanisha urithi wa tamaduni kutoka kizazi kimoja hadi

kingine. Kwa maana pana umuhimu mkubwa wa kuiga tamaduni zinazofaa katika jamii ili kuzikuza ama kuziendeleza tamaduni hizo.

4.2.13 Kichupa

Kichupa ni jina la wimbo na la mchezo wenyewe, mtafiti aliwahushuhudia watafitiwa wa shule ya msingi Pandani wakiwa wanacheza mchezo huu kwa kutumia mbinu ya ushuhuda wakiwa wamo mchezoni watoto hubebana lakini kifudi fudi na huku wanaimba wimbo ufuatao.

*“Kichupaaaaaaaa, kichupaaaaaaaa,
Cha mafuta mazuri,
Ukilala, chanukia vizuri,
Kichupa cha mafuta mazuri”*

Kwa upande wa maana wa wimbo huu, ndani ya mchezo huu, ilibidi mtafiti aonane na watafitiwa walimu wa shule hiyo kwani mtafiti hakuridhika na maoni ya watoto tu, katika kufafanua maana ya wimbo huu, walisema kuwa, wimbo unamaanisha mwanamke ambae analala na mume wake anatakiwa ajitie manukato mazuri ili kumfurahisha bwana. Wakaongezea kwa kusema hali kama hio inapelekea kudumu kwa ndoa.

4.2.14 Sisimizi

Sisimizi, ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, katika mchezo huu watotohujipanga mistari miwili wakiwa wameelekeana na huku wanapiga njiwe chini na wimbo ufuatao,

*“Sisimizi mbio mbio,
 Wenda wapi na kilio,
 Nenda huko matangani,
 Ni nani aliekufa,
 Mzungu na baniani,
 Raha waringia nini, shingo kipapatiko na ini,
 Waringia nini, shingo, kipapatiko na ini.”*

Kwa upande wa maana wa wimbo huu, mtafiti alibahatika kuwahoji watafitiwa wote, katika nyakati na siku tofauti, hapa wimbo huu ukafafanuliwa kwa maana tatu tofauti kama ifuatavyo:

Kwanza wimbo huu unamaanisha kuwa mionganini mwa mambo ambayo yanatakiwa yaharakishwe ndani ya jamii ya Pemba kwa vile ni waislamu karibuni wote ni suala la maiti kuzikwa. Pili wimbo huu unamaanisha kuwa binadamu hatakiwi kuringa kwani hana cha kuringia, tatu wimbo huu unakumbusha enzi walizotawala wazungu na wahindi katika visiwa vyta Zanzibar na kuwatumikisha watu kama punda, sasa kuondoka kwa watu hawa ilikua ni furaha kwa wazanzibari.

4.2.15 Kitango Malemale

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, kupitia mchezo huu, mtafiti alibahatika kuwaona watafitiwa wa shule ya Uondwe Msingi kwa macho yake, kwa njia ya ushuhudiaji katika kucheza mchezo watoto huipanga mstari mmoja wakiwa wamekaa kitako na huku wanaelekeza vichwa vyao huku na kule wakiwa wanaimba wimbo ufuataao.

*Kitango male male,
Huku mawili na huku mawili mane.*

Walipohojiwa watafitiwa kuhusu wimbo huu, kwa upande wa maana walisema, wimbo huu unamaanisha watoto kujifunza maswali ya Hisabati kabla hawajaenda shule, ili wakifika shule iwe ni rahisi kujifunza.

4.2.16 Majani ya Mdimu

Majani ya mdimu ni wimbo na ni jina la mchezo wenyewe, mchezo huu huchezwa na watoto wenyewe wakiwa wamejipanga duara na huku wamekaa kitako wakiwa wameviweka pamoja viganja vyao kwa pamoja kila mtu na vyake, wakati wanacheza, wanasaga viganja vyao na kuvitupa chini na huku wanaimba wimbo ufuatao:

*”Majani ya mdimu, majani ya mdimu,
Saga saga saga saga---
Funika, funua, funua, funika,
Shahada mara tatu,
I, 2, 3...”*

Ama walipohojiwa watafitiwa wa shule ya Pandani kuhusu maana ya wimbo huu, walifafanua kuwa wimbo huu unawaamsha watoto waweze kupambana na mambo ya ushindani. Maalim wa shule hiyo Bi Mashavu alikazia mkono kauli hiyo kwa kusema ni vizuri watoto wetu wapambane tokea hivi sasa hususan katika masomo yao ili waweze kukabiliana na ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia.

4.2.17 Mnara wa Njiwa

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe. Katika kucheza mchezo huu, watoto hukaa kitako chini na kujipanga duara na huku kila mmoja akiwa kakamata njiwe mkononi anaipiga piga na chini njiwe hiyo na pia wanabadilishana lakini katika mwendo wa kasi, na huku wanaimba wimbo ufuatao.

“Mnara mnara,

Mnara njiwa,

Akija baba,

Nitamwambia,

Kunguru mweupe, kaota mkia,

Akosae, abinywe ukucha---,

Nikitaka kwenda Tanga, Tanga kuna umande Tanga,

Nikitaka kwenda unguja, Unguja kuna umande Unguja,

1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, 8, 9, 10,”

Watafitiwa wa shule ya Mzambarauni, walisema kuwa wimbo huu maana yake hasa ni kuwaadilisha watoto watulie, wawe na heshima na adabu nzuri kwani mtoto akikosa yote hayo huwafedhehesha wazee wake na yeze mwenyewe, kwa kutilia nyama hili, Maalim Said, aliongezea kwa kusema ni kweli hayo hasa ukizingatia wazee wa jamii ya Wapemba ni watu na heshima zao.

4.2.18 Chakula Bora

Chakula bora ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe. Kupitia wimbo huu, mtafiti alibahatika kuwaona watafitiwa wa shule ya Maandalizi ya Pandani kwa kutumia mbinu ya uchunguzi makini, wakiwa mchezoni watafitiwa hao, walikua

wamekaa kwa pamoja wanaimba wimbo ufuatao wakiwa wameshika baadhi ya hivyo vyakula kama sehemu ya kuonesha ishara ya vyakula vyenyewe, wimbo wenyewe ni:

*“Chakula bora chakula bora,
Hima tumieni, aaa tumieni, hima tumieni,
Tulen i chakula bora, masihara tuachen i,
Tuepuke na madhara na madhara mwilini,
Mboga maziwa na nyama, visibakie dishini,
Chakula bora chakula bora, hima tumieni, hima tumieni”.*

Ama kwa upande wa maana ya wimbo huu, mtafiti katika kuwahoji watafitiwa hao maana ya wimbo huu ni kuwa watoto wanatakiwa wapewe vyakula vizuri ili wajengeke kiafya kwani afya nzuri ni muhimu kwa kiumbe chochote chenye uhai. Katika kukazia juu ya hili mtafitiwa mwengine ambae ni mwalimu Bi Asha, alisema hata miti nayo ikikosa udongo wa rutba basi haikui vizuri.

4.2.19 Elimu

Ni jina la mchezo wenyewe, ambapo katika mchezo huu, watoto hujipanga mistari miwili wa kike na wakiume kana kwamba wako darasani, halafu katika mikono yao hukamata vijiti kwa kiashirio cha kalamu ama penseli katika wimbo huu mwisho kuna vawel ambao watoto huzitaja na huku wanaandika chini harufi hizo kama ifuatavyo.

*“ Baba na mama msinikataze,
Kwenda skuli kusoma,*

Elimu ya sasa kama chai ya moto,

Ukinywa upulizie a, e,i,o,u... ”

Kwa maana hasa ya wimbo huu, mtafitiwa alibahatika kukutana na watafitiwa wa shule ya msingi ya Pandani na Mzambarauni katika kufafanua maana hasa ya wimbo huu watafitiwa walisema wazazi wanatakiwa wasitunyime sisi watoto haki yetu ya kupata elimu kwasababu elimu ni ufunguo wa maisha yetu.

4.2.20 Jina Lako Nani?

Jina lako nani ni mchezo ambao huchezwa na watoto wenyewe wakiwa wamejipanga duara na wakiwa wanarusha mikono huku na kule, kwa ishara ya furaha kutoka katika miyo yao na huku wanaimba wimbo ufuatao.

“Jina lako nani yoyoyo,

Jina langu Sami yoyoyo,

Unaishi wapi yoyoyo,

Naishi Semewani yoyoyo,

Wamtaka nani yoyoyo,

Namtaka Ali yoyoyo,

Japo kuwa humtaki mama nalia,

Cheza nae na msondo mama nalia,

Haya tikisa bega, tikisa bega, tikisa bega,

Haya kata mauno, kata mauno, kata mauno.”

Katika kufafanua maana ya wimbo huu watafitiwa wa shule ya Uondwe Msingi walisema, wimbo huu unawaandaa watoto kabla hawajaanza kusoma angalau kujuwa

vitu mbali mbali vikiwemo majina yao, Pia kupitia wimbo huu watoto hupata mazoezi ya viungo, hata hivyo kupitia wimbo huu watoto hususan wa kike hupata kujua haki zao zikiwemo za kujichagulia wachumba.

4.2.21 Safari Yetu

Safari yetu ni jina la wimbo katika mchezo wa watoto wa jamii ya kipemba, ambapo mchezo huu aghlabu watoto huimba wakiwa katika safari mbali mbali kama vile za vyombo vya moto, katika kucheza mchezo huu, watoto hao hujipanga kwa pamoja mathalani kwenye gari na huku wakiimba wimbo ufuatao kwa sauti ya upole kama ya kuomba dua.

“Safari yetu, amba,

Ni ndefu sana, amba,

Ina vikwazo, amba,

Vya kila aina, amba,

Mola jalia amba, tufike salama,

Mola jalia amba, tufike salama

Kwa upande wa maana ya wimbo huu watafitiwa karibuni wote walilingana kwa kusema wimbo unaonesha kuwa siku zote mtu anapoenda safari anatakiwa asome dua, ama baada au kabla ya safari hio na hususan vyombo vya moto kwani ndivyo vyenye ajali ya mara kwa mara.

4.2.22 Jungu la Uji

Jungu la uji ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, katika kucheza mchezo huu, watoto hujipanga kwa pamoja katika duara wakiwa wamesimama na huku

wameshikana mikono kama ishara ya umoja wa jamii ya Wapemba katika kuzunguka kwa mbio huku wanaimba wimbo ufuatao.

*“ Jungu la uji, jungu la uji
 Halipwagi, halipwagi,
 Hata likipwaga, lapwagia mahaba,
 Mtoto akitaka soma, mpelekeni Qurani kwanza,
 Usimbio na uende mbio,
 Usimbio na uende mbio”*

Ama kwa upande wa maana ya wimbo huu, pia watafitiwa karibuni wote walilingana kwa kusema, katika wimbo huu wazazi wanahimizwa kuwa elimu ya mwanzo ambayo watoto wa jamii ya Kipemba wanayotakiwa waipate ni elimu ya Qurani ambayo hulenga katika kumjua mola wao na uwezo wake kwa ujumla.

4.2.23 Kanambia Baba Nichupe

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe. Kwa kutumia mbinu ya ushuhuda, mtafiti aliwashuhudia watafitiwa wa shule za Maandalizi zote tatu, yaani Pandani, Mzambarauni, na Uondwe wakiwa wamesimama kwenye vizingiti vyatya milango yao ya madarasa, ukizingatia vizingiti hivo ni vikubwa kwa wao, lakini mtafiti alipouliza juu ya hatari ya hapo, alijibiwa kuwa ndio mchezo wenyewe unavokuwa, watafitiwa waliimba wimbo ufuatao na kila wakifika karibu na mwisho hujirusha.

*“Kanambia baba nichupe,
 Kama siwezi kuchupa,
 Chupu chupu chupu,
 CHUUUUU... ”*

Kwa upande wa maana ya wimbo, watafitiwa walimu, walisema kuwa maana hasa ya wimbo huu ni kuwapa watoto mazoezi ya viungo vya mwili.

4.2.23 Samaki

Hili ni jina la wimbo na jina la mchezo wenyewe, katika kucheza mchezo huu, watoto hususan wa kiume, huipanga mstari mmoja wakiwa wamechutama mithili ya watu watakao vua na huku wanaimba wimbo ufuatao.

*“Nilimpata samaki, mkubwa mno,
Na wewe mwenye nguvu, kwanini ukamuachia,
Kanitafuna kidole, nalia iii mama, nalia ii.”*

Ama kwa upande wa maana ya wimbo huu, mtafiti baada ya kuwahoji watafitiwa, alijibiwa kuwa, wimbo unatoa tahadhari juu ya madhara ya samaki wakubwa na thamani ya mama katika jamii ya Wapemba.

4.2.24 Wakati

*Kengele lialia, na saa zimefika,
Mama leo tumbo laniuma, siwezi kusoma soma,
Walimu sisi sisi, daktari sisi sisi,
Tulivute dau la elimu, lisirudi nyuma nyuma”.*

Maana ya wimbo huu kwa ujumla ilipatikana pale mtafitiwa wa shule ya msingi ya Uondwe aliposema kuwa, walimu mashulen i wanatakiwa wajali muda wa kuwatoa wanafunzi kwenda makwao ukizingatia watoto wengine ni wadogo sana

hawastahamili njaa, na maana ya pili ni umuhimu wa elimu katika maisha ya kila siku.

4.3 Usanii Unaojitokeza Katika Nyimbo za Michezo ya Watoto

Kwa mujibu wa Kitabu Teule Kidato cha Tatu na cha Nne (2005) wanafafanua kuwa, Usanii ni ubunifu wa kisanaa ambao hutumiwa na msanii katika kazi za fasihi kwa ajili ya kupamba kazi yake na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii. Maana hiyo ilitosha kwa mtafiti kuendelea kuufafanua usanii uliojitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto. Ubunifu huo ni kama vile matumizi ya methali, misemo, nahau, ibara, picha, tamathali za semi nakadhalika.

Usanii unaotumika katika nyimbo za michezo ya watoto ni mwingi, katika tasnifu hii usanii uliotumika ni kama vile matumizi ya mitindo mbalimbali, matumizi ya methali , matumizi ya misemo, matumizi ya tamathali za semi , matumizi ya tanakali za sauti , matumizi ya taswira mbalimbali, nakadhalika.

4.3.1 Matumizi ya Methali na Misemo

4.3.1.1 Matumizi ya Methali

TUKI (2004: 240) na Mauya (2006:1) wanasema kuwa methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa ni usemi unaotoa matunzo ya ukweli. Methali pia hutumiwa kufumbia au kutolea mfano matukio mbalimbali katika jamii na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumika. Methali hutumiwa kwa lengo la kuonya, kuadilisha na kuongoza jamii katika mambo mbalimbali.

Utafiti huu umefanyaika katika kisiwa cha Pemba ambapo watu wake takribani asilimia tisiini na tisa ni wafuasi wa dini ya Kiislamu. Katika suala zima la kuwalea na kuwakuza watoto katika mila za Kiislamu ni mtoto kuanza masomo yake katika vyuo vya Qur-ani ambapo ataanza kujengeka kwa kumtegemea Allah pekee, ambayo ndio nyenzo kuu ya Uislamu. Katika jamii kumezuka shule nyingi za watoto wadogo za kujifunza, ambapo watoto hulazimika kuanza shule kabla ya madrasa jambo ambalo hurudisha nyuma maadili ya Uislamu. Katika wimbo ufuatao muna methali inayosema:

“Mtoto akitaka soma mpelekeni Qur-ani kwanza”

Kwa kumaanisha elimu ya kwanza anayotakiwa mtoto wa Kiislamu aipate ni “Qur-ani na si jambo la busara kupelekwa shule kwanza,”wimbo unaofafanua

“Jungu la uji, jungu la uji

Halipwagi, halipwagi

Hata likipwaga

Lapwagia mahaba,

Mtoto akitaka soma,

Mpelekeni Qur-ani kwanza”

Hivyo wimbo huwo umetumia methali ya mtoto akitaka soma mpelekeni Qur-ani kwanza,ili kutoa mafunzo kwa jamii ya Kiislamu kuwa iwaanzishe watoto kujua elimu ya dini yao kwanza kabla ya lolote. Hata katika upande wa watafitiwa walipoulizwa walikiri kuwa ni ukweli kuwa mporomoko wa maadili sasa umepungua katika dini ya Uislamu kutokana na watoto kutoshirikishwa kikamilifu kumjua muumba wao.

Aidha, katika maisha ya kila siku inaonekana kuwa, kuna maisha ya watu ambao hali zao ziko juu na wale ambao hali zao za kimaisha ziko chini. Lakini binaadamu anatakiwa asishangae kumkuta mtu ambae yuko juu akajikuta ana hali ya chini na yule ambae yuko chini akawa na hali ya juu. Wote huu ni uweza wake Allah (s.w) katika wimbo ufuatao unadhihirisha hayo ya methali isemayo “*Aliye juu mnganje chini*”. Ndani ya wimbo wa Njuguni lembwe;

“ *Njuguni lembwe*

Njuguni lembwe

Aliye nyuma, atangulie mbele

Wa usoni twende”

Hapa methali ya “alie nyuma atangulie mbele” imetumika kuitanabaisha jamii kuwa mtu hatakiwi kujivuna kwa kipato alichonacho kwani hajui ni wakati gani aliyekupa atakupokonya .na hata baadhi ya watafitiwa walipoulizwa kuhusiana na suala hili, walikiri ukweli na wakatoa mifano ya watu hao.

4.3.1.2 Matumizi ya Misemo

Maendeleo ya TUKI (2004:273) na Manya (2006:1) yanabainisha kuwa misemo ni fungu la maneno linalotumiwa na jamii ya watu fulani kwa namna maalumu ili kutoa maadili. Misemo hutumiwa ili kupata mafunzo mema kwani masuala yanayojitokeza katika maisha ya kila siku hujidhihirisha pia katika fasihi ya jamii.

Kwa mfano, katika jamii zetu tunamoishi wazee wamezoea kuwalea watoto wao kwa kuwapenda mno jambo ambalo linamfanya asahau kuwajenga katika maadili ya kimajukumu katika familia, mpaka wazee hao wanakuwa katika hali ya uzee na

watoto umri wao wa kujijenga na hayo unakaribia kuisha ndio mzee anawakumbusha kana kwamba kasahau kufanya hivyo.kwa mfano nyimbo ifuatayo inaonesha haya .

“Watoto wangu eeee

Mimi mama yenu, eeee

Sina nguvutena eeee

Za kuua simba, eeee

Simba ni mkali, eeee

Anaua baba, eeee

Anauwa mama, eeee

Anauwa shangazi, eeee

Anauwa kaka... eeee”

Hapa msemo wa “simba ni mkali” umetumika kuwatanabahisha watoto wasijipweteke kuwategemea wazazi kila siku, na baadae wahamasike katika kujitengenezea maisha yao wenyewe ili waepukane na ukame ndani ya jamii. Hapa “samba” limetumika kama “njaa”, na kwamba baba na mama hawana tena nguvu za kupambana nayo, hivyo watoto wanatakiwa wajengwe mapema kujua wajibu wao katika maisha ambapo jamii inaanishwa na kutanabahishwa katika maisha yao ya baadae.

4.3.2 Matumizi ya Tamathali za Semi

Tamathali za semi ni vifananisho au viwakilishi vyta dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazolingana. Tamathali za semi hutumika kwa ajili ya kupanua, kupuuza, kubadilisha maana za dhamira au maana za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu iliyokusudiwa na mtunzi. Dhima ya kutumia tamathali za semi ni

kupanua, kuyakinisha, na kuipa uhai na uhalisi zaidi dhana inayoelezwa. Wakati huo huo matumizi ya tamathali za semi huburudisha na huzindua akili na huacha athari ya kudumu katika hisi na mawazo ya hadhira.

Kwa upande mwengine Kahigi anasema tamthali za semi kimsingi hutumika kuhamisha maana ya kawaida inayonekana, kwa mfano matumizi ya taashiri, sitiari, majazi, ishara, isitiara, na kadhalika. Kwa maana nyengine Kahigi anafafanua kuhusu matumizi ya tamathali kuwa ni uwasilishaji wa maana kwa njia iliyotolewa kupidia kejeli, chuku, kikinzani. Maana inayonekana huwa sio lengo la mtunzi mpaka uihakiki na kuihusisha na mambo kadhaa kama vile utamaduni na historia ndipo utapata kilichokusudiwa na athari yake kwa hadhira. Katika nyimbo za michezo ya watoto tamathali za semi zimetumika kwa wingi kwa malengo mbalimbali yakiwemo ya kitafsida, kibalagha, kitashbiha na mengineyo kama yaonekanavyo hapa chini.

4.3.3 Matumizi ya Tauria/ Tafsida

Gibbe (1980:95) amefasili Tauria kuwa ni tamathali za semi ambayo husema mambo kwa lugha laini inayambatana na kuchora na kuonesha hisia za watu. Senkero (2011: 18) anasema Tafsida ni aina ya tamathali ambayo hujitokeza kwa matumizi ya maneno, misemo au nahau ambayo hupunguza ukali au matusi badala ya kutumia lugha ya uwazi.

Katika jamii za waafrika yapo baadhi ya mambo hasa yanayohusu viungo vya uzazi na mambo ya mapenzi huwa ni mwiko kuyataja hadharani maneno haya yanapotajwa hadharani jamii humuona mtu aliesema kuwa amekengeuka maadili na hana heshima mfano katika wimbo ufuatao unaonyesha jinsi mtoto wa kike anavyoona haya mbele

ya wazazi wake kutamka suala la mapenzi. Pia anaona haya kumwambia mpenzi wake kuwa yuko katika hedhi, hivyo anatumia tamathali hii kupitia wimbo ufuatao.

“Kinyuli nyulika

Mwanangu mwanajumbe

Kavaa nguo mbili

Yatatu kaibandika

Kakasi na ulimbo

Alie juu naaushe”

Walipohojiwa baadhi ya watafitiwa kuhusu wimbo huu, walisema ni kweli kuwa msichana huyu baada ya kutembelewa na mpenzi wake kwa kutoonana nae siku tatu nyuma aliogopa wazazi wake, kwa kitendo cha kwenda kinyume na mila na desturi za jamii ya Wapemba. Kwamba msichana kama hajaolewa ni miiko kuleta mwanamme nyumbani kwao. Ili kukwepa adhabu aliamua kuwakusanya watoto na kuwapanga mikono yao mmoja juu mmoja chini na kuanza kuimba wimbo huu kwa kumtanabahisha mpenzi wake kuwa amedharurika (yuko katika miezi) na ndio maana akawa hamuoni. Hapa tafsida **kakasi na ulimbo aliye juu na ushe** imetumika kuadilisha jamii juu ya kuenda kinyume na mila na desturi ya jamii ya Wapemba.

Pia matumizi ya Tafsida katika nyimbo za michezo ya watoto inaonekana katika wimbo ufuatao wa **Yai bovu**, ambao huimbwa na watoto katika michezo yao ya kila siku.

“Yai bovu, yai bovu,

Linanuka, linanuka,

*Linanukaje, linanukaje,
Mh, Mh, Mh, lishachacha,
Mh mh mh lishachacha”*

Katika jamii ya Wapemba aghlabu watu huwa wanastiriana katika baadhi ya mambo, mathalani mtu kaenda shughulini akaonekana kajipura lakini wakati huo huo kunguni akawa anatambaa kwenye mtandi wake, basi wenzake huona taabu kumuambia muhusika moja kwa moja, hivyo huweza kumtumilia mtu wake wa karibu kupeleka ujumbe. Na kupidia wimbo huo unafafanua kuwa, kawaida msichana anapokuwa kwenye hedhi huwa ananuka kama hatozingatia masuala ya usafi ambapo hapo kale watafiti wanassema msichana ambae alikuwa ananuka kupita kiasi, kumbe msichana yule yumo kweye siku na wala hajisafishi kwa wakati, ndio maana wasichana wenzake wakacheza mchezo wenyewe wimbo huo bila ya mwenyewe kujua lakini mwisho alibaini.

4.3.4 Matumizi ya Balagha

Tamathali hii hutia chumvi kuhusu uwezo wa viumbe, tabia zao na kuhusu sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha au kusisitiza (Senkoro 2011:12) .pia Mulokozi na Kahigi (1979) wametoa dhima ya balagha kuwa ni kuongeza utamu na kuleta athari fulani.

Kupitia wimbo ufuatao balagha inajitokeza hivi: Kuna mama ambae ana maziwa makubwa sana ambayo eti ye ye anapokwenda na maziwa nayo yanaburutika hivyo humbidi abiringishe maziwa kwanza na ye ye afuatie .hii ni balagha kwa sababu si rahisi hali kama hii kuweza kutokezea, kwa mfano wimbo ufuatao unafafanua.

“Mama njoo

Mama njoo

Nyumbani kuna wageni,

Mama njoo,

Mwanangu,

Mwanangu,

Mcheka kilema si mkwe wangu,

Mwanangu,

Bingiri bingiri, nikaone mkwe wangu.”

Hapa inaonekana kuwa ni balagha hii iliyotumika katika wimbo huu, lakini katika hali ya kawaida jamii inaadilishwa kuwa isiwe na tabia ya kuwacheka walemvu kwani wao hawakuomba. Walipohojwa watafitiwa, walisema kuwa wimbo huu aliuimba mama kumtanabahisha mtoto mwanangu atakaenicheka kwa sababu ya huu ulemavu wangu, basi huyo si mkwe wangu, na kweli mama alimkataa mkwe kwa sababu hiyo. Hivyo tunatakiwa tuachane na tabia hiyo kwani kuna msemo unaosema hujafa hujaumbika.

4.3.5 Matumizi ya Tanakali za Sauti

Tanakali za sauti ni mbinu itumiayo mwigo wa sauti ili kutoa picha au dhana ya kile kinachowakilishwa au kupambanuliwa na sauti hizo (Mohammed 2004). Katika suali la uchumba ndani ya jamii za Kizanzibari inatokezea kuwa mwanamume kaenda kuposa nyumbani kwao msichana husika, basi msichana huyo huulizwa jee unamtaka fulani? Basi kwa vile ni vigumu kwa enzi hizo mtoto mwari kujibu moja kwa moja kuwa anamtaka, basi hutoa sauti ya “Kilio” sauti ambayo huashiria kuwa

mchumba anamtaka. Na pia katika nyimbo za michezo ya watoto zipo tanakali za sauti nyingi tu ambazo hurejelea jambo fulani kwa mfano katika wimbo ufuatao.

“Mtoto alia × 2 mtoto alia ×2

Kampeleke, kampeleke

Kwa babaee kampeleke

Kwa mama yake kampeleke

Ng’uwang’u kampeleke

Shing’wa kampeleke “

Hapa ng’wangu na shing’wa ni mlion wa sauti ya mtoto mchanga unaoufuata ile miguu anayoitoa nje na kuibana. Kupitia tanakali hii ya sauti, jamii inapata kujifunza kuwa inatakiwa iwapatie watoto mazoezi ya viungo kwani mazoezi ya viungo ni njia mojawapo ya mtoto kujengeka kiafya.

Aidha katika wimbo ufuatao wa **mabata madogo madogo** unaonesha tanakali ya sauti ya mabata jinsi wanapokuwa katika sehemu wanazozipenda wanavofurahika, tanakali ambayo inaonesha kuwa mara nyingi viumbe wa aina mbalimbali hujisikia raha wanapokuwa huru katika kila hali,wimbo unafafanua.

“Mabata madogo dogo wanaogelea,

Wanaogelea, katika shamba zuri la bustani,

Wanapenda kutembea bila viatu, bila viatu,

Katika shamba zuri la bustani

Na mabawa yao yanalia kwa kwa kwa

Kwakwa X 4”

Kupitia wimbo huu jamii inapata kujifunza juu ya uhuru wa mtu ndani ya jamii kwamba siku zote mtu anapokuwa huru hususan katika maamuzi huishi vizuri, mathalani mabata wanapoliza mabawa yao wakiwa bwawani.

4.3.6 Matumizi ya Kejeli

Kejeli ni usemi ambao maana yake ya ndani ni kinyume chake na inabeuwa maana yake halisi. Kejeli hubeba kebehi, kwa maana ya kwamba kile kinachosemwa sicho kinachokusudiwa. Katika jamii nydingi za kiafrika muna watu ambao kawaida wanajigeuza kupe katika kuuma kunyonya na kukandamiza wenzao. Yaani wenzao wanajishughulisha na harakati za kujikwamua na njaa kama vile kulima, kushona nakadhalika lakini utakutia kuna watu wengine wamekaa tu hawana kazi yoyote na kusubiri kila kinachohangaikiwa na wenzao na wao wanakula bila ya aibu. Wimbo ufuatao kwa kutumia kejeli unasawiri haya.

“Mbangano, mbangano - mbangano

Twende msituni - mbangano

Nikaona kidege - mbangano

Nikamwambia kitege -mbangano

Bora ukitege wewe - mbangano

Nikaondoka nikakitega - mbangano

Nikamwambia kichinje - mbangano

Bora ukichinje weye - mbangano

Nikamwambia kichune - mbangano

Bora ukichune weye – mbangano

Nikaondoka nikakichuna – mbangano

Nikamwambia kipike – mbangano

Bora ukipike weye – mbangano

Nikaondoka nikakipika – mbangano

Nikamwambia njootule - mbangano

Huku ni kula, nifanye ×2”

Hapa kupitia wimbo huu inaonekana kuwa umetumika kikejeli zaidi ili kuwakejeli wale wote wenye tabia ya uvivu ndani ya jamii kuwa waachane na tabia hii kwani inarudisha nyuma ujenzi wa maendeleo ya jamii. Na pia baadhi ya watafitiwa walipohojiwa kupitia wimbo huu walikiri juu ya suala hili na wakatoa mfano wa kuwa mtu mwenye tabia hii huwa ni mzigo kwa familia.

Matumizi ya kejeli pia yamejitokeza katika wimbo unaofuata ambapo katika wimbo huu unaonesha ni jinsi gani watu wa visiwa vya Zanzibar walivyokuwa furahani baada ya kuondolewa kwa mkoloni aliekuwa akiwanyanyasa kwa muda mrefu. Kimetumika kiumbe sisimizi kama kejeli kwamba hata viumbi vidogo vidogo vilingia furahani kwa hili kama wimbo unafafanua:

“*Sisimizi wenda wapi*

Nenda huko matangani,

Aliekufa ni nani

Mzungu na baniani,

Raha waringia nini,

Shingo kipapatiko na ini,

Waringia nini

Shingo kipapatiko na ini”

Matumizi ya kejeli katika nyimbo hii yametumika kuyakejeli kutoweka kwa mkoloni ndani ya jamii za wazanzibari. Pia yametumika kuwakejeli wale binaadamu wanaoringa na kujidai labda kwa uzuri na kipato walichojaaliwa na Muumba kuwa haifai kufanya hivyo kwani viumbe wote wamekuja kwa udongo na watarudi kwa udongo na hata walipoulizwa watafitiwa karibuni wote walikiri hili.

4.3.7 Matumizi ya Sitiari

Gibbe (1980: 86) ameifasili sitiari kuwa ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha vitu viwili. Mlinganisho huu hufanywa kwa kudokeza tu. Vilevile Mulokozi na Kahigi wamefasiri sitiari kuwa ni uhamishaji wa maana na hisi kutoka katika kitu au dhana nyengine, vitu hivyo vinavyohusishwa kwa kawaida huwa havina uhusiano wa moja kwa moja.

Matumizi ya sitiari hijitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto kwa mfano kama inavyoelweka katika jamii, hususan jamii za kimasikini ambapo ndani ya familia muna mume na mke, kawaida mume ndie anaeshughulika ili mkono uwende kinywani kwa kufanya harakati za hapa na kule ilikupeleka mbele gurudumu la maisha.

Inapotokezea mume huyu kuondoka kwenda masafa ya mbali na pengine akachukua siku nyingi kurudi, mara nyingi mke huishi katika maisha ya taabu kwa sababu kashazoea kuchumiwa na mumewe na inatokezea chajio kilichoachwa nyumbani hakitoshi kukidhi siku alizoondoka mume huyo, hivyo mke hulazimika kuvumilia hali hiyo ili asitoe aibu au siri hiyo nje kama wimbo ufuatao unavyodhihirisha hayo:

“Kachiri kachiri ... saga

Mume wangu kasafiri ... saga

Kaniachia ukili ... saga

Upatao pima mbili... saga

Na kipande cha Hariri ... saga

Kachiri saga kachiri saga”

Hapa hali ya uvumilivu imefananishwa na kachiri kwani kachiri ni vigumu kuisaga katika harakati za kutafuta dawa kama ilivyo na ugumu subra kwa wanawake walio wengi. Hivyo jamii inaadilishwa iwe na subra na uvumilivu wakati wa shida. Aidha katika ulimwengu tunaoendanao sasa inaonekana vitu kama vile njaa, umaskini, ukame na mfumuko wa bei za vitu unazidi kupamba moto kadiri. Siku zinavyoenda mbele, jambo ambalo huwafanya wazee kuwasomesha ikiwa pamoja na kuwahamasisha watoto wao wapigane na dhiki kama hii.

Katika nyimbo za michezo ya watoto sitiari kama hizi zimetumika kushajihisha jamii na jambo hilo kama wimbo unavyofafanua:

“Watoto wangu ee,

Mimi mamaye, ee

Sina nguvu tena , ee

Za kuuwa simba, ee

Simba ni mkali ee

Anaua baba, ee

Anaua mama, ee

Kupitia wimbo huu pametumika sitiari “simba” kuonesha jinsi vitu kama njaa na kadhalika vilivyohatari katika maisha ya binaadamu. Hivyo jamii inaadilishwa kufanya kazi kwa bidii ili kupigana na njaa.

4.3.8 Matumizi ya Tashbiha

Gibbe (1980:86) ameifasili Tashbiha kuwa ni tamathali ambayo hulinganisha vitu viwili kwa kutumia viunganishi linganishi mbalimbali, mfano katika wimbo unaofuata matumizi ya tashbiha yamejitokeza kama hivi ifuatavyo.

“Nasaka mke wangu, nasaka mke wangu

Hapa hayupo, hapa hayupo

Kenda wapi, kenda wapi

Kenda kwa msusi, kenda kwa msusi

Ruhusa kampa nani, ruhusa kampa nani

Kapewa na msusi, kapewa na msusi

Yeye kama nani, yeye kama nani?

Aaaaa..., hatuui, aaaa....hatuja”

Hivyo kupitia wimbo huo tamathali ya tashbiha imetumika ili kutanabahisha jamii hususan akina mama kuwa si vizuri kujifanyia mambo bila ya ruhusa za waume zao, hata kama huo urembo unatia kwa ajili ya mume lakini jambo zuri na la sharia uage kwa mume na ndivyo dini ya Kiislamu inavyotaka.

Vile vile matumizi ya tashbiha yamejitokeza katika wimbo ufuatao, ambapo katika wimbo wenyewe unafafanua zaidi kuhusu elimu na umuhimu wake. Katika jamii zilizo nyingi inaaminika kuwa elimu ni bahari, elimu ni nuru ya kumuangazia

mwanadamu na maisha yake. Pia elimu ni ufunguo wa kufungulia maisha ya mwanadamu, kwa njia hii wazazi wanatakiwa wasiwanyime watoto wao haki ya kupata elimu, wimbo unafafanua hilo:

*“Baba na mama msinikataze,
Kwenda skuli kusoma,
Elimu ya sasa kama chai moto,
Ukinywa upulizie,
A, e, i, o, u, ...”*

Hapa, tashbiha **kama** imetumika kuonesha ni jinsi gani ilivyo ngumu sasa kupata elimu inayofaa, hivyo wanahimizwa wazee wafanye kila hali wafatilie namna ya kupata elimu bora kwa watoto wao na sio wakae tu. Hata mtafitiwa ambae ni mwalimu wa shule ya Mzambarauni alikiri hili kwa kutoa methali moja inayosema “Mtaka cha mvunguni sharti ainame”.

4.3.8 Matumizi ya Tashhisi

Kwa mujibu wa Tahakiki na vitabu Teule kidato cha 5 na 6 (2005) wamefasili Tashhisi kuwa ni mbinu ya kisanaa ambayo hutumika katika kazi za fasihi ambayo hutumika kuonyesha vitu visivyo na sifa ya kibinaadamu hupewa sifa ya kibinaadmu kwa lengo kuonesha ujumbe fulani.

Katika nyimbo za michezo ya watoto, mbinu hii imetumika kwa malengo mbali mbali mathalani kuonesha uwezo wa Allah (saw), katika wimbo ufuatao unafafanua:

*“Nani kaona upepo, nani kaona upepo,
Si mimi wala si wewe, si mimi wala si wewe*

*Unapopita chini yamti, chini yamti, majani hupeperuka,
Majani hupeperuka... ”*

Hapa upepo umepewa uwezo wa binaadamu wa kutembea sehemu moja na nyengine, ambapo wanajamii kuitia wimbo huu wanatanabahishwa juu ya uwezo wa Allah (saw), kwamba mionganii mwa vitu ambavyo Muumba kaviumba vyenye manufaa ya binaadamu ni upepo ambapo wanajamii wanatakiwa kutanabahi juu ya hili.

4.3.9 Matumizi ya Takriri

Kwa mujibu wa vitabu teule Kidato cha 5 na 6 (2004) Takriri imefasiliwa kuwa ni mbinu ya kisanaa ambayo hutumika kurudia rudia maneno ama silabi katika tungo. Mara nyingi mbinu hii hutumika kuonesha msisitizo wa jambo linalokusudiwa, mathalani katika wimbo ufuatao unadhihirisha haya.

*“Kijani cha mperani, labeka bwana,
Twenzetu mpirani, siwezi bwana,
Huwezi una nini nina mimba bwana,
Umepewa na nani? ni Hasani bwana,
Mwambie akutoe, Hawezi bwana,
Hawezi ana nini ana homa bwana,
Mwambie ale dawa, ni chungu sana
Mwambie ale pipi, we! ni tamu sana.”*

Hapa msamiati “bwana” umeonekana kujirudiarudia kwa lengo la kuonesha msisitizo wa alie fanya kitendo kile kuwa ni mvulana ambae anataka ujauzito

utolewe lakini msichana kaonekana kuwa na msimamo, na kuitia wimbo huu wasichana wanatakiwa wawe na msimamo katika swali hili, kwani utoaji wa mimba ni hatari wanaweza hata kupoteza maisha ya watu.

Aidha matumizi ya takriri yamejitokeza katika wimbo ufuatao kwa lengo la kuonesha msisitizo wa jambo husika. Kupita wimbo huo viumbe mbali mbali wanatakiwa watafakari na kutanabahi kwa kina juu ya uwezo wa Allah (sw) kwamba kutokana na uwezo huo, kaumba vitu mbalimbali ulimwenguni ambapo vinatumika katika maisha ya kila siku, na vitu hivo basi, kavigawa vyenye uhai na visivo na uhai wimbo unafafanua hilo:

*“Vitu vyenye uhai, vitu vyenye uhai,
Watu, wanyama na miti x2
Visivyo uhai, visivyo uhai, meza, kabati, na kitit,
Visivyo uhai, visivyo uhai, ni meza kabati na kitit.*

Hapa Takriri ambayo imejitokeza katika wimbo huu, inaweka msisitizo zaidi juu ya mgawanyo wa vitu katika ulimwengu ambapo wanajamii wanapata kuadilika juu ya uwezo wa Allah [s.w]. Na watafitiwa kama vile Maalim Ali wa Pandani alionesha msisitizo juu ya hili.

4.3.10 Mtindo wa Kutaja Majina ya Vyakula

Majina ya vyakula ni mionganini mwa usanii uliotumika kuitia nyimbo za michezo ya watoto. Vyakuka kama vile mbogamboga, samaki, nyama, maziwa nakadhalika, hivi ni aina ya vyakula ambavyo mwanadamu anatakiwa avipate ili kujenga afya bora kama wimbo ufuatao unavyofafanua:

*“Chakula bora, chakula bora
 Hima tumieni, aaa tumieni,
 Tuleni chakula bora, masihara tuacheni,
 Tuepuke madhara na maradhi mwilini,
 Mboga, maziwa, nyama, uwanga hata maini.
 Chakula bora chakula bora,
 Hima tumieni, aaaa tumieni, hima tumieni”*

Hapa jamii inaadilishwa umuhimu wa chakula bora katika kujenga afya njema ndani ya maisha ya kila siku kwani kuna msemo usemao “mwili haujengwi kwa matufali”. Hivyo wanajamii wanaaswa hata kama ni masikini, basi waone umuhimu wa kupanda mbogamboga ambazo zinasaidia katika kujenga afya ya binaadamu kama vile mtoriro, matembere na kisanvu.

Aidha, mtindo huu umejitokeza tena katika wimbo ufuatao, ambao umetaja na kuonesha vyakula vya aina ya nafaka, kuonesha kuwa mionganini mwa mazao ya nafaka ambayo yanalinwa katika jamii ya wapemba, ndizi ni mionganini. Wimbo unaafafanua.

*Baba uyo, atoka shambani,
 Na mkungu wa ndizi, Baba uyo,
 Tukampokeeni, tukampokeeni,*

Katika wimbo huu jamii inapata kuadilika juu ya heshima ya watoto kwa wazazi wao, ikiwemo kumpokea mzigo wakati anaporudi safari. Lakini mtafiti aliwasikia watafitiwa walimu takribani katika shule zote, wakilalamika juu ya kuporomoka kwa

heshima za watoto ndani ya jamii ya wapemba, yote hii imesababishwa na kuwa watoto hawachezi tena michezo kama hii ambayo ndani yake huwa muna nyimbo zenyenye maana kama hivi. Lakini ukweli ni kwamba nyimbo hizi zina faida yake kwa wanajamii husika.

4.3.11 Mtindo wa Daiolojia

Majibizano ama daiolojia ni mbinu ya kisanii iliyotumika pia katika nyimbo za michezo ya watoto. Kwa mujibu wa tahakiki vitabu teule kidato cha 3 na 4 wanaeleza: Daiolojia ni majibizano ya ana kwa ana baina ya fanani na hadhira. Mara nyingi mbinu hii hutumika katika kazi za fasihi kwa lengo la kuleta maelewano mazuri kati ya wazungumzaji. Wimbo ufuatao unafafanua juu ya dhana hiyo:

“Nipeleke nipeleke, wapi

Kwa Juma Buda, Kwa Juma Buda kunani

Bijuma kafumaniwa, Kafumaniwa na nani

Bwana muuza mafuta, Ni nani kakwambieni

Ashura wa madebeni, aaaa mkamateni, aaaa mkamateni...”

Kupitia mtindo huo, hapa jamii inaadilishwa juu ya suala zima ya watoto wanaoharibiwa mitaani, hivyo wale wote ambao huhusika na matukio kama haya wanatakiwa wakamatwe wafikishwe kwenye vyombo vyaya sharia ili sharia ichukue mkondo wake. Katika kutilia mkazo hili, Maalim Ramlia wa Skuli ya Mzambarauni alisema ubakaji katika jamii ya Pemba umeengenezeka kwa sababu wale wote ambao wanahusika na uhalifu huu hawachukuliwi hatua zinazostahiki, na badala yake rushwa hutumika kuficha wahalifu hao lakini ukweli ni kwamba jamii inatakiwa ibadilike kupitia nyimbo hizi ili iweze kujenga jamii ilio bora.

Mtindo huu pia umejitokeza katika wimbo ufuatao, ambao unaonesha majibizano kati ya mnyama (tumbili) na binaadamu Katika majibizano haya yanaonesha kuwa ni marufuku kwa tunda ambalo limeshaliwa na mnyama kuliwa na binaadamu, wimbo unafafanua.

“Tumbili walani

Nala komamanga,

Nigiae name, nikampe mwanagwa,

Akija akifa jee

Nitatoa sanda na kombe la wanja,

Utanipa kibamba uwa, mate mate yauwa,

Utanipa kibamba uwa, mate mate yauwa”

Kupitia mtindo huu, ndani ya wimbo, kwanza jamii inapata kuadilika kuwa katika jamii ya Wapemba, kuna baadhi ya watu wanaweza kuongea na wanyama japo kwa lugha ya ishara. Pia jamii inaadilishwa kuwa isiwe na tabia ya kula vyakula ama tunda lililowachwa na wanyama, kwa Pemba matunda hayo huitwa “mabweke”. Kwa sababu ni hatari kwa afya ya binaadamu, kwani huenda kusababisha hata kifo.

Mtafitiwa wa shule ya Uondwe ambae ni maalim Abdalla Khalid, alitilia mkazo juu ya suala hili kwa kusema, ni vizuri kufannya hivyo ukizingatia katika kipindi hichi pana mripuko wa maradhi ya “**Ebola**” na jambo moja ambalo serikali imelipigia mbiu ni hili ili jamii ijkinge na maradhi ya “Ebola”, “Ukimwi” na maradhi mengineyo ya hatari.

4.3.12 Mtindo wa Kutumia Viumbe Wadudu

Mtindo wa kutumia viumbe wadudu, ni mionganini mwa mtindo uliotumika katika nyimbo za michezo ya watoto, ili kutoa ujumbe fulani, mathalani wimbo ufuatao umetumia kiumbe sisimizi kuonesha kama ni mionganini mwa viumbe wanaotumika katika jamii zetu kama wimbo unavyofafanua:

“Sisimizi wenda wapi

Nenda huko matangani,

Aliyekufa ni nani?

Mzungu na baniani,

Raha waringia nini, shingo kipapatiko na ini.

Waringia nini, shingo kipapatiko na ini.”

Katika wimbo huu, kupitia mtindo huu, jamii inapata kutanabahi kuwa, kumbe hata viumbe kama hawa kwa uwezo wa Allah walifarijika kuondoka kwa mkoloni katika visiwa vyta Zanzibar. Vile vile jamii ya wapemba inaadilishwa kuwa si jambo la busara binaadamu kujivuna kwa sababu binaadamu hamna kitu, Katika kutilia mkazo juu ya hili watafitiwa wa shule ya Msingi Pandani, walitilia mkazo juu ya hili la binaadamu kutojivuna na kuringa kwa kipato au uwezo aliopewa na Allah (sw). Hivyo jamii inatanabahishwa kwa hili.

4.3.13 Mtindo wa Utahoaji Maana

Mtindo huu umetumika katika nyimbo za michezo ya watoto, ambapo katika mtindo huu, lugha ya Kiarabu na Kiswahili imetumika katika kufafanulia maana hiyo, kupitia mtindo huu, jamii ya Wapemba inapata kuhakikisha kuwa kumbe ni kweli

wazanzibari walitawaliwa na wakoloni wa Kiarabu na wakaacha athari mbali mbali zikiwemo za lugha. Wimbo ufuatao unafafanua:

*“Ainakum tibil amsi, Ulikua wapi jana
Kuntum maridhwa, nilikua ni mgonjwa,
Alwaa jantu dawa, vipi ulipata dawa
Dawa jantum, hapana sikupata,
Bai-ash-rab maa, bali nilikunywa maji,
Allahu ya shafiy, mungu akaniponesha.”*

Hapa kupitia wimbo huu, jamii inapata kuadilika juu ya suala zima la matibabu ya kwamba kitu kidogo tu mtu linaweza kumponyesha kwa uwezo wa Allah (sw), na pia wanajamii wanatanabahishwa waachane na tiba za kiganga na badala yake wamkinai Allah [s.w] katika katika kila jambo.

4.3.14 Mtindo wa Kutaja Majina ya Miji na Mitaa

Mtindo huu umejitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto, ambapo kupitia wimbo ufuatao majina ya miji kama vile Dar es salaam yamejitokeza ili kuonesha kuwa kisiwa cha Pemba kimo ndani ya Tanzania. Watu kutoka Pemba huenda wakitembea Dar es salaam na kurudi kwa shughuli mbali mbali kama vile za biashara na kuwaona ndugu, jamaa na marafiki. Wimbo ufuatao unaonesha hilo:

*“Nilikwenda, nilikwenda,
Nalikwenda Daresalama, Daresalama, Daresalama,
Nikala, nikala,
Nikala wali kwa nyama x3*

Tonge ya kwanza,

Tonge ya kwanza ikanipita, x3

Tonge ya pili,

Tonge ya pili ikanipita x3

Tonge ya tatu,

Tonge ya tatu ikanipita x3

Kibibi, kibibi,

Kibibi kanipa maji x3

Kibwana, kibwana,

Kibwana kanitukana x4

Kwaheri nakwenda zangu, nakwenda zangu, nakwenda zangu”.

Kupitia wimbo huu, jamii inaadilishwa kuwa, inapokula chakula iwe na tabia ya kueka maji ya kunywa. Katika jamii ya kiislamu haifai kula bila ya kueka maji kwani nikinyume na taratibu zilizowekwa na dini ya uislamu. Jambo hili linaweza kusababisha madhara kwa binaadamu, mathalani mtafitiwa wa shule ya Mzambarauni Bi Ramla alitoa ufanuzi juu ya hili, kwa kusema kuna mtu mmoja enzi za masahaba alitolewa roho kwa kosa hili.

4.4 Dhamira Zilizojitokeza Katika Nyimbo za Michezo Ya Watoto

Msingi mkuu wa nadharia ya **uchambuzi matini** ni kwamba kazi ya Sanaa inapaswa ichambuliwe vipengele vya fani na maudhui. Kwa upande wa fani kupitia tasnifu hii umeonekana ufaishi uliojitokeza kama vile matumizi ya taswira, miundo mbali mbali, matumizi ya tamathali, pia imeonekana kuwa ndani ya nyimbo za michezo ya watoto muna dhamira nyingi ambazo zimesawiri maisha ya kila siku.

Kwa mujibu wa tahakiki ya vitabu teule kidato cha 5 na 6 (2005), na kidato cha 3 na 4 [2005]. Wamefasili dhamira kuwa ni jumla ya mawazo ambayo msanii hutaka yafike kwa wanajamii, ikiwemo kuelimisha, kuadilisha, kuburudisha, na hata kurekebisha jamii.

Miongoni mwa dhamira hizo ni kama vile:

- a) Uvumilivu na ujasiri,
- b) Heshima na nidhamu,
- c) Kutokujibika katika familia,
- d) Uhasharati,
- e) Kuepuka kiburi,
- f) Ruhusa kwa wanandoa,
- g) Uvivu,
- h) Mazoezi kwa watoto,
- i) Uweza wa Allah,
- j) Utigemezi,
- k) Kutotenda maovu kwa wengine,
- l) Adabu mzuri na usafi.

4.4.1 Dhamira ya Uvumilivu katika Ndoa

Dhamira ya uvumilivu imejitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto, uvumilivu ni ile hali ya mtu kufanya subira juu ya ugumu wa hali fulani katika maisha. Dhamira hii ya uvumilivu imejitokeza katika nyimbo nyingi tu za michezo ya watoto kama ifuatavyo:

Kuna wimbo wa “**kachiri**” ambao wimbo huu umetumika kitaswra zaidi kwa ajili ya kuonyesha uvumilivu na ujasiri anaotakiwa kuonesha mwanandoa pindi aondokewapo na mumewe aidha kwa kufiwa au kuondoka kwenda safari, kwani imezoleka kwa akina mama wahudumiwe kila kitu na waume zao, hivyo wanapoondoka ugumu wa kimaisha hubakia kwa akina mama, kwa hali hii akina mama wanatakiwa wavumilie. Wimbo ufuatao unasawiri hayo:

Kachiri kachiri.....saga

Mume wangu kasafiri.....saga

Kaniachia ukili.....saga

Upatao pima mbili.....saga

Nakipande cha Hariri.....saga

Hapata kuku nikamkaranga

Na pili pili na dawa ya manga

Kachiri saga, kachiri saga

4.4.2 Dhamira ya Ruhusa kwa Wanandoa

Data zinaonyesha kuwa katika dini ya Kiislamu ndani ya kisiwa cha Pemba mke anapotaka kuondoka ndani ya nyumba yake hata kama anaenda kwa jirani tu basi kwanza atake ruhusa kwa mume wake, tena ruhusa hiyo aombe kwa sauti nzuri, nyepesi, pole, na itakayomtoa nyoka pangoni.

Kutokana na hali za maisha sasa hivi, akina mama walio wengi wamejiingiza katika pirika za kimaisha mbalimbali kama vile vyama vyaya ushirika, biashara, Saccos mbalimbali na mambo mengine katika kupambana na maisha. Katika hali kama hii utamkuta mwanamke wakati mwengine anatoka bila ya ruhusa ya mumewe akija

anauliza mke yuko wapi? .Hivyo dhamira hii inalenga kuwataka akina mama wawe na tabia yakuomba ruhusa kwa waume zao wanapoenda safari. Wimbo ufuatao wa NASAKA MKE WANGU unafafanua:

*“Nasaka mke wangu nasaka mke wangu
Hapa hayupo na hapa hayuko
Kenda wapi kenda wapi
Kenda kwa msusi, kenda kwa msusi
Ruhusa kampa nani, ruhusa kampa nani
Kapewa na msusi, kapewa na msusi
Shanuo kampa nani Shanuo kampa nani
Kapewa na msusi, kapewa na msusi.”*

Kupitia wimbo huu jamii inaadilishwa (kina mama) kawaida ya kuomba ruhusa kwa waume zao pindi wanapoondoka majumbani kwao. Hata kama ameenda kutia urembo kwa ajili ya mume bac ni lazima apate ridhaa ya mume.

4.4.3 Dhamira ya Tabia ya Wanawake Kutochagua Waume

Data zianaonyesha kwa kupitia dhamira hii, imeonekana kuwa hapo zamani akina mama waliozeshwa waume bila ya kuulizwa kama unamtaka au la, na mara nyingi mtoto wa kiume huvishwa kanzu akaambiwa leo unaenda kumuona fulani. Baada ya watu kuingia ugeni (Sayansi na Teknolojia) hawataki tena kuchaguliwa wachumba na wazee wao, wanahisi kuwa wanayofanyiwa si haki, sasa imekuja mpaka kuwambiwa wasichana wasichaguwe waume kwa sababu wanaume wakuo ni wachache duniani na waliobakia wengi wanakwazwa na ugumu wa maisha au

mambo maovu kama vile zinaa, hivyo mume akija asirudishwe madamu tabia ni nzuri. Haya yanathibitishwa na wimbo wa MACHICHA ufuatao:

*“Machicha kutafute bwana
Akichelewa waume hapana
Wanawake tele wanaume hapana”*

Katika wimbo huu unawaadilisha wanawake kuwa watoto wa kike ni wengi sana duniani hivyo wasichague waume na pindi watakapofanya hivyo watakuja zikwa na nchi ila wazingatia taratibu sahihi pamoja na tabia njema.

4.4.4 Dhamira ya Tabia Njema

Data zinaendelea kuonesha kuwa katika kisiwa cha Pemba wazee huwalea na huwafunza watoto wao katika maadili mazuri ikiwemo tabia njema kama vile kutulia, kuwa na nidhamu, kuwa na heshima juu ya mkubwa au mdogo, kuwa na adabu, wapishi hodari na wasishughulike na maisha ya juu. Kwa kipimo hichi hapa mtoto huwambiwa kafunzika na kaleleka kwa maadili ya Kipemba, jambo ambalo humfanya mtoto mwenye tabia nzuri kama hizi kupata mume mapema na amtakae.

Na iwapo mtoto hakukulia katika maadili mema kama haya huambiwa hakufunzika wala kuleleka jambo ambalo humpelekea kukosa mume kwani waume wanaowa wanawake waliotulia na walioofunzika. *Mathalani wimbo ufuatao wa BUA unaafafanua:*

*“Bua ee watoto bua
Sha sham bio
Asha wako nani*

Wangu mimi Suleimani

Suleimani hakutaki

Amtaka mwanamwari

Apikae wali mwema

Apeleka barazani

Kwa Sefu bin Suleiman

Kitambi ni nguo gani

Haradua mrekani sha sham bio”

Hivyo kupitia wimbo huu, jamii inaadilishwa iwalee watoto wao katika maadili mema ili wapate waume walio wema mapema.

4.4.5 Dhamira ya Kuepuka Kiburi

Data zimebainisha kuwa kiburi ni ile hali ya mtu kujiona au kujidai kwa kipato alichonacho au uwezo alokuwa nao au jinsi alivyo. Hivyo katika jamii ya Wapemba huwa tuna kawaida ya kukatazana mtu asiwe na tabia hii, kwani anaepasa kuwa na tabia hii ni Allah pekee yake ambae ana uwezo juu ya kila kitu. Pia mtu hatakiwi kuwa na kiburi ama kujiona kwa kile amabacho Allah kamjaalia.

Kwani kama ni utajiri yeye ndio alokupa na hujui lini atakunyang’anya kumpa ambae ulimdharau, hivyo kwa kutumia methali ya “Aliye juu mngoje chini” wimbo ufatao wa NJUGU NI LEMBWE unafafanua:

“*Njuguni lembwe*

Njuguni lembwe

Aliye nyuma atangulie mbele

Wa usoni twende”

Hivyo kuitia wimbo huu jamii inafunzwa tabia ya kuepuka kiburi katika maisha ya kila siku. Dhamira hii pia imejitokeza katika wimbo ufuatao ambao nao unaonesha kuwa binadamu hatakiwi aringe kwa sababu hatuna cha kuringia kutokana na maumbile yetu yote yamemilikiwa na Muumba wa ulimwengu ambae ye ye ana uwemo wa kukitoa hicho binaadamu anachoringia na kumuacha mlemavu.kama wimbo ufuatao unavyofafanua:

Raha waringia nini

Shingo kipapatiko na ini,

Waringia nini

Shingo kipapatiko na ini

Hivyo kuitia wimbo huu, jamii inapata kuadilika juu ya kuepuka kiburi katika maisha ya kila siku ili jamii iishi kwa salama, upendo na mafanikio katika maisha yao.

4.4.6 Dhamira ya Mazoezi ya Viungo kwa Watoto

Katika makuzi ya mtoto hujumuisha chakula chenye lishe nzuri pamoja na mazoezi, kwa njia hii mtoto huonekana kuwa na afya njema na inayopendeza pia machoni mwa watu. Data zinaendelea kuonesha kuwa suala la mazoezi ya viungo pia limetiliwa mkazo kwa watoto wachanga ili wakuwe kimwili na kiakili na kamwe isijengeke ile tabia ya mtoto kumlaza kila wakati, hali hii inazorotesha maendeleo ya ukujaji wa mtoto. Haya yanadhihirika katika wimbo wa MTOTO ALIA ufuatao:

*Mtoto alia, mtoto alia, mtoto alia, mtoto alia
 Kampeleke, kampeleke
 Kwa mama ee, kwa mama yake
 Kampeleke, kampeleke
 Kwa baba ee kampeleke Kwa baba yake, kampeleke
 Ngwangu, kampeleke kwangu, kampeleke shingwa, kampeleke”*

Kupitia wimbo huu jamii ya kipemba inaadilishwa suala zima la mazoezi kwa watoto wachanga kwani “ngwangu nashingwa” ni mlio wa mtoto mchanga unaoifuata ile miguu anayoitoa nje na kuibana. Dhamira hii pia imejitokeza katika wimbo wa “**kanambia baba nichupe**” ambao katika mchezo wenyewe unavyochezwa unaonesha kuwa ni mazoezi tosha ya viungo kwa vile watoto hujirusha juu na chini, wimbo wa KANAMBIA BABA NICHUPE unafafanua.

*Kanambia Baba nichupe,
 Kama siwezi kuchupa,
 Chupu chupu chupu chupu*

Hivyo kupitia wimbo huu, wanajamii wa kipemba wanaadilishwa umuhimu wa mazoezi ya viungo kwa watoto wao na ndipo mtoto atakapokuwa vizuri. Mathalani watafitiwa wote walitilia mkazo juu ya suala hili hili ya kwamba mionganii mwa vitu vinavopelekea makuzi mazuri ya mtoto, ni mazoezi ya viungo yasiyo na athari kwao.

4.4.7 Dhamira ya Uweza wa Allah

Kupitia nyimbo za michezo ya watoto data zinaonesha kuwa dhamira ya uwezo na maajabu ya Muumba imejitokeza kwa sababu Allah (s.w) ana uwezo wa kufanya kila jambo ambapo mwanaadamu hawezi kufanya.

Mathalani mtu anapotizama jinsi gani mbingu na ardhi pamoja na nyota zilizotengenezwa atajua kuwa kweli Allah (s.w) anaweza na hashindwi kufanya chochote kile, hivyo Allah (s.w) hatakiwi kufananishwa na kiumbe chochote kwa sababu kufanya hivyo ni kumshirikisha yeye na shirki ni dhambi kubwa.

Katika wimbo ufuatao unaoneshwa ni jinsi gani Allah kazitandika mbingu zikiambatana na nyota na ambavyo nyota mara huwepo na mara hutoweka na kuonekana nyakati nyengine yote haya ni kudhihirisha nguvu na uwezo wake ni mkubwakama wimbo wa KITAMBAA CHANGU CHEUPE unavyofafanua:

Kitambaa changu cheupe

Kina madoa meupe

Kimeishi miaka mengi

Na kaka seifu abenduke, bendu

Nasote tubenduke, bendu

Bendu, bendu

Kupitia wimbo huu jamii inapata fursa ya kuadilika juu ya uwezo wa Allah (s.w) , kwani wimbo huu unazisifu mbingu jinsi zilivyo wakati wa usiku pia zinasifiwa nyota ambazo zimepewa jina la madoa meupe.

Data zinaendelea kuchambua na kuonyesha kuwa dhamira hii, imefafanuliwa tena katika wimbo wa **nani kaona upepo?** Ambapo kupitia wimbo huu, jamii inapata kuweka mazingatio akilini mwao juu ya ukubwa na uweza wa Allah (S.W) ya kwamba mionganini mwa vitu ambavyo vimeumbwa ulimwenguni ni upepo, upepo ambao unatumika kwa haja tofautitofauti, kama vile kuleta hewa nzuri, lakini la

kushangaza ni kwamba upepo hauonekani bali unaona tu raha katika mwili na majani kupeperuka kama wimbo wa NANI KAONA UPEPO unavyofafanua:

“Nani kaona upepo

Si mimi wala si wewe, si mimi wala si wewe

Unapopita chini ya mti, chini ya mti,

Majani hupeperuka”

Kupitia wimbo huu jamii inapata kujifunza na kutafakari kwa kina uweza wa Allah (S.W) na kuona kuwa pana haja ya kumtii yeye tu Muumba wa ulimwengu na vyote vilivyomo.

Vile vile, dhamira hii imejadiliwa tena katika wimbo ufuatao, ambao unaonesha kuwa kutokana na uweza alionao Allah (s.w) kaamua pia kubagua vitu ulimwenguni na kuviweka katika makundi mawili, nayo ni vitu vyenye uhai na vitu visivyo uhai, kama ambavyo wimbo unavofafanua.

“Vitu vyenye uhai, vitu vyenye uhai,

Ni watu wanyama na miti, ni watu wanyama na miti.

Visivyo uhai, visivyo uhai, Ni meza kabati Na kitit,

Visivyo uhai, visivyo uhai, ni meza kabati na kitit.”

Hapa wanajamii wanaadilishwa kuwa wasione vitu vilivyomo ulimwenguni vimejibagua tu wenyewe labda kwa usayansi alionao kiumbe, hapana wote huu ni uweza wa Allah (s.w). Na kwa upande wa watafitiwa walipoulizwa kuhusu hili walikiri ipasavyo.

4.4.8 Dhamira ya Kufanya Kazi kwa Bidii

Data zimeonesha kuwa katika nyimbo za michezo ya watoto, dhamira ya kufanya kazi kwa bidii imejitokeza ili kuweza kupambana na hali ya umaskini inayoambatana na njaa. Kupitia wimbo huu wanajamii hususan watoto katika familia wanaaswa waache utegemezi kutoka kwa wazazi wao na badala yake wajishughulishe na shughuli mbalimbali kama vile kutafuta elimu, kwani hao wazee ambao wanaowategemea iko siku watazeeka hivo wapi watakimbilia. Kwani kuna msemo usemao “Binaadamu si samaki” Kwani samaki kila akipea huzidi nguvu lakini kila binaadamu akipea anapungua nguvu kama wimbo ufuatao unavyofafanua:

“ *Watoto wangu ee, ee*

Mimi mama yenu, ee

Sina nguvu tena, ee

Za kuwa simba, ee

Simba ni mkali, ee

Anaua baba, ee

Anaua mama, ee

Anaua dada, ee.....”

Hivyo kupitia wimbo huu jamii inaonywa kuachana na tabia ya utegemezi na badala yake ifanye kazi kwa bidii ili kujijengea maisha bora.

4.4.9 Dhamira ya Kuepuka Utugemezi katika Maisha

Data zimeonesha kuwa utegemezi ni dhamira nyengine ambayo inajitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto ili kuwabidiisha wanajamii wafanye kazi kwa bidii na waepukane na utegemezi katika maisha. Kwani imeonekana kuwa ndani ya jamii

muna watu wamejigeuza kupe ambapo hutegemea kupata kila kitu kutoka kwa wenzao, hali hii inatanabahisha katika nyimbo za michezo ya watoto kuwa si nzuri kupitia wimbo ufuatao.

“Chura mwana unaerukaruka

Funga ng’dbe twende zetu kwetu

Farahani si mtumwa wetu

Chura, chura, chura.”

Kupitia wimbo huu jamii inaadilishwa na kutahadharishwa juu ya suala zima la kuepuka utegemezi kwa kila kitu kutoka kwa watu wengine, hali hii si nzuri kwani inarudisha nyuma maendeleo ya wanajamii.

4.4.10 Dhamira ya Kutowajibika katika Familia

Data zimeonesha kuwa kutowajibika katika familia ni dhamira ambayo pia imejitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto, hii hutokana na kuwa akina baba waliowengi baada ya kipindi fulani, pengine baada ya kushazaa watoto wengi, baba hujiona hapati mda wa kustarehe na mkewe hivyo huamua kutafuta kimada chengine ili apate kustarehe nae.

Kwa hali hii humlazimu kile anachokipata akipeleke kwa kimada huyo kwa lengo la kujiridhisha huku akiwaacha mke na watoto nyumbani wakiteketetea. Hali hii kwa jina jengine huitwa “Utelekezaji wa familia”. Katika wimbo ufuatao wa KIBUZI unadhihirisha haya:

“Kibuzi, kibuzi cha meme, cha meme

Mtoto wa mbuzi kajamba

Kajambile mchunga

Mkono tindi na wende Makka

Ukachukue jambia na upanga

Kuku, simba kalegea

Kalegea kawa mkongwe

Mkongwe kama Mwanamize

Jitu lisilo akili halijui kitu

Kwake hakushughuliki amba

Ashughulikia kwa mwanamke wanje

Du, funika paja lako mama

Keshokutwa nitakuja mama

Usiseme nakutukana mama

Nakufunza uwe mtu

Kwa kibakuli cha nyama mama”

Hapa kupitia wimbo huu, jamii inapata kuadilika kuwa waachane na tabia ya kuteketeza familia majumbani kwani, uwepo wa jambo hili ni hatari kwa maisha ya kila siku, njaa nakadhalika vinaweza kujitokeza ndani ya familia husika.

4.4.11 Dhamira ya Madhara ya Tabia Mbaya

Data zimeonesha kuwa madhara ya tabia mbaya kupitia nyimbo za michezo ya watoto, zaidi wanakusudiwa watoto wa kiume na wa kike ambao wana tabia ya kuchezewa miili yao kwa aidha kufanyiwa kwa makusudi kitendo kibaya au kubakwa; kwani imeonekana kuwa ulimwengu sasa umeja watoto wa aina hii ambao huwa hawaoni tabu yoyote kufanya kitendo hichi. Hivyo kupitia nyimbo za

michezo ya watoto jamii inazidi kupatauelewa juu ya madhara ya kitendo hichi kwa wanajamii kama wimbo huu wa BAMBA unavyobainisha:

“Bamba *Bamba !Bomba*

Umenipiga mpini wa kata

Na hivi sasa mashuzi mbwata, mbwata,

Bingina”

Hivyo wimbo huu unawakataza watoto kutofanya mambo mabaya kwani matokeo yake ni kuharibika, hususan wasichana ambao hutakiwa wakutikane wazima (bikra) watakapoolerwa, kwani iwapo msichana ataolewa, kwa utamaduni wa kisiwa cha Pemba, na akakutikana mtoto huyo hayuko bikra basi mtoto au mwanamke huyo huweza kurudishwa kwao (kuachwa/ kupewa talaka) mapema mno. Hivyo wimbo unaadilisha umuhimu wa tabia njema kwa wanajamii ikiwa ni pamoja kwa wanawake kutunza heshma yao kabla na hata baada ya kuolewa.

4.4.12 Dhamira ya Uvivu

Data zimeendelea kuonesha dhamira ya uvivu kwamba inawezekana kuzungumzwa kwa mapana sana katika nyimbo za watoto, mathalani kuna wale watu ambao katika taasisi za serikali au binafsi ambao hufanya uvivu mpaka wakasahau majukumu yao ya kazi, au uvivu wa majukumu ambao pengine mtu anamtegemea mwenzake hata katika shughuli za mapishi, anataka apikiwe. Hivyo hii si tabia nzuri kwa sababu kama ni mfanyakazi ofisini kwa tabia hii unachokipokea sio halali yako, na kama ni mwanafunzi hutofanikiwa katika masomo au kama ni nyumbani hutopata maendeleo ya aina yoyote ile kama wimbo wa MBANGANO MBANGANO unavofafanua hapa chini:

“ *Mbangano, mbngano, mbangano*
Twende msituni, - mbangano
Nikaona kidege, - mbangano
Nikamwambia kitege - mbangano
Bora ukitege wewe - mbangano
Nikamwambia kichinje - mbangano
Bora ukichinje wewe - mbangano
Nikaondoka nikakichinja - mbangano
Nikamwambia kichune - mbangano
Bora ukichune wewe - mbangano
Nikaondoka nikakichuna - mbangano
Nikamwambia kipike - mbangano
Bora ukipike wewe - mbangano
Nikaondoka nikakipika - mbangano
Nikamwambia njoo tule - mbangano
Huku ni kula nifanye, Huku ni kula nifanye”

Kupitia wimbo huu jamii inaadilishwa iachane na uvivu, kwani uvivu ni kikwazo cha ujenzi wa jamii mpya.

4.4.13 Dhamira ya Malipo ya Uovu

Data zimeonyesha kuwa siku zote katika maisha uovu hulipwa kwa uovu na wema hulipwa kwa wema. Kupitia nyimbo za michezo ya watoto pia dhamira ya malipo ya uovu imejitokeza ambapo kupitia dhamira hii, jamii inaonywa kutowafanyia wenziwao uovu au ubaya wa aina yoyote, kwasababu wewe unaefanya ubaya huo

kwa mwenzio uhakikishe utalipwa hata kama umetenda kwa siri au dhahiri, inawezekana wewe hutolipwa moja kwa moja lakini anaweza akalipiziwa mtoto wako au mjukuu wako au jamaa yako. Haya yanaelezwa na wimbo wa KADIA ufuatao:

*“Nipeni kisu na wembe - kadia
Nilichinje domo langu - kadia
Na hilo domo si langu - kadia
Kipanga anakuja, akija na aje - kadia
Nikikosa kuku japo jogoo nitamkamata – kadia”*

Hivyo kupitia wimbo huu jamii inaaswa kutowafanyia uovu wenzetu kwani pindi tukiwafanyia uovu na kama watatukosa watalipiza kisasi kwa jamaa zetu. Dhamira ya uvivu pia imejitokeza katika wimbo wa HAKUNA GOGO PUMBAVU ufuatao:

*“Hakuna gogo pumbavu - hoyo
Linaloshinda la mnazi - hoyo
Ukilipiga mashoka - hoyo
Ndani kwa ndani liwazi – hoyo
Muna wingi wa watwana
Na wingi wa wajakazi
Shikeni jembe mlime
Kipakacha nikumbatie bwana
Naona baridi sana”*

Hivyo kupitia wimbo huu watu wanakatazwa uvivu na badala yake wafanye kazi kwa bidii kama vile kulima, ili wapige vita umasikini.

4.4.14 Dhamira ya Usafi

Data zimeonehsha kuwa dhamira ya usafi pia imejitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto, katika kufafanuliwa dhamira hii,ni kuwa inashajihisha jamii izingatie suala zima la usafi unaweza ukawa usafi wa mazingira. Na usafi unaweza ukawa usafi wa mwili, roho na mazingira ya jamii, katika kuanya hivyo maradhi mengi tu yanawezekana yakapungua kama vile kipindipindu, Ukimwi nakadhalika, wimbo ufuatao wa FAGIA UWANJA unafafanua::

“Fagia uwanja peupe

Panga wanao bisada”

Hivyo kupitia wimbo huu jamii inaadilishwa suala la usafi. Dhamira ya usafi pia imejitokeza katika wimbo ufuatao ambao unaonesha kuwa usafi ni muhimu hata katika miili ya wanaadamu, kwasababu kawaida jinsia ya kike ikifikia umri fulani huwa ina tabia ya kutokwa na hedhi kila mwezi, hivyo katika hali hii wasichana wanatakiwa wajiveke katika hali ya usafi ili wasitoe harufu mbaya kwa wenzao. Na iwapo itatokezea msichana kuwa na tabia ya uchafu katika siku zake basi huambiwa kwa njia ya fumbo kama wimbo unavyofafanua:

“Yai bovu, yai bovu,

Linanuka, linanuka

Linanukaje, linanukaje,

Mh, mh, lishachacha, mh mh lishachacha”

Hivyo kupita wimbo huo, jamii inaadilishwa iachane na tabia ya uchafu kwani iwapo msichana atakua na tabia hii atakua hadumu ndani ya ndoa. Mtafitiwa mmoja ambae ni mwalimu wa skuli ya Pandani Maandalizi aliongezea kwa kusema: Kawaida

wazee wa Kipemba huwa na tabia ya kuwafunza watoto wao suala la usafi ili wasiwafedheheshe siku ya ndoa na wasijifedheheshe wenyewao kwa waume zao.

Wimbo ufuatao wa KICHUPA unasisitiza usafi kwa wanandoa, mathalani imezoleka kwa wanandoa hususan katika jamii ya kipemba kwamba msichana anapotaka kuolewa mionganini mwa mambo ambayo hufunzwa ni suala la usafi kwa mume wake ili wapate kudumu katika ndoa na katika usafi huo ni kulala na mme wake akiwa amejitia manukato kama vile haliudi, vikuba, mafuta mazuri na mapambo mengine yenyeye kumvutia mume.

Kichupa, kichupa,

Cha mafuta mazuri,

Ukilala, chanukia vizuri,

Wasichana chanukia vizuri

Kupitia wimbo huu, wanandoa katika jamii wanaadilishwa kudumisha usafi katika ndoa zao ili wadumu katika ndoa.

4.4.15 Dhamira ya Umuhimu wa Chakula Bora

Data zimeendelea kufanua kuwa katika jamii zetu kuwa, ili mtu aweze kuishi vizuri basi afya njema ni muhimu. Na ili mtu awe na afya njema, basi anatakiwa ale vyakula vizuri, kama vile, mboga mboga, maziwa, nyama, samaki na hata maini. kwani kuna msemo unaosema mwili haujengwi kwa matufali .mathalani, hata mtoto mdogo, ili akue vizuri ni budi mama mzazi azingatie umuhimu wa vyakula hivi kwa mtoto wake.Haya yanafafanuliwa kupitia wimbo wa CHAKULA BORA ufuatao:

*“Chakula bora, chakula bora,
 Hima tumieni, aaa tumieni, hima tumieni,
 Tuleni chakula bora, masihara tuachenzi,
 Tuepuke na madhara, na maradhi mwilini,
 Mboga, maziwa na nyama, samaki pia maini
 Chakula bora, chakula bora,
 Hima tumieni, aaa tumieni, hima tumieni”.*

Hapa jamii inaadilishwa kula vyakula vya mlo kamili ili kujenga na kuimarisha kiwiliwili. Aidha katika kutilia mkazo dhamira hii, kupitia mlo kamili pia watoto hupelekea kupata nguvu za kuwashangiria viongozi wao wanapokuja kuwatembelea nchini, mathalani wimbo ufuatao unawashajihisha watoto wanywe maziwa ili wawe na furaha muda wote na atakapokuja Raisi wawe na hamu ya kumshangilia.

Wimbo wa WATOTO WADOGO unafafanua.

*“Watoto wadogo,
 Kunyweni maziwa,
 Akija Raisi,
 Muruke ruke kama njija stop”.*

Hapa kupitia wimbo huu jamii inaadilishwa tabia ya kunywa maziwa katika kujenga afya. Walipoulizwa baadhi ya watafiti kuhusiana na hili, walifafanua kuwa uwezo wa kununua maziwa hawana, lakini Mtafiti aliwapa moyo kwa kuwambia angalau wapande mboga mboga za majani ambazo hazihitaji gharama kubwa.

4.4.16 Dhamira ya Madhara ya Mama wa Kambo

Data zinaonesha kuwa katika jamii, mapenzi ya mtoto hasa yako kwa mama mzazi. Ikitokezea bahati mama yule kuondoka aidha kwa kufariki au kutalikiwa basi baba ni budi aowe, kwa njia hii mtoto hulazimika kulelewa na mama wa kambo. Na inaaminika hasa kuwa mama wa kambo huwa hana huruma kwa watoto wa mume, hivyo katika hali hii mtoto hujikuta anateswa, ananyanyaswa na kudhalilishwa na baadhi ya mama wa kambo. Wimbo wa NAJUTA unafafanua:

*“Najuta, aaaaaa
Kukaa, aaaaaa
Na mama, aaaa
Wa kambo, aaaaa,
Anitesa, anitesa uyo, anitesa anitesa uyo.”*

4.4.17 Dhamira ya Umuhimu wa Elimu

Data zimeendelea kutoa ufanuzi kuwa elimu ni ufunguo wa maisha. Hivyo wazazi ama walezi wanatakiwa wafanye bidii zote katika kuhakikisha mtoto anapata elimu iliyo bora, na sio kumfutika ndani tu akawa anafanya mambo yasiyomuhusu kwasababu bila ya elimu hakuna mafanikio yatakayopatikana duniani na akhera. Pia katika kutafuta elimu, asichaguliwe ni elimu ya aina gani na hatua mbalimbali zichukuliwe kuhakikisha mtoto anapata elimu. Wimbo wa BABA NA MAMA unafafanua

*“Baba na mama, msinikataze
Kwenda skuli kusoma
Elimu ya sasa kama chai moto*

Ukinywa upulizie.....

a, e, i, o, u.....”

Hapa jamii inaadilishwa wasiwanyime watoto fursa ya kupata elimu kwasababu elimu ni nuru ya maisha.

4.4.18 Dhamira ya Utoaji Mimba

Data zimeonyesha kuwa kupitia nyimbo za michezo ya watoto, dhamira hii pia imejitokeza.kwa sababu utoaji wa mimba ni kitendo ambacho kimeshamiri ndani ya jamii zetu, mathalani utamkuta mtoto wa kiume anaamua kufanya mapenzi na msichana kwa makusudi, halafu msichana huyo akipata mimba, mvulalana hutoa wazo la kuitoa mimba kama wimbo wa KIJANI CHA MPERANI unavofafanua:

“ *Kijani cha mperani, labeka bwana,*

Twenzetu mperani, siwezi bwana

Huwezi una nini ? Nna mimba bwana

Umepewa Na nani ? Ni Hassani bwana,

Mwambie akutoe, hawezi bwana

Hawezi ana nini? ana homa bwana

Mwambie ale dawa, ni chungu sana

Mwambie ale pipi, we Ni tamu sana.

Hapa jamii inaadilishwa kuwa wasichana wasiwe rahisi wanapoambiwa na wavulana watoe mimba, wanatakiwa wakatae kwani madhara yake ni makubwa sana. Aidha, katika wimbo huu jamii inaadilishwa juu ya umuhimu wa kula dawa kwa wagonjwa

ili kupunguza ama kuondoa kabisa kasi ya maradhi yaliyomsakili mtu, ubeti wa mwisho wa wimbo huu huu unafafanua:

'Mwambie ale dawa,n ichungu bwana

Eti ale pipi,we!ni tamu sana'

4.4.19 Dhamira ya Umuhimu wa Wakati

Data zimeendelea kufafanua kuwa katika jamii ya aina yoyote ile, kumewekwa kitu muhimu ambacho kinawaongoza wanadamu katika kufanya pirika zao za hapa na pale, kitu chenyewe ni ‘wakati’ kwani bila ya kuwa na wakati ulimwenguni, mambo yasingelikwenda sawa. Hivyo wanadamu tunaadilishwa kuujali wakati si tu katika aya za Qurani, bali mpaka kwenye nyimbo za michezo ya watoto.wimbo ufuatao wa KENGELE LIA LIA unafafanua.

“ Kengele lia lia, na saa zimefika

Mwalimu leo, tumbo laniuma,

Siwezi kusoma soma...”

Hapa kupitia wimbo huu jamii inaadilishwa kuzingatia umuhimu wa wakati katika sehemu yoyote ndani ya jamii, iwe ni msikitini, ofisini, mashuleniyuoni, mahakamani na hata nyumbani.

4.4.20 Dhamira ya Kuwa na Malengo katika Maisha

Data zimeendelea kuchambua kuwa katika maisha ya kila siku kila mwanadamu ana lengo lake la maisha ambalo kajiwekea, ndio maana utawakuta watu wanahangaika huku na kule lakini kila mmoja akiwa na lengo lake rohoni. Mathalani wanafunzi

aghlabu huwa wanasoma wakiwa na malengo tofauti tofauti, kama vile kuwa Rais, daktari, mwalimu, rubani, meneja wa kampuni fulani, professa, nakadhalika. Kwa njia hii utakutia elimu huwa inapewa kipao mbele kama wimbo wa DAKTARI SISI SISI unavofafanua:

*“Daktari sisi sisi, walimu sisi sisi,
Raisi sisi, Marubani sisi,
Wabunge sisi, Mashekh sisi
Makatibu sisi sisi, wenyewe viti sisi sisi
Tulivute dau la elimu, lisirudi nyuma nyuma.”*

Utafiti umegundua kuwa wimbo huu unaadilisha juu ya suala zima la kusoma kwa bidii ili kufikia katika lengo mtu alokusudia. Baadhi ya watafiti walisema kuwa wanafunzi waliowengi sasa hivi hawasomi kwa malengo na ndio maana hawatilii mkazo suala la umuhimu wa elimu. Mtafiti ameona mwenyewe katika shule ya Uondwe wakati alipokwenda kukusanya data watafitwa wengi wamekimbia masomo na kwenda pwani, lakini kupitia tasnifu hii jamii itajifunza kupitia nyimbo za watoto.

4.4.21 Dhamira ya Utiegemezi kwa Allah (s.w)

Data zimeonyesha kuwa katika jamii ya Pemba kwa vile asilimia kubwa ni waislamu, kutofanya jambo lolote lile bila ya kumtanguliza Allah [s.w], kwa ajili ya kutaka msaada kwake kwa jambo ambalo mtu analifanya, na hali hii imekuwa ni kama sehemu ya utamaduni. Mfano kwenye tendo la ndoa basi kwanza anatangulizwa yeye, katika safari, masomo na mengine mengi, kwani yeye ndie anaetaka jambo liwe na kama hataki basi haliwi, kwa njia hiyo ni budi waumini wa Dini ya kiislamu wamuombe.

Wimbo ufuatao wa SAFARI YETU unavofafanua.

*“Safari yetu, amba,
Ni ndefu sana, amba
Ina vikwazo, amba,
Vya kila aina, amba
Allah jalia amba, tufike salama,
Allah jalia amba, tufike salama”.*

Kupitia wimbo huo, jamii inaadilishwa ijenge tabia ya kumtegemea Muumba wa Mbingu na Ardhi katika kila jambo, au kabla ya kufanya jambo lolote lile kwani kufanya hivi ndiyo mafanikio ya jambo lolote alifanyalo mtu. Baadhi ya watafitiwa waliongezea kwa kusema, na ye ye mwenyewe [Allah], anasema: “niombeni nikupeni”, kupitia aya za Qur-ani mbali mbali.

4.4.22 Dhamira ya Onyo kwa Wanajamii

Data zimeendelea kuonesha kuwa katika jamii ya kipemba kwa baadhi ya watu kuwa na tabia ya kula matunda ambayo yameachwa na wanyama, nyumbani kwao mtafiti katika kijiji cha Pandani Wilaya ya Wete, matunda haya huita “mabweke ama manyeke.” Jambo ambalo kunbe lina madhara kwa wanajamii lakini inaonekana wanajamii hawa hufanya haya bila ya wao kujuu athari yake. Mathalani ni hivi karibuni tu Serikali nayo ilipiga marufuku ulaji wa matunda ya aina hii ili kujiepusha na maradhi mbalimbali kama EBOLA ambayo inasadikiwa kuuwa watu wengi, kumbe hata nyimbo za michezo ya watoto zinatoa onyo hili kama wimbo ufuatao wa TUMBILI WALANI unavyofafanua:

“Tumbili walani

Nala komamanga,

Nigiae name, nikampe mwanangwa,

Akija akifa

Nitatoa sanda na kombe la wanja,

Utanipa kibambaua, mate mate yaua,

Utanipa kibambaua, mate mate yaua

Hivyo kupitia wimbo huu, jamii inaonywa iachane na tabia ya kula matunda yashayoliwa na kuachwa na wanyama kama hao, kwani inatokezea kuwa mate ya wanyama wengine ni sumu kwa binaadamu, ikaja kupelekea madhara Fulani ama kifo kabisa.

4.5 Muhtasari

Kimsingi katika sura hii, mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na mchango wa nyimbo za watoto katika kukuza maadili ya jamii, uchunguzi katika mkoa wa Kaskazini Pemba wilaya ya Wete. Miongoni mwa mambo yaliyosawiri utafiti huu ni kama vile, mifano mbali mbali ya michezo ya watoto ambayo ndani yake muna nyimbo zenye maana, usanii ambao umejitokeza katika nyimbo za michezo ya watotokatika kuibua ujumbe na dhamira mbalimbali ambazo zimejitokeza katika nyimbo za michezo ya watoto ikiwemo kuadilisha jamii katika kutenda mema.

SURA YA TANO
MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Utafiti huu umechambua mchango wa nyimbo za michezo ya watoto katika kukuza maadili ya jamii, mfano katika jamii ya Wapemba. Nyimbo arubaini na mbili (42) ziliteuliwa na kuhakikiwa mashairi yake na kubainishwa mbinu zake za kisanii kama kuonesha jinsi fani ilivyochangia kuleta ujumbe. Utafiti umefanyika katika kisiwa cha Pemba na ulihusisha mkoja mmoja na wilaya moja na vijiji vitatu. Mkoa wa Kaskazini Pemba, wilaya ya Wete, ndani ya kijiji cha Pandani, Uwondwe na Mzambarauni.

5.2 Muhtasari

Tasnifu hii ilikusudia kujibu maswali yaliohusika katika utafiti huu ambayo ni:

Je, ni nyimbo zipi za michezo ya watoto zinazopatikana katika maeneo ya kisiwa cha Pemba?

Je, ni mchango gani unaopatikana kupitia nyimbo za michezo ya watoto ambazo husaidia kuibua dhamira mbali mbali?

Jee ni mbinu zipi za kisanii ambazo zimetumika ndani ya nyimbo za michezo ya watoto ambazo zilisaidia kuibua ujumbe?

Maswali haya yamepata majibu ya kwamba iko michezo mingi tu ya watoto ambayo ndani yake muna nyimbo zenye maana kama ambavyo mtafiti alizifafanua ndani ya sura ya nne, na kupitia nyimbo hizo jamii inapata kujifunza mambo mengi tu ya kimaadili na kiakili, ambapo nyimbo hizo hutumia mbinu mbalimbali katika kuibua ujumbe husika.

Kwa ujumla ukiangalia mbinu za kisanii zilizotumika ndani ya nyimbo hizi, utahisi kama ni za watoto kweli, lakini ukweli ni kwamba, ndio, nyimbo huimbwa na watoto ndani ya michezo yao lakini ujumbe unaopatikana katika nyimbo hizi unalenga jamii moja kwa moja, wakiwemo akina mama, akina baba, na hata watoto wenyewe.

Nyimbo hizi zimetumia sitiari, tamathali za semi, mitindo mbalimbali na mbinu nyengine za kisanaa kama vile takririni, tanakali za sauti, nakadhalika. Nyimbo hizo zimebeba dhana mbalimbali zinazowahu su watoto hao ndani ya kisiwa cha Pemba na kudhihaki baadhi ya mambo yanayoendelea kufanyika katika jamii, mfano wanaume kuenda kinyume na familia zao ikiwemo suala la ndoa. Na inaonekana wahusika hasa wa nyimbo hizi ni watoto wakiwa katika michezo yao, lakini ujumbe wa nyimbo hizi ni wa jamii mzima.

Kwa ujumla kwa mujibu wa Data zilizokusanywa kutoka uwandani, inaonyesha dhahiri nyimbo za michezo ya watoto, huimbwa na watoto wenyewe ndani ya michezo yao, watoto hao huanzia umri kati ya miaka 8-15 na aghlabu katika kipindi hichi cha uwepo wa Sayansi na Teknolojia (ugen). Nyimbo hizi watoto hawa huziimba wakiwa shulenii katika kipindi maalum cha michezo yao, ambapo walimu wao hubakia kuwatazama huku wakifanyakazi zao.

Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Pemba Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba, ndani ya vijiji vya Pandani, Uondwe, na Mzambarauni. Mkabala wa kinadharia uliotumika katika kukamilisha tasnifu hii ni kama vile: Nadharia ya Uchambuzi matini, Muingiliano matini na Nadharia ya Mwitiko wa msomaji.

5.3 Mchango wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu unadhamiria kuibua hisia na ari za wazee wa jamii ya Pemba kuona kuwa ipo haja ya watoto wao kuwatengea muda maalum wa kucheza michezo yao ya jadi ambayo ndani yake muna nyimbo zenyenye kutoa elimu kwa wanajamii kwa ujumla.

Pia kupitia utafiti huu tunaamini wanajamii kwa ujumla wao watakuwa tayari kujirekebisha kutokana na makosa ambayo aidha walikuwa wanayatenda kwa makusudi au bila ya wenye wao kujua. Hata hivyo, kupitia tasnifu hii, walimu wakuu washule mbalimbali za Pemba watakuwa tayari kuona ipo haja yakufanyika vikao shuleni vitakavoshajihisha muendelezo wa michezo ya watoto mashuleni.

5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulihusu mchango wa nyimbo za michezo ya watoto katika kukuza maadili ya jamii ya Wapemba. Katika kisiwa cha Pemba michezo ya watoto ipo mingi sana ambayo ndani yake muna nyimbo.

Katika utafiti huu zimefafanuliwa nyimbo chache kwani haikuwa rahisi kuchambua zote nakuonyesha mchango wake katika jamii. Hata hivyo zilizochambuliwa zimewakilisha nyingine, kwa ujumla wake nyimbo za michezo ya watoto katika tasnifu hii zimechambuliwa kwa kuzingatia nadharia ya uchambuzi matini, mwingiliano matini, na mwitiko wa msomaji. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa kufanyike tafiti katika wilaya nyengine ndani ya kisiwa cha Pemba kupitia nyimbo za michezo ya watoto.

Mtafiti pia amependekeza tafiti nyengine zifanyike katika bara la Afrika zinaohusu nyimbo mbalimbali kama vile za harusi, msondo, beni nakadhalika. Aidha mtafiti anapendekeza, kupitia hizi nyimbo za michezo ya watoto, ufanywe utafiti kuhusu muundo kipengele ambacho mtafiti hakukichambua.

5.5 Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa ufupi mambo yote yaliojadiliwa katika utafiti huu. Mambo yaliotafitiwa na mtafiti uwandani na maktabani, katika nyimbo zenyewe na wakati wa uchanganuzi. Mapendekezo ya tafiti yametolewa ili kuwa mwongozo kwa watafiti wengine wapate pa kuanzia.

MAREJELEO

- Andanenga, A. A. S. (2002). *Bahari ya Elimu ya Ushairi*. Ndanda: Benedictine Publications.
- BAKIZA, (2010). *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*. Dar es Salaam: TUKI
- Culler, J. D. (1982). *On Deconcentration Theories and Critisms after Structuralism*. New York: Comel University Press.
- Farsy, S. A. (1960). *Kurwa Na Doto*. Dar es Salaam: Easten African Publication.
- Farsy, S. A. (1965). *Ada za Harusi katika Unguja, Nairobi, Dar es Salaam*, Kampala: East African Literature Bureau.
- Finnegan, R. (1970). *Oral literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.
- Haji, A. (1992). *Uhakiki wa Fasihi Kidato cha Kwanza Zanzibar*. Zanzibar: E.W.W Mbweni.
- Haji, J. A. (1983). *Fasihi Simulizi*. Taasisi ya Kiswahili na Luga za Kigeni. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.
- Hamad, A. (2008). *Matumizi ya Ushairi na Muziki wa Kiswahili katika Maisha ya kila siku Pwani ya Afirka ya Mashariki*. Zanzibar: BAKIZA.
- Hussein, E. (1970). *Alikiona*, Nairobi, Dar: es: Salaam, Kampala: East African Publishing House.
- Kahigi, K. (1975). *Lugha katika vitabu vya Watoto*, Dar es Salaam: Kioo Cha Lugha, JUZ NA UK 21-34.
- Kin'gei, J. na Kisovi, S. (2005). *Misingi ya Fasihi Simulizi*, Nairobi: Focus Publications.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Age Intenational Publishers.

- Kristeva, S. (1980). *Desire in Lang and Semiotic Approches to Literature and Art.* New York: Colombia University Press.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili Nadharia, Historia na misingi ya Uuchambuzi. Dar es Salaam na Nairobi.* Dar es Salaam: Mture Education Publishers Ltd na Phoenix Publishers Ltd.
- Masamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili 500 BK hadi 1500 BK.* Nairobi: The Jommo Kenyatta Foundation.
- Mazigwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili na Utamaduni.* Nairobi. The Jommo Kenyatta Foundation
- Mohammed, S. M. (1967). *Nyota ya Rehema,* Nairobi: Oxford University Press.
- Mohammed, S. A. (1989). *Asali Chungu.* East African Publication.
- Mohammed, S. A. (1984). *Kina cha Maisha.* Nairobi: Longman Kenya.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi,* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Msokile, M. C. (1991). *Kunga za Fasihi na Lughha.* Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.
- Mulokozi, M. M. C. (1996a). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M. (1989b). *Tanzu za Fasihi Simulizi,* Mulika na. 21 uk 1-21.
- Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- Mwita, M. B. (2009). *Uhakiki wa Mtindo na Maudhui katika baadhi ya Tamthilia za Penia Mlama*. Dar es Salaam: Mulika JUZ 28 uk 1004-128.
- Mkwera, F. M. V. (1990). *Tamrini za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Omar, S. (2008). *Fasihi na Jinsi: Mfano kutoka Nyimbo za watoto Tanzania Kiswahili Juzu*. 71, uk 98-106.
- Oriedo, E. (2000). *Fani katika Riwaya za Shaban Robert*: Kusadikika, Utubora Mkulima na Siku ya watanzi wote. Hanningtone.
- Othman, S. Y. (2007). *Hullabies, Woman Writing Africa*, Nairobi: The Eastern Region the Feminist.
- Safari, J. A. (1993). *Harusi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Sengo, T.Y (1991). *Tungo za Pwani*. Dar es salaam, TUKI.
- Sengo, T. Y. (1995). *Itikadi katika Jamii za Kiswahili. Lughha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili* uk 27- 44.
- Senkero, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam. University Press.
- Senkero, F. E. M. K. (19983a). *Fasihi*. Dar es Salaam: Univesity Press and Publicity Centre.
- Senkero, F. E. M. K (2011b). *Fasihi*. Dar es Salaam. KAUTU.
- Senkoro, F. (2003). *Nadharia naTakiluki*. Dar es Salaam: DUP
- Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na NDAKI, Tanzania*, Mwanza: Serengeti Bookshop Mwanza.
- Stude, T. (1995). Language Change and Language Maintenance in the Island of Tumbatu, LUGHA, UTAMADUNI NA FASIHI SIMULIZI YA

- KISWAHILI uk 83-117. TUKI Chuo kikuu Dar es Salaam na Idara ya Taaluma za Asia ya Chuo Kikuu Hansinki.
- TAKILUKI, (1983). *Fasihi Simulizi Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* New York: University of New York.
- Wafufa, R. M na Njogu, K. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2003a). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008b). *Kazi ya Fasihi. Istilahi na nadharia*. Nairobi. Focus Publication Ltd.
- Wamitila, K. W. (2002c). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phonix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. na Balisidiya, M. (1979d). *Utafiti, Mbinu za Ukusanyaji Fasihi Simulizi na Hatma yake Lugha yetu*. Dar es Salaam: BAKITA

VIAMBATANISHO

Kiambatanishi 1: Nyimbo za Michezo ya Watoto

1. KINYULI

Kinyuli nyulika

Mwanangu mwana wa Jumbe

Kavaa nguo mbili

Wanakakasi na urimbo

Alieyuu naushe.

2. KACHIRI

Kachiri kachiri.....saga

Mume wangu kasafiri.....saga

Kaniachia ukili.....saga

Unaopata pima mbili.....saga

Na kipande cha hariri.....saga

Kachiri saga, kachiri ..saga.

3. SHAKA MKE WANGU

Nasaka mke wangu! Nasaka mke wangu!

Hapa hayupo na hapa hayupo

Kenda wapi! Kenda wapi!

Kenda kwa msusi, kenda kwa msusi

Ruhusa kampa nani! Ruhusa kampa nani!

Kapewa na msusi, kapewa na msusi

Shanuo kampa nani? Shanuo kampa nani?

Mafuta kampa nani? Mafuta kampa nani?

Kapewa na msusi, kapewa na msusi

Yasisi yankaraga sia yasisi yankaranga sia.

4. MACHICHA

Machicha katafute bwana

Ukichelewa waume hapana

Wanawake tele ,waume hapana.

5. SADA MBARAKA

Watoto muwagapi? x2

Ni wale wale Sada Mbaraka x2

Kilengelenge nitakuja - Mbaraka

Nije nchukuwe wangu - Mbaraka

Tunalalia tunalalia

Wanamchukua watoto wa Mmakonde

Wanamchukua wanamfikicha

Wanamchukua wanamfikicha.

6. SHA SHA MBIO

Bua ee watoto bua

Sha sham bio

Asha mume wako nani?

Wangu mimi Sulemani

Sulemani hakutaki anamtaka mwanamwari

Anayepika wali mwema, anayepeleka barazani

Kwa Seif bin Sulemani

Kitambi ni nguo gani

Nahiari Marekani sha sham bio.

7. NJUGUNI LEBWE

Njuguni lebwe

Njuguni lebwe

Aliye nyuma atangulie mbele

Wa usoni twende.

8. KITIKITI

Kitikiti cha mfaume

Kitikiti cha mfaume

Tukale nyama kwa mfaume x2

9. ZIKIRI

(Wanaume) Wanawake mnaokwenda kudhikiri

Waume zenu huwa wako wapi?

(Wanawake) Huwa wamelala, huwa wamelala

10. MTOTO ALIA

Mtoto alia x2

Kampeleke

Kwa mama yake

Kampeleke x2

Kwa baba yake kampeleke

Ng'uwang'u kampeleke

Shing'wa kampeleke.

11. KITANGO MALE MALE

Matango yaliyopangwa sawa sawa kudem

Huku mawili manne kudem.

12. KITAMBAA CHANGU CHEUPE

Kitambaa chanu cheupe

Kina madoa meupe

Kimeishi miaka mingi

Na kaka Seif abenuke – benubenu.

13. KIBUZI:

kibuzi, kibuzi cha meme, cha meme x2

Mtoto wa mbuzi kajamba

Kajambile mchunga

Dekedeke mwimbaji

Mkono tindi na wende Makka

Ukachukue jambia na upanga

Kuku Simba kalegea

Kalegea kawa mkongwe

Mkongwe kama Mwanamize

Jitu lisilo akili halijui kitu
 Kwake hakushughulikii
 Ashughulikii kwa mwanamke wa nje
 Du, funika paja lako mama
 Nakufunza uwe mtu mama
 Kwa kibakuli cha nyama mama.

14. CHURA:

Chura mwana unayerukaruka
 Funga ng'ombe twende zetu kwetu
 Farahani si mtumwa wetu
 Chura, chura, chura

15. BAMBA:

Bamba! Bamba! Bamba!
 Umenipiga mpini wa kata
 Na hivi sasa mashuzi mbwata, mbwata
 Bingiria.

16. MBANGANO:

Mbangano Mbangano - Mbangano

Twende msituni	-	Mbangano
Nikaona kidege	-	Mbangano
Nikamwambia kitege	-	Mbangano
Bora ukitege wewe	-	Mbangano
Nikiondoka nikakitega	-	Mbangano
Nikamwambia kichinje	-	Mbangano
Bora ukichinje wewe	-	Mbangano
Nikaondoka nikachinja	-	Mbangano
Nikamwambia kichune	-	Mbangano
Bora kichune wewe	-	Mbangano
Nikaondoka nikakichuna	-	Mbangano
Nikamwambia kipike	-	Mbangano
Bora ukipike wewe	-	Mbangano
Nikaondoka nikakipika	-	Mbangano
Nikamwambia njoo tule	-	Mbangano
Huku ni kula nifanye	x2	

17. HIKOSA FARANGA JIMBI TANGWIA:

Nipeni kisu na wembe - kadia

Niukate mdomo wangu - kadia

Na huo mdomo si wangu - kadia

Ni mdomo wa mkwe wangu - kadia

Kipanga anakuja; akija na aje - kadia

Nikikosa kuku japo jogoo

Nitamkamata

18. HAKUNA GOGO PUMBAVU:

Hakuna gogo pumbavu - hoya

Linaloshinda la mnazi - hoya

Ukilipiga mashoka - hoya

Ndani kwa ndani liko wazi - hoya

Muna wingi wa watwana - hoya

Na wingi wa wajakazi - hoya

Shikeni jembe mlime - hoya

Uvivu hauna kazi - hoya

Kipakacha nikumbatire

Bwana naona baridi sana.

19. KINYUKI KIPENYAPENYA:

Kinyuki kipenyapenya

Mzinga wa leo na leo mzinga

Leo nyama, nyama ya ng'ombe.

20. FARIJALA:

Farijala wee Farijala

Umemuacha mkeo ndani

Unapita ukizunguka na ufyagio

Mama mbange mbange

21. MNARA WA NJIWA:

Watoto mnara, mnara wa njiwa

Akija baba nitkuja kumwambia

Sungura mweusi kaota mkia

Anayekosa atafinywa

Nitaka kwenda Bara, Bara

Kuna umande Bara

Ninataka kwenda Tanga, Tanga

Kuna jahazi inatoka Tanga.

(Umande ni majimaji yanayokuwemo kwenye majani wakati wa alfajiri kabla ya kuchomoza jua).

22. FAGIA UWANJA

Fagia uwanja peupe

Panga wanao Bi Saad

23. JUNGU LA UJI

Jungu la uji, Jungu la uji,

Halipwagi, halipwagi,

Hata likipwaga,

Lapwagia mahaba,

Mtoto akitaka soma, mpelekeni Qur-an kwanza

24. MAMA WA KAMBO

Najuta, aa! aa!

Kukaa, aa! aa!

Na mama, aa! aa!

Wa kambo, aa! aa!

Anitesa, anitesa uyo x3

25. MAZIWA

Watoto wadogo,

Kunyweni maziwa,

Akija raisi,

Muruuke ruke kama njiba stop.

26. WATOTO WANGU

Watoto wangu ee, Ee,

Mimi mama yenu, Ee,

Sina nguvu tena, Ee,

Za kuuwa simba, Ee,

Simba ni mkali, Ee,

Anauwa baba, Ee,

Anauwa mama, Ee,

Anauwa dada, Ee

27. SAMAKI

Nilimpata samaki, mkubwa mno,

Na wewe mwenye nguvu, kwanini ukamwachia,

Kanitafuna kidole, nalia iii mama nalia iii.

28 WAKATI

Kengele lialia, masaa yamefika x2

Mama leo tumbo laniuma, siwezi kusoma soma,

Walimu sisi, daktari sisi.

Tulivute dau la elimu, lisirudi nyuma nyuma.

29. KIJANI CHA MPERANI

Kijani cha mperani, Labeka bwana,

Twenzetu mperani, siwezi bwana,

Huwezi unani, ninamimba bwana

Umpewa na nani, ni Hasani bwana,

Mwambie akutoe, hawezi bwana,

Hawezi ana nini, ana homa bwana,

Mwambie ale dawa, ni chungu sana,

Mwambie ale pipi, we! Nitamu sana.

30. ELIMU

Mama na Baba, msinikataze

Kwenda skuli, kusoma

Elimu ya sasa, kama chai moto,

Ukinywa upulizieeeeeee,

a, e, i, o, u.....

31 **CHAKULA BORA**

Chakula bora, chakula bora

Hima tumieni, aaa tumieni, hima tumieni,

Tuleni chakula bora, masihhara tuacheni

Tuepuke na madhara, na maradhi mwilini

Mboga, maziwa na nyama,

Visibakie dishini,

Chakula bora, chakula bora

Hima tumieni, hima tumieni.

Kiambatanishi 2: Michezo Yenyewe Inavyochezwa

1. KINYULI

Kinyuli ni wimbo pia ni jina la mchezo wenyewe. Mchezo huu huchezwa na watoto wa kike na wakiume aghlabu ni watoto wadogo wadogo, ambao hukaa kitako chini na kufanya duara. Huweka mikono yao kila mmoja juu ya mwensiwe kwa kufinyana ile mikono. Wakati wanaimba wimbo huu wa ‘kinyuli’ huwa mikono hio inayogandana kwa kufinyana huipeleka juu na chini kufuatana na wimbo unavyoimbwa. Watoto wote huimba kwa pamoja. Wanapofika ‘na aushe’ yule mkono wake ulioko juu anaondosha, kwa hivyo unabaki mkono wake mmoja katika ule mchezo. Wimbo huendelea mpaka mikono yote imeondoshwa.

Hivyo hili ni fumbo lililotolewa na mwanamke kumhofisha mvulana (mpenzi) wake. Alikuwapo mvulana mmoja ambaye alikuwa na msichana aliyeenziwa sana kwao. Zilipita kama siku tatu pasi na kukutana. Hatimae mvulana alitoka kwenda kwa mpenzi wake na kuwa aliwaogopa mno wazee wake, hapo msichana aliwakusanya watoto wawili au watatu na kuwapanga mikono yao moja juu ya mwengine na kuwaimbia wimbo huo:

Muradi: E mpenzi wangu mwandani hakika mpenzi wako umpendaye Kadharuka. Yaani mwenzio nimo katika miezi, ndio maana usinione siku hizi. Ama sina nafasi ya kustarehe nawe na ufanye haraka kuondoka hapo ulipo.

2. KACHIRI

Wimbo huu unaimbwaa katika michezo ya ‘kachiri’, ambaao huchezwa na watoto wa kike tu. Huchezwa na watoto wawili wawili waliosimama na kuelekeana. Wakati wanaimba wimbo huu huwa wanasagasaga miguu juu ya ardhi.

Kachiri ni aina moja ya dawa ya tumbo. Ni dawa ya watoto wachanga nayo nayo husagwa kwenye mkungu na maji kidogo, tena ni gumu sana. Wimbo huu unamfunza mwanamke astahamili shida za mumewe akiondoka, aweze maisha ya shida kuisaga kachiri ambayo ni miguu. Pia mume anaweza kuondoka asimuachie nguo za kutosha kama mfano wa nyimbo inavyosema, ‘kipande cha hariri’. (kitambaa cha Hariri ni cheupe na laini).

3. SHAKA MKE WANGU

Shaka mke wangu ni wimbo unaoimbwa katika mchezo wenye jina hili la wimbo. Mchezo huu huchezwa na watoto wa kike tu. Watoto wote hujipanga duara ipokuwa wawili; mmoja hukaa ndani ya duwara na mmoja nje ya duwara. Wale waliofanya duara hukamatana mikono. Yule aliye nje ya duara hupita akipigapiga ile mikono na kusema. ‘Shaka mke wangu, shaka mke wangu! Na wote hujibu, hapa hayupo na hapa hayupo! Yule aliendani huwa anajificha ili yule aliye nje asimwone. Wanapofika kuimba ‘Yasisi yankaranga sia’, huwa wote wanazunguka mbio mbio na wale wawili huwa wanafukuzana kupita ndani na nje ya duara. Azma kubwa ni kufukuzana (kati ya mume na mke) ni kumkamata mke ndani ya duara.

Wimbo huu unamfunza mwanamke kutoondoka kwake bila ya ruhusa ya mumewe.

4. MACHICHA

Mchezo wa machicha na wimbo wake huchezwa na kuimbwa na watoto wa wanawake tu. Wanapocheza hujipanga msitari mmoja wakiwa wamesimama bega kwa bega wanaimba. Wanapofika ‘kiguru che che che! Wanarukaruka kwa mguu mmoja pamoja na kwenda mbele.

Maana ya wimbo huu ni kuwafanya wanawake wasichague wanaume wanapotakiwa kuolewa.

5. SADA MBARAKA

Wimbo huu huimbwa katika mchezo wa ‘Sada Mbaraka’. Aghalabu huchezwa na watoto wa wanawake tu. Wote hujipanga msitari mmoja bega kwa bega na kuelekea mbele. Mmoja hukaa kando. Huyu ndie anaeuliza, ‘Watoto mu wangapi?’ Baadae huenda kwenye ule msitari kumchukua mtoto mmoja mmoja mpaka awamalize wote wakati wimbo huu unaimbwa.

Wimbo huu unaelezea njinsi hapo zamani watoto wa visiwani walivyokuwa wakiwaogopa Wamakonde kwazole chale zao za mwilini. Watoto wakiamini kuwa Wamakonde wakiwachukua watoto, wakiwaficha na kuwala.

6. SHA SHA MBIO

Mchezo huu unatokana na wimbo unaoimbwa ‘sha sha mbio’. Huchezwa na watoto wakike na wakiume. Watoto hujipanga duara na kumatana mikono. Halafu mmoja huimba, ‘bua ee watoto bua! Wote huitikia, ‘sha sha mbio’. Halafu wote humuuliza

mtoto mmoja, mfano ‘Asha wako nani?’ Baadaye watoto wakiume yejote aliyemo kwenye lile duara hujibu. Huendelea hivi hivi mpaka wote wamalize.

Wimbo huu ukiimbwa wasichana wakati huo kwamba watoto waliokuwa wakiolewa ni wale ambao wametulia, adabu, waliokuwa wapishi hodari, na wasioshughulikia maisha ya hali ya juu.

7. NJUGUNI LEMBWWE

Huu ni wimbo pia ni jina la mchezo. Mchezo huu huchezwa na watoto wa kike tu. Hujipanga mmoja nyuma ya mwenzie, baadae wakifia kusema, ‘aliyenuma atangulie mbele’ yule wa nyuma huondoka na kwenda kukaa usoni. Huendelea kwenda na huku wakiimba mpaka yule aliyekuweko nyuma, mwanzo wa mchezo awe pale pale nyuma.

Wimbo huu una maana si hoja mtu kuwa maisha yake yako juu chini; maisha yanaweza yakanyanya ghafla. Kunyanya ghafla kwa maisha pia sio mwisho, kwani yanaweza yakarudi kama mwanzo.

8. KITIKITI:

Wimbo wa mchezo huu ni ‘kitikitii’. Mtoto mmoja hubebwa na watoto wenziwe wawili wakishikana mikono kwenye mabega sawa sawa. Aghalabu hawa wanaobeba huwa ni wenye afya. Mchezo hutegemea watoto waliopo kuanzia watatu. Wimbo huu ulikuwa na lengo la kutikuza ufalme wa utawala

9. ZIKIRI

Katika mchezo huu watoto wanaume hujipanga na wanawake hupita kwa kundi huku wanadhidikiri.

Wimbo huu una maana hapo zamani ilikua shida kwa wanawake kutoka bila ya ruhusa za waume zao, lakini hata hivyo wengine waliokuwa wakiweza waliondoka bila ya kuaga.

10. MTOTO ALIA

Watoto huchukuana na wimbo huu wa ‘mtoto alia’ wanapofika kusema ‘Ng’wang’u huenda kichura, lakini miguu huitolea nje na wanaposema ‘Shingwa’ miguu huitia ndani.

Ng’wang’u na Shing’wa ni mlion wa mtoto mchanga unaoifuata ile miguu anayoitoa nje na kuibana. Funzo hasa la mchezo huu ni kuwapa watoto mazoezi ya viungo kwani huendelea kucheza na kuanza kutoka mmoja mmoja mpaka anabaki mmoja wa mwisho ambae ndie mshindi.

11. KITANGO MALE MALE

Jina hili ni la wimbo na pia ni mchezo wenyewe. Mchezo huu huchezwa na watoto wa kike na wa kiume. Wote hukaa kitako chini na kunyoosha miguu. Wakati wanapoimba huwa wanasota huku na huku, wakipiga makofi kushoto na kulia kwa pamoja. Mwanzo huimba polepole na pia kusota kwao huwa ni kwa hali ya utaratibu, lakini baadaye huimba upesi na usotaji wao pia huwa ni wa mbio mbio. Yule anayebaki nyuma huzomewa.

Wimbo huu unampa mtoto mazoezi ya kimwili pale anaposota upesi upesi na pia kumpa mtoto mazoezi ya akili kwa kujua upande gani apige makofi, kufuatana na wenziwe. Pia ndani yake mna funzo la hisabu.

12. KITAMBAA CHANGU CHEUPE

Wimbo huu huimbwa katika mchezo unaochezwa na watoto wa kike na wa kiume. Wachezaji hujipanga duara na halafu wote huimba kwa pamoja. Jina la wimbo na la mchezo ni hili hili .wanapoimba kila mtoto hutajwa jina lalake kwa zamu na anapotajwa mfano “na kaka seif abenduke” basi mwenye jina hili hukisukuma nyuma kifua chake kwa nguvu. Mwisho wa wimbo husema ‘bendu bendu bendu’ ambapo huvisukuma nyuma na mbele vifua vyao kwa nguvu mpaka wachoke.

Wimbo huu unazisifu mbingu jinsi zilivyo wakati wa usiku. Pia zinasifiwa nyota ambazo zimepewa jina la madowa meupe.\

13. KIBUZI

Nyimbo ya mchezo huu ni kibuzi.watoto wote waliopo hukaa kitako na kunyoosha miguu. Mmoja ndiye anayeimba, “kibuzi kibuzi” na wengine wote huitikia “Cha meme cha meme”. Baadaye yule aliyeanza kuimba ndiye atakaye endelea na wimbo. Wakati anapoimba “kibuzi, kibuzi” huwa anaupeleka mkono wake mmoja kwenye miguu ya wenziwe. Anapoanza “mwana mbuzi kajamba” huligusa ufuti la mtoto mmoja wapo kwa kidole cha shahada na kuimba mpaka amalize wimbo. Mtoto anaeguswa hulala chali mpaka wote wamalizike. Halafu muimbaji husimama na kuwaambia, “watoto nyoka yuko mahali fulani” huendelea kutaja majina ya miji

mpaka uwaambie kuwa nyoka yupo hapo walipo. Hapo tena wote huruka na anaebakia kalala chini, huimba kwa pamoja; mwezetu kaliwa na nyoka". Hii ina maana, "mwenzetu mmoja ametafunwa na nyoka".

Wimbo huu unamlwaza mwanamke ambaye hashughulikiwi na mumewe wakati mumewe huyo anajishughulisha na mwanamke wa nje. Ananasihija kutokufanya ghadhabu za kukutaka vita. Badala yake astahamili na akubali kupokea anachogaiwa na majirani na asione anatukanwa.

14. CHURA

Hili ni jina la wimbo na ni jina la mchezo pia. Watoto wote waliopo hujipanga mstari, wakisha huchutama. Wanapofika mwisho wa nyimbo husema chura chura, huwa huku wakiruka kamavile chura anavyoruka.

Wimbo huu unawakataza wale watu wanaotegemea sana msaada kutoka kwa watu wengine, kwamba wajisaidie wenyewe; wasimtumaini mtu kwa kila kitu.

15. BAMBA

Jina la wimbo na la mchezo ni hilihili "Bamba". Watoto hukaa kitako chini na kuimba. "Bingiri" wote ubingiria kwa pamoja.

Wimbo huu unawakataza watoto kufanya mambo mabaya kwani matokeo yake nikuharibikiwa.

16. MBANGANO

Huu ni wimbo na mchezo wake una jina hili hili. Huchezwa na watoto wa kike na wa kiume. Watoto hujipanga mistari miwili huku wakielekeana. Huimba kwa kujibizana. Mwisho kundi moja hulifikuza kundi la pili na kulipigapiga kwa viatu vyovyote ambavyo haviumizi.

Mbagano ni jina la mtu. Wimbo huu unawakejeli wale watu ambao wanapenda kula bila ya kufanya kazi yaani, wanyonyaji.

17. HIKOSA FARANGA JIMBI TANGWIA

Katika mchezo huu ambao huchezwa na watoto wa kike na wa kiume watoto hujipanga halafu mmoja huwaelekea wenziwe, na kuanza kuimba halafu kuwafukuza wale wenziwe.

Wimbo huu unatuasa kutowafanya uovu wenzetu kwani, pindi tukiwafanya uovu wataka kutulipa na kama watatukosa, watalipiza kisasi kwa jamaa zetu.

18. HAKUNA GOGO PUMBAVU

Wimbo huu huimbwa na watoto waliosimama kwa mstari huku wasaga miguu kwenye ardhi. Wanapokuwa wanaimba wakifika “kipakacha nkumbatire bwana”, halafu wanagusana mabega kwa mikono upesi upesi.

Wimbo huu unakataza uvivu. Badala yake unahimiza kufanya kazi.

19. KINYUKI KIPENYAPENYA

Hili ni jina la wimbo na pia ni jina la mchezo. Watoto wawili hukamatana mabega na kuacha nafasi ili mtoto mwingine aweze kupita baina yao. Halafu wale wengine wao hujipanga mmoja nyuma ya mwenzake huku wakiwa wamekatana mabega. Baadae huimba huku wakienda kule waliko wale watoto wawili walioshikana mabega. Wakifika pale hujaribu kupita ambapo ambapo mmoja katika wao hukamatwa. Humo hukua kando na kumuuliza mfano, dhahabu na almasi anataka nini? Anapojobu kuwa amechaguwa moja wapo huekwa upande. Huendelea hivyo hivyo mpaka wote wamemalizika. Mwisho huweka makundi mawili na viongozi wao ni walioshikana mabega. Watoto wa kila kundi hushikana kwenye viuno halafu viongozi waoko mbele ndio waovutana. Watakao shindwa huimbiwa, “Simba kalegea” huku wanazomewa.

Wimbo huu unawafundisha watoto kuchagua kitu ambacho wanakipenda.

20. FARIJALA

Wimbo huu wa “Farijala” ambalo ni jina la mtu, pia ni jina la mchezo wenyewe. Mchezo huu huchezwa na watoto wa kike na wa kiume. Watoto wote hujipanga kwa mstari. Mmoja kutoka kuchuma majani marefu mti na kujifanya kama anafyagia huku wenziwe wanamuimbia. Wimbo unapofika “Mama mbange mbange” wote hurukaruka kwa shangwe na kumzunguka yule aliyekuwa akifyagia. Hufanya hivi kwa zamu.

Wimbo huu unakumbusha kwamba mwanamme lazima baadhi ya wakati amwache mkewe ndani (hata kama anampenda sana) ili akafanye kazi itakayowapatia riziki.

21. MNARA WA NJIWA

Mchezo huu wimbo wake ni huu “mnara wa njiwa”. Aghalabu mchsezo huchezwa na watoto wa kike lakini pindi wakitokezea watoto wa kiume ambao ni wadogo wadogo nao huruhusiwa kucheza. Watoto waliopo hukaa kitako na kujipanga duara. Kila mmoja huchukuwa jiwe moja analoweza kulifumbata mkononi. Mwanzo huimba tu ambapo kila mmoja hulichukua jiwe lake na kulipiga chini usoni pa mwenzake. Lakini jinsi anavyoliweka ni kama anaepiga makofi pale juu ya ardhi huku anafuata wimbo unaoimbwa. Kwa hivyo wote huyaweka yale mawe kwa pamoja. Hufanya hivi upesi upesi. Anayekosa mwisho wote hupiga na kumfinya, lakini kidogo tu bila ya kumuumiza.

Wimbo huu unawafunza watoto wawe na adabu mzuri, kwani, mtoto akiwa hana heshima huwafedhehesha wazee wake

22. FAGIA UWANJA

Wimbo ambao huimbwa katika mchezo huu ni “Fagia uwanja”. Mchezo wake huchezwa na watoto wa kike na wa kiume. Wote hujipanga duara. Wanapoanza kuimba, huenda mbele na kurudi nyuma kwa pamoja. Na wanaposema, “Fagia perupe”, wote huinama chini na kupeleka mikono yao huku na huku kama wanaofagia. Wanaposema, “Panga wanao Bi Saada”, hufunga mikono yao kama wanaopanga vitu mle ndani ya duara wakati wanafanya hivi, huwa wanakwenda mbele, wakirudi nyuma.

Wimbo huu unawafundisha watoto wawe safi na pia wayaweke mazingira yao katika usafi.

Kiambatanishi 3: Orodha Ya Wahojiwa

MAJINA YA WAHOJIWA	ENEO	TAREHE	WILAYA.
WANAFUNZI NA WALIMU WA SHULE YA MSINGI PANDANI.	PANDANI.	27/12/2014	WETE
WANAFUNZI NA WALIMU WA SHULE YA MSINGI MZAMBARAU TAKAO	MZAMBARAUNI .	05/01/2015	WETE
WANAFUNZI NA WALIMU WA SHULE YA MSINGI UWONDWE.	MTAMBWE.	15/01/2015	WETE